
# Vita vya Utambulisho

## Njia ya Uhuru



Adrian Ebens

# Vita vya Utambulisho

Adrian Ebens

Hati Miliki ©2018 Adrian Ebens
Kimeboreshwa kutoka toleo za awali
ISBN-13: 978-1-57258-668-0
Maktaba ya Congress Nambari ya Kudhibiti: 2011903965

Kiini cha dura (Duracell) ® kinamilikiwa na Procter & Gamble Co. na kusajiliwa Marekani na nchi zingine. Marejeleo ya Kiini cha dura ® katika muktadha huu yamefanyika kikamilifu kimfano kwa lengo la kuelezea, wala sio kuashiria kuidhinisha au uhusiano na chapa ya Kiini cha dura ®, au kampuni yake zali, Procter & Gamble.

Isipokuwa imeashiriwa mafungu yote ya Bibilia yametolewa katika tafsiri mpya ya mfalme Yakobo

Kimechapishwa na Maranatha Media

MARANATHA MEDIA

Fatheroflove.info
adrian@identitywars.org

# Yaliyomo


Sehemu 1. Falme Mbili – Utambulisho Uliopotea

1. Mti wa Kiini cha Dura ........ 5
2. Chemchemi ya Uzima ........ 12
3. Karibu na Moyo wa Mungu ........ 21
4. Ufalme wa Familia ........ 25
5. Mgogoro wa Famila ........ 29
6. Jahanamu Duniani ........ 34
7. Mstari wa Maisha ya Mbinguni ........ 42
8. Kulinganisha Falme Mbili ........ 49
9. Moyo wa Babeli ........ 53

Sehemu 2. Hatima Mmoja – Utambulisho Kurejeshwa

10. Kuvunja Minyororo ya (Kiini cha Dura) Duracell ........ 60
11. Kufungua Malango ya mbingu........ 68

Sehemu ya 3 – Safari ya Kurudi Kuwa Mwana

12. Maisha yanayo Wezeshwa na Kiini cha Dura. ........ 73
13. Ngazi ya kwenda Mbinguni ........ 77
14. Miungu Ifananayo, Majina Tofauti. ........ 82
15. Unasoma Jinsi Gani? ........ 89
16. Sio Mtumishi Tena ........ 93
17. Anguko la Babeli ........ 97

**Kitabu hiki ni ari kwa**

Babangu mpendwa Habeli, Ambaye
alinifunza kuwa jasiri, kuwa
mwaminifu daima, kumaliza
nilichoanzisha, na kutoruhusu
udhalimu

Mamangu mpendwa Evely, Ambaye
alinifunza kudumisha ndoto zangu,
kuwa mbunifu, kupenda maumbile,
na kuwa mkarimu

Dadangu mpendwa Karen, Ambaye
tulikua naye utotoni na mara nyingi
alitumia yaani yake kunifanya
kucheka

# Sehemu 1. Falme Mbili – Utambulisho Uliopotea

## 1. Mti wa Kiini cha Dura

Chumba kilikuwa na mwanga mdogo. Kwenye ukuta mmoja kulikuwa na mabango kadhaa, picha ya mwanamziki wa pop na nyingine ya mchezaji ambaye mara nyingi alihudumu kama dirisha katika utamanio wa uhalisia. Kwenye ukuta mwingine mlikuwa na dawati na vitabu vichache vya shule juu yake, lakini sura ya kati ya dawati hili mlikuwa mfumo mdogo wa stereo lakini wenye nguvu. Kwa kweli hiki kilikuwa chumba cha kijana ambaye alionyesha matarajio, msukosuko na ndio, ndoto.

Pambano kubwa lilikuwa kali moyoni mwangu, pambano la hatima, nukta ya ukweli. “Si kudhani ningefanya jambo kama hilo,” Nilinong’ona nikikazia macho sakafu. Dhana ya nafsi yangu ilikuwa inajaribiwa kwa ukali. Pambano lilikuwa kali sana kiasi ya kwamba nilitafuta farijiko kwa mabango yaliyokuwa yamenisaidia mara nyingi kabla ya kugeuza mawazo yangu kutoka kwa mazao niliyokuwa navuna sasa.

Anga lilijazwa na hisia ya kukata tamaa. Akili yangu ilikuwa inashika ishara ambazo zingetuliza hali yangu iliyosumbuliwa; Masomo, riadha, kueleza zilikuwa baadhi ya ishara nilizoshikilia, lakini sasa zilionekana kukosa nguvu za kunisaidia. Wingu la kugonjesha lilishuka juu yangu na likaanza kuondoa hisia zangu za tamaa ya makuu. Lilipiga teke na kufungua sehemu za moyo

zilizotuzwa na kuiba hazina zake, na kisha likafanya kwa chumba kitakatifu kwa vyote – matumaini.

Nilikuwa nimezungumza na mama yangu kwa namna niliyokuwa nimeahidi nafsi yangu sitawahi. Huu ndio mrija wa mwisho ulionifanya nitambue kuwa sikuwa mtu ambaye nilitaka kuwa. Sikujipenda, na nilitaka kubadilika, lakini ilionekana hakukuwa na matumaini.

* * *

Dhiki. Dhiki ni mojawapo ya laana kuu inayoharibu jamii yetu leo. Shirika la afya la ulimwengu linasema:

> Dhiki inaongoza katika kusababisha afya duni na ulemavu kote ulimwenguni. Zaidi ya milioni 300 ya watu wanaishi na dhiki hivi sasa, ongezeko la zaidi ya 18% kati ya 2005 na 2015.[1]

Jaribu kufahamu ubaya wa tatizo hili katika takwimu ya 2011 ifuatayo:

- Milioni 1 kujiua kila mwaka. Kifo kimoja kila sekunde 40 au 300 kwa siku.
- Kwa kila mmoja ambaye hujitoa uhai, aghalabu jaribu 20 zakufanya hivyo. Hiyo ni 60,000 kwa siku.
- Kote ulimwenguni, kiwango cha kujitoa uhai kimeongezeka kwa 60% kwa miongo mitano iliyopita – zaidi kwa mataifa yaliyoendelea.
- 60% ya kujiua kwote hutendeka katika Asia. China, India na Japan wanahusishwa na 40% ya kujiua kwote, kulingana na WHO.[2]

Nini kinachoendelea juu ya uso wa dunia? Nini kinachohuzunisha maishani kiasi ya kwamba mamilioni ya watu wanachagua kufa kuliko kuiona siku nyingine?

Katika kitabu chake "*The Mind Game*", Philipo Day anatupa kauli hii yenye kubeua sana:

[1]http://www.who.int/mental_health/management/depression/en/

[2]https://www.medicalnewstoday.com/articles/234219.php

> katika wakati uliopita, wanafamilia wenye kujali walikusanyika pamoja na kumpa ndugu aliyehuzunika hakikisho na makini ya kuzungumza mambo anayopitia. … Leo, na kuvunjika kwa umoja wa familia, kebehi za dini, na utengano wa familia nyingi kwa wekundu uliokithiri wa maisha ya karne ya 21. Uchunguzi wa kisaikolojia umechukua kazi ya uhauri ambayo ilikuwa ikifanywa na jamaa au wahudumu jirani. Ninaamini kwa kina kuwa hili limekuwa na athari za kufufua juu ya jamii.[3]

Philipo Day anaorodhedha sababu tatu: (1) Kuvunjika kwa umoja wa familia; (2) Kebehi za dini; (3) Utengano wa familia nyingi kwa wekundu uliokithiri wa maisha ya karne ya 21. Sababu kuu ni kuvunjika kwa umoja wa familia. David Van Biema akitoa maoni yake juu ya swala hili alisema yafuatayo:

> Kizazi tofauti na kingine kimekuja kuwepo, kimoja ambacho kwacho mamillioni wamekumbwa na huzuni kubwa ya kifo. Ni wana wa talaka. Wao tu katika mstari wa mbele wa vita vinavyoonekana kutokuwa na mwisho.[4]

Jim Conway katika kitabu chake "*Adult Children of Legal and Emotional Divorce"* anaelezea kwa uwazi maelezo ya uchungu na hasara inayo pitiwa na maelfu ya wale ambao wameteseka athari za familia zilizovunjika pengine kwa sheria au kihisia. Moja wapo ya sababu muhimu ambayo anaelezea ni ukosefu wa usalama na swali la kila wakati la "Mimi ni nani?" na "Ninafaa kupendwa?"[5]

Maswali haya yanaelekeza kwa chanzo hasa cha taharuki ya wanadamu – hisia ya maana. Je, mtu yeyote ananijali? Ninamaana yeyote? Maswali haya yalijiingizaje katika saikolojia ya mwanadamu? Kujibu swali hilo tunapaswa kurudi katika Mwanzo.

Ghafla Hawa alijipata akikazia macho mti waliokatazwa. "Mbona Mungu ametukataza kula tunda la mti huu?" alishangaa. Tunda lilionekana kuvutia sana, likimuonyesha kuenda mbele. Ghafla akasikia sauti ikitoka kwenye mti. Shetani,

---

[3]Philipo Day, *Introduction - http://www.campaignfortruth.com/Eclub/100702 /depressionandsuicide.htm*

[4]DavidVan Biema, "Learning to Live with a Past that Failed," People, May 29, 1989, p 79.

[5]Jim Conway, *Adult Children of Legal or Emotional Divorce*, (Monarch Publications, 1990) p 53.

akiona fursa hii, anamjaribu kupitia mtindo wa joka; "Ati hivi ndivyo Mungu alivyosema sema, 'Msile matunda ya miti yote ya bustani'?"[6] Shetani anamuongoza Hawa kujadiliana na pia kuweka shauku mawazoni mwake kuhusu uhalisi wa neno la Mungu. Ukweli kwenye mjadala wao na mantiki, Hawa hafai kwa Shetani. Ongeza kwa silaha hii isiyojulikana ya udanganyifu na giza, na mashindano yatakuwa makubwa kidogo kama Hawa ataonyesha nia ya kushiriki kwa kufungua kinywa chake.

'Matunda ya miti ya bustani twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio kati ya bustani Mungu amesema, 'Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.'"[7] Hawa alikubali mashindano kwa kurudia maneno ambayo Mungu alikuwa amezungumza, lakini sasa yuko katika tatizo la kina. Hamu yake mwenyewe, ikiunganishwa na kufungua mashindano kwa Shetani, kulimwacha bila kujiandaa kwa taarifa yake ifuatayo ya kuangusha taya, "Hakika hamtakufa."[8]

Umewahi kuwa na mazungumzo na mtu katika muktadha wa "urafiki" mnajadiliana na kisha unahisi kwa kiasi hauwezi kudhibiti hali hii hadi mpinzani wako aangushe kitu juu yako kuutoka "uwanja wa kushoto"? kitu ambacho hujawahi tarajia, kitu ambacho hutupaa kama uchafu katika ulainishaji wa mafuta uzungukao mawazoni mwako na kukusiaga kwa miguu? Sio kwamba kile walichokisema kilikuwa chochote chenye uzito mkubwa au kuangazia, lakini haukutarajia litoke kwao. Uwezekano wao kunenena maneno kama hayo kwa ujasiri na kwa hivyo halijawahi kutendekea.

Shetani, akiona kuwa amepunguza mwendo wa windo lake sasa kwa usahihi mkubwa analeta karibu pigo lake la ushindi. "…Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu,mkijua mema na mabaya."[9]

Mafungu haya machache yanaweza kuwa kama kupitia mji mdogo wa nchi; pepesa na utayakosa. Dhana ambayo Shetani aliingiza kwa Hawa ilikuwa na mbegu ya laana ambayo sasa inawapiga wana wote wa Adamu – pambano la

---

[6]Mwanzo 3:1
[7]Mwanzo 3:2,3
[8]Mwanzo 3:4
[9]Mwanzo 3:5

maana. Dhana ambayo inasikika kama ya kukomboa inatoa kiini hasa cha minyororo ambayo inawafanya wanadamu kuwa watumwa katika taabu na giza. Inasikika kama mkazo kidogo? Salia nami tunapoangazia dhana hii "Hakika hamtakufa," na tuangazie tunda lake na jukumu lake katika kusababisha maswali ya kunugunika, "Je, kuna mtu yeyote ananijali?" na "Ninafaa kupendwa?"

Nakumbuka nilipokuwa na umri wa kama miaka nane hivi, dada yangu alikuwa amepokea mwanasesere ambaye angelia na kucheka na hata kunywa maziwa. Kile ulichohitajika kufanya ni kuweka viini vya dura viwiili kwenye sehemu ya nyuma na aliweza kuendelea. Alimpa dadangu saa za burudani. Nilitaka kumpa mbwa amle kwa sababu kilio chake kilikuwa kimeanza kuudhi baada ya kipindi, lakini nikawaza njia nzuri kwa sababu sikutaka kumsikia dadangu akilia kwa saa nzima. Mtoto huyu alikuwa na uzima tu kwa kuweka viini vya dura viwili sehemu ya nyuma, na kwa kifupi hili ndilo wazo ambalo Shetani alikuwa akipitisha kwa Hawa. Hawa, hauhitaji kushtushwa na yale ambayo mtu mwingine anayasema, unao uzima ndani yako. Unaweza fanya utakavyo na hautapata madhara yoyote kwa sababu unao uzima ndani yako. Hakika hautakufa, na kadri utakavyo rudi hapa kwenye mti huu kuongeza kiini cha dura chako moto utakuwa sawa.

Unaweza fikiria mtoto wa umri wa miezi 18 akiwaambia wazazi wake, Nadhani naweza ishi kwa kujitegemea sasa, nilikuwa nazungumza na mbilikimo wa bustani shambani na anasema kwamba nina nguvu ndani yangu ambazo zitaniweka hai na kunikirimia mahitaji yangu yote, basi shukurani kwa usaidizi wako wote, na pengine tutakutana siku nyingine." Hili ndilo hasa lilitendeka kwa Adamu na Hawa katika bustani. Dhana *Hakika hamtakufa* ilikuwa imenyakuwa hisia zao za kumtegemea kikamilifu Baba yao wa mbinguni. Ilishambulia msingi hasa wa wale walikuwa binafsi. Ilichanganya hisia yao ya utambulisho na hivyo thamani yao kama wana wa Mungu. Mbona Adamu na Hawa hawangetambua kosa lao na wageuke katika nafasi ya kumtegemea kikamilifu Baba yao wa mbinguni? Natamani ingekuwa rahisi hivyo, lakini athari za dhana kwamba *hakika hamtakufa* kwa sababu mna nguvu ndani yenu wenyewe, hata kwa fursa ya pili, ina athari ya papo ya kukuzuia kurejea. Tutazungumza zaidi kuhusiana na hili baadaye, lakini kwanza, wacha turejee kwa tukio hilo la mti.

Tambua pendekezo la Shetani kuwa watakapokula tunda hili, kwa kiwango fulani macho yao yatafunguka kwa kiwango cha juu cha uwepo. Madai yao hapa sio tu kuwa mna nguvu ndani ya nafsi zenu, bali pia malighafi ya ulimwengu yana vitu vyenye nguvu, ambavyo mara tu unapo vimiliki, vinaweza kufanya uwe na nguvu hata zaidi. Karibu kwenye ulimwengu wa mali.

Katika Mwanzo 3:4,5, Shetani yuko katika wigo kamilifu la mbinu ya injili kushinda waumini kwa ufalme wake wa ndoto. Anatoa ufalme ambao unaahidi nguvu na kurudhishwa kwa wale wote watakao ukumbatia. Ufalme huu umewekwa katika misingi miwili mikuu:

1. Una uzima ndani yako ambao unakufanya kujitegemea kikamilifu kutoka kwa kitu chochote au utawala.

2. Mazingira yetu yana watu, vifaa na vitu ambavyo, kama tutavimiliki au kuhusishwa navyo, vinaweza tufanya tuwe na nguvu zaidi, kuangaziwa zaidi na kutosheka zaidi katika maisha.

Kupitia kwa mti huu wa ujuzi, Shetani alikuwa akitoa kuishi kunako pata nguvu za kiini cha dura; uzima usiohitaji chochote kutoka nje au utawala hivyo basi kichwa cha sura hii ni – mti kiini cha dura. Shetani anatwambia kwamba kiini cha dura za miili yetu zitadumu kama tutafuata falsafa yake katika maisha.

Ni muhimu kukumbuka kwamba Adamu na Hawa walipokula tunda la mti, hapakuwa na sumu asili iliyowafanya kuhofu, wadhambi au waasi. Bibilia inatwambia kuwa mti ulifaa kwa chakula.[10] Sumu ilikuwa maneno ya Shetani aliyoyasema kwa Hawa. Sumu ni kanuni ya ufalme wake. Baadhi ya watu walizua swali, "Mbona niteseke wakati Adamu na Hawa walikula tunda? Sikula kutoka kwa mti huo." Ukweli ni kwamba kila wakati tunapotenda kwa kujitegemea kwa Mungu, tunakula tunda kwa njia sawa na ile ambayo Adamu na Hawa walikula kwa sababu tumemeza sumu ya Ufalme wa Shetani. Kwa kweli, tutajifunza kuwa kweli tunakula kutoka kwa mti huu kila siku na tunateseka kuvimbiwa kwa kutisha kama tokeo.

[10]Mwanzo 3:6

Wazo kuwa hatuwezi ishi kando kutoka kwa Mungu linaweza kosa kuonekana ajabu kwa watu wengi, lakini katika sura ifuatayo tutajifunza kuwa mawazo ya aina hii ni ya kujiua.

## 2. Chemchemi ya Uzima

Imekuwa siku ndefu kazini. Tulikuwa katika sehemu ya mwisho ya kuandaa bajeti yetu – kwa kweli bajeti tisini ambazo lazima zingeunganishwa kuwa bajeti moja. Ilikuwa mchakato laini, kuchora mapato yaliyokuwepo miongoni mwa mameneja wote wenye kutaka ukuu, kutarajia, na kudai kipande kikubwa cha pai ili kuafikia malengo yao. Akili yangu ilikuwa ikijaribu sana kusukuma takwimu hizi kutoka kichwani mwangu ghafla simu ilikiriza. "Hello… nini baba, mwanangu." Baba alisikika kana kwamba ana himaya ya Nchi ikijengwa mabegani mwake. "kuna nini Baba?" "Mama amehusika katika ajali mahututi." Maneno hayo yalinigonga kama nyundo. Mara moja nilianza kutetemeka na moyo wangu ukaongeza mpigo maradufu. Misuli yangu ikawa na kiwamba, adrenaline ikaujaza moyo na mwili wangu. "Ajali?" Nilikuwa karibu kunogona ili kushikilia imetosha. "Ni mahututi vipi?" "hakika ni mahututi mwanangu."

Wakati huo nilitamani ningeweza kuruka kupitia kwa simu kumfikia Babangu lakini alikuwa umbali wa saa 12 kwa barabara na ningengoja hadi asubuhi ili kupata ndege. Nilipokata simu, mawazo yangu yalikuwa yakizunguka – mshtuko, hofu na ganzi vyote vilinigonga kwa wakati mmoja. Mara hiyo nikakumbuka Yesu na mara tu ni kazama magotini mwangu nakulia "Oh Yesu – Tafadhali usimwache afe." Nilifungua Bibilia yangu na kuomba tu na kuomba tena hadi hali ya utulivu ikanijia na nikahisi karibu na amani. Kisha mawazo yangu yalishangaa juu ya mambo ya kilimwengu maishani hadi yangenigonga tena; hofu, unyonge na mshtuko. Mara kwa mara nilipiga magoti na kuomba tu na kumtazama.

Mama alikuwa katika safari yake kwenda kufunza somo la muziki. Alikuwa kwenye barabara kuu ya mistari miwili ambayo ina mwachano wa mita kumi unaotenganisha barabara hizo mbili. Alikuwa akijaribu kulipita gari lingine na ndiposa akajipata juu ya muungano na hayo tu ndio ambayo alikuwa akiyakumbuka. Gari lililokuwa likitoka upande mwingine lilikuwa limepoteza mwelekeo na likavuka mwanya wa mita kumi uliokuwa kati ya barabara hizo mbili na kumgonga mamangu ana kwa ana. Nguvu za mgongano zilisukuma injini ya gari la mama kupitia kwa ukuta wa moto na kwa wakati uo huo usukani ukikwaruza uso wake. Kwa sababu isiyojulikana, kwa wakati huo kiti kilivunjika, na ninashukuru kuwa kilivunjika kama sivyo angekufa papo hapo. Walipompeleka hospitalini, alikuwa amevunjika mikono, miguu na upande wa kushoto wa uso ulikuwa umeharibika.

Mama alipokuwa amebebwa hospitalini kulikuwa na daktari ambaye alikuwa amemaliza zamu yake. Alipomuona mama alirudi kazini mara moja. Alipigana kwa saa nane kuyaokoa maisha ya mama, na hatimaye baada ya nukta nyingi za wasiwasi alitulia. Hakika siwezi pata maneno hasa ya kumshukuru daktari huyo; hata hakuna yaani inileteayo machozi. Mtu huyu alifanya kazi kwa saa 16 mfululizo na kisha akawa na wazo la kumpigia babangu 3 asubuhi ili kumjuza kuwa mama alikuwa katika hali mbaya lakini sasa yuko imara. Bado ninashukurani nyingi kwake, mfano unaong'awa ujuzi, ushupavu na ukarimu wa taaluma ya matibabu.

Siku chache baada ye mimi na mke wangu tulikuwa kwenye wadi ya makini ya juuu pamoja na Mama. Nilifurahia sana kumuona akiwa hai. Madakitari walishangazwa na jinsi alivyopata afueni haraka. Tuliambiwa kwamba hatacheza kinanda tena na pengine hata hatatembea tena. Lilikuwa ni pigo kubwa, lakini bado alikuwa nasi, na nilikuwa na shukurani. Lorelle alikuwa akitazama rekodi za kila siku za mama na akanipa ishara nisongee karibu. Ilionyesha wazi sehemu ambayo walidhani wangempoteza mama, na kisha ghafla bin vuu hali yake hatari iliondoka na akaanza kua. Hakukuwa na rekodi ya jinsi hili lilitendeka, lakini nilijua kwamba Baba yangu, mwanzilishi wa maisha, alikuwa amemtuma Mwanawe ili kumhifadhi. Ninashukurani sana kwa nguvu za kutoa uzima za Yesu. Leo hii, Mama anatembea na wakati mwingine anapocheza kinanda, nahisi wingi wa shukurani kwa Yesu kwa kumwokoa mama kutoka kwenye kifo cha ghafla.

Inapofikia kwa kufahamu chanzo cha uzima, Bibilia hutuacha bila shaka. Tunasoma yafuatayo kuhusu Yesu katika Wakolosai:

> **Kwa Yeye vitu vyote vilivyoko mbinguni na juu ya nchi viliumbwa,** vile vitu vinavyoonekana na vile visivyoonekana, kama ni viti vya enzi au falme, au wenye mamlaka au watawala, vitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake. (17) Yeye alikuwapo kabla ya vitu vyote **na katika Yeye vitu vyote vinashikamana pamoja**. Wakolosai 1:16, 17

Kila kitu tunachoweza kuona au kusikia, na hata vitu tusivyoweza kuona, viliumba na sasa vinadumishwa na Yesu Kristo.[11] Angazia kwa makini maneno ya kumalizia ya sentensi ya mwisho. Na *katika Yeye* vitu vyote vinashikamana pamoja. Kifungu kinatwambia wazi kuwa nguvu za uzima za Mwana wa Mungu zinashikamanisha ulimwengu wote pamoja. Paulo anaweka wazo hili kwa njia nyingine katika kitabu cha Matendo:

> "Mungu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo ndani yake, Yeye ndiye Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu. (25) Wala hatumikiwi na mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji chochote, **kwa sababu Yeye mwenyewe ndiye awapaye watu wote uhai na pumzi na vitu vyote.** (26) Kutoka kwa mtu mmoja, yeye aliumba mataifa yote ya wanadamu ili waikalie dunia yote, **naye akaweka nyakati za kuishi.** (27) Mungu alifanya hivyo ili wanadamu wamtafute na huenda wakamfikia ingawa kwa kupapasa – papasa ijapokuwa kwa kweli **hakai mbali na kila mmoja wetu.** (28) **'Kwa kuwa katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu'.** Kama baadhi ya mashairi yenu yalivyosema, 'Sisi ni watotowake' Matendo 17:24-28

Hapa tunaona Mungu ambaye anahusishwa kwa karibu sana na Maisha yetu. Paulo anaanza taswira kubwa na kisha anaishusha chini katika kiwango cha binafsi na moyoni:

---

[11]"Kwani vitu vyote vyatoka kwako, na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea." 1 Nyakati 29:14

1. Ameamua nyakati na sehemu za kila taifa.
2. Hakai mbali na *kila* mmoja wetu.
3. …na hatimaye Paulo anaenda kwenye moyo wa jambo hilo na anasema *katika Yeye* tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu.

Kwa hivyo tunaishi *katika Yeye* na kisha mantiki rahisi hutwambia kuwa hatuwezi ishi bila Yeye. Kama Mwakilishi wa Mungu Mtakatifu, Yesu, Mwana wa Mungu, alisema "…kwa maana pasipo mimi hamwezi kufanya neno lo lote."[12] Tafadhali elewa kuwa hili linamaanisha kuwa hatuwezi fanya lo lote kimwili, kiakili au kiroho bila Yeye. Tunamtegemea Mungu na Mwanawe kabisa kwa kila kitu, kama mtoto mchanga anavyowategemea wazazi wake.

Wacha nionyeshe hoja hii kwa sababu maana yake imefika mbali. Angazia kiungo cha kustaajabisha cha moyo. Hufanya kazi kama pampu ya kusambaza damu mwilini mwetu, bila kupumzika, kwa miongo. Cha kustajabisha kuhusu moyo ni kuwa papo ya moyo haionekani kusaidiwa na chochote kilicho nje yake. Misuli ya moyo inaweza kuwa mkataba na kupumzika bila kichocheo cha moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa neva. Ina kile kiitwacho mfumo wa asili wa kusawazisha. Kama kitabu cha anatomia kinavyoiweka: "Mfumo wa kutuliza una tishu maalum za misuli ambazo hutoa na kusambaza msukumo wa umeme ambao huchochea fiber za misuli ya moyo kuwa mkataba."[13] Fiber hizi za misuli hakika zina umaarufu kwa sababu zinatoa msukumo wa umeme ambao hautoki kwenye mfumo wa neva. Ni ajabu kabisa kuwa hakuna mahali popote katika kitabu cha anatomia panaangazia swali la jinsi fibre hizi za misuli ya moyo zinatoa msukumo huu wa umeme ili kutuliza moyo. Inaitwa maalum na asili, na je inafanya vipi, na nguvu hizi zinatoka wapi?

Hapa ndipo kunakuwa na njia panda. Bibilia inatwambia kwamba nguvu hizi zinatoka moja kwa moja kwa Mungu, "katika Yeye tunaishi." Matendo 17:28. Lakini Shetani anatwambia kwamba ni asili ndani yetu; ni sehemu tu ya mchakato wa biologia ambao tunamiliki sisi wenyewe, "Hakika hautakufa."

---

[12]Yohona 15:5

[13]Gerard Tortora na Nicholas Anagnostakos, *Principles of Anatomy and Physiology*, (HarperandRow Publishers, NewYork, 1984) Uk 463.

Mwanzo 3:4. Hili ni jambo muhimu sana. Aidha moja au lingine. Kuna wakristo wengi ambao hujaribu kuchukua njia ya mkato kuhusiana na jambo hili, "Kweli, Mungu aliumba kila kitu lakini ni kama upepo, saa ya juu. Aliianzisha na akaiacha iendelee." Kama Mungu kwa kiwango aliumba kiini cha dura na kukiweka ndani yetu. Bibilia haifunzi wazo hili. Tumeunganishwa kwa karibu Kwake na tunamtegemea kabisa nukta sekunde ya kila sekunde ya kila dakika ya kila saa ya kila siku. Mungu kikamilifu, kwa kujua, kwa upendo anatusambazia nguvu za umeme ambazo hufanya moyo wetu uzidi kudunda. Kuna kitu kuhusiana na ukweli huu ambao unaweza tufanya sisi kama wanadamu hakika kuwa na wasiwasi, lakini tutaangazia hilo baadaye. Ukweli ni kwamba tunahitaji kulielewa jambo hili vyema sasa hivi. Aidha tuamini kuwa "Katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima" au tuamini "Hatutakufa hakika" Hakuna kuwa katikati.

Licha ya kuwa hili linachangamoto kwa watu wengi, tumeangazia tu sehemu ya kimwili ya uwepo wa mwanadamu. Lazima sasa tuangazie masuala ya akili na kiroho. Tazama mafungu yafuatayo:

> Kusudi langu ni kuwa watiwe moyo na kuunganishwa katika upendo, ili wapate kujua ulivyo utajiri wa ufahamu kamili, waijue siri ya Mungu, yaani, Kristo mwenyewe, (3) **ambaye ndani Yake kumefichwa hazina yote ya hekima na maarifa**. Wakolosai 2:2,3

> Bwana akanena na Musa, na kumwambia, (2) "Angalia, nimemwita kwa jina lake Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila ya Yuda; (3) **nami nimemjaza roho ya Mungu, katika hekima, na maarifa, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina,** (4) ili abuni kazi za ustadi, kuwa fundi wa dhahabu, na wa fedha, na wa shaba, (5) na kukata vito kwa kutiwa mahali, na kuchora miti, na kufanya kazi ya ustadi iwayo yote." Kutoka 31:1-5

Bibilia inadhihirisha Mungu kama chanzo cha hekima na maarifa. Wakolosai 2:2,3 inatia katika changamoto dhana kuwa sisi kama wanadamu tunaweza kuwa waanzilishi wa hekima na maarifa. Hekima yote na maarifa yote hutoka kwa Mungu kupitia kwa Kristo Mwanawe. Mfano wa hili unaonekana katika

Kutoka 31:1-5. Hapa tunamwona Mungu akimpa mtu hekima na ujuzi wa kazi ya kila aina. Inavutia kwamba tunarejelea watu ambao wanaonyesha uwezo na talanta kama "vipawa." Kwa kweli wana vipawa kutoka kwa Mungu.

Wacha tujipeleke kwenye kati ya tamasha. Hadhira ilifungwa kutazama msichana mdogo mwenye kipawa alivyopeleka vidole vyake juu na chini ya kinanda kikuu kilichokuwa kikivutia kwenye jukwaa. Anafanya kinanda kiimbe sawasawa – mguzo wa mkono wa bwana. Kisha anajenga kilele, na kisha tunagundua kuwa mwisho umefika. Tunawasia aendelee – lakini wimbo unaisha na umati unafoka kwa makofi, ungwana kama wa umaridadi huo na neema vikiunganika kwa hamu na kiwango cha juu. Msichana mdogo anainama na kuvuta hewa nzuri ya kutukuzwa kisha anatoka kwenye jukwaa.

Wacha turudi nyuma kidogo, kwa sababu kuna jambo la kuvutia kuhusu mazingira haya ya kawaida. Kila wakati jambo kama hili linatendeka hadhira itavunjika kwa kuimba "Sifu Mungu wa neema yote" au jambo la namna sawa. Makofi yanapawswa kuelekezwa kwa Mungu aliyepeana maarifa na hekima na uwezo. Moyo wa mcheza kinanda unapaswa kutiririkwa na upendo na shukurani kwa Mungu kwa sababu ya karama ambayo amempa, lakini hili linafanyika kwa nadra sana. Kama kwa kweli tulitenda kwa njia hii, hatuwezi tukapitwa na mafanikio au kukatishwa tamaa na kushindwa kwa sababu uwezo wa kutenda hautokani nasi, na kama hautokani nasi, basi hatuwezi pokea malipo wakati tumefanikiwa au tuhisi kukatishwa tamaa wakati tumeshindwa.

Hapa kuna simama laana ya mti wa kiini cha dura. Fikiria uhuru wa mwendesha piki piki akipewa uhuru katika wingu wazi.[14] Hisia za uhuru unaoshuhudia tunapofanikiwa, kuamini kuwa tumeanzilisha mafanikio hayo inalinganisha na msisimko wa kupanda miguu elfu juu ya dunia kushuhudia mitazamo ya ajabu kutoka juu. Lakini iwapo tutajipata juu sana, ukosefu wa hewa safi unaweza tufanya tupoteze fahamu au tuugue kutofanya kwa engine na kutufanya tuvunjike duniani. Kadri tunavyo panda katika uongo wa nguvu

[14]Nyiririko iliyotiwa nguvu, pia inayojulikana kama 'paramotoring' au PPG, ni aina ya sayansi ya anga ya mwangamkuu ambapo rubani huvaa mtambo wa injini mgongoni mwake (a paramotor) ambao humpa nguvu za kutosha kuweza kuinukaakitukia nyiririko. Inaweza anzishwa kwa hewa tulivu, na nchi tambarare, na rubani huyo pekee – hakuna usaidizi unahitajika. Wikipedia.

za ndani, kadri kasi ya msukumo ilivyojua wakati tunavunjika duniani. Hakuna kuepuka laana ya mti wa kiini cha dura. Mara tunapoonja tunda lake hiyo hamu ya kupanda inavutia, na mwishoe matokeo hayawezi epukika. Hakuna ajali kuwa "Huzuni ndiyo inaongoza katika kusababisha ulemavu kimataifa."[15]

Tunda la mti wa kiini cha dura linaleta hamu ya kupanda juu katika sehemu ambazo sio salama kwetu. Kadri tunavyokula matunda mengi, ndivyo hamu ya kupanda inakuwa nyingi na ndivyo wingi wa hakika ya kuvunjika ilivyo. Ni mapigo mangapi umepokea tayari? Ni mangapi zaidi unaweza pokea? Ni thamana kuwazia kuhusu hilo.

Wacha twende kwa kiwango kifuatacho. Tumeangalia maana ya utegemezi wa kimwili na akili, lakini vipi kuhusu utegemezi wa kiroho na maadili. Hili ni jambo lenye changamoto, hivyo basi kaza mikanda ya kiti chako; inaweza kuwa safari ngumu.

Bibilia inatwambia kuwa "Mungu ni upendo." 1 Yohana 4:8. Hili linatwambia kwamba Mungu ndiye chanzo cha upendo. Pia inarejelea Mungu kama Mungu wa matumaini. Warumi 15:13. Wazo hili limefafanuliwa zaidi katika Wagalatia:

> Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, (23) upole, kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria. Wagalatia 5:22,23

Maana ya kifungu hiki ni ya kuondoa pumzi. Wacha tuichambue kwa dakika. Sifa hizi zote zinatokana na kuwa na Roho wa Mungu. Hili linamaanisha kuwa bila Roho wa Mungu hauwezi kuwa na upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema na mengineo. Nilikuwa nikiwazia kuhusu ukweli wa Bibilia siku nilipokuwa nikitembea katika bustani kando ya ziwa. Ilikuwa imetulia na yenye Amani. Ghafla niligundua mama aliyekuwa akimsukuma msichana wake kwenye mniginio. Wote walikuwa wakicheka pamoja na bila shaka walikuwa wakifurahia uwepo wa kila mmoja wao. Upendo ambao mama huyu alikuwa akishuhudia kwa mwanawe ulikuwa ukiongozwa na Mungu. Wazo la kupenda na kuwa na utu na upole kwa mwanawe haukutoka

[15]http://www.who.int/mental_health/management/depression/en/

moyoni mwa mama huyu, lakini moyoni mwa Mungu, na ulipeanwa kwa mama huyo aliyechagua kuudhihirisha, na ukawa upendo wa mama. Katika hali hii sio upendo wa mama kabisa, ila upendo wa Mungu ukidhihirishwa kupitia kwa mama. Upendo huu ulikuwa sehemu ya mama kwa sababu alipokea Roho wa Mungu na akaudhihirisha. Katika hali halisi, hakuna kitu kama upendo huo wa mama kwa wanawe au upendo kati ya mume na mke. Je, hilo linasikika lenye ukali? Vyema hili ndilo ambalo Bibilia inafundisha.

Nimewasilisha wazo hili mara nyingi wakati ninahubiri au ninapozungumza kwa semina na inafurahisha kuona jinsi hadhira inavyolipokea. Nyuso zingine zinaonekana kana kwamba nimeingilia msingi ule wa jamii ya mwanadamu. Kwa mamilioni yote ya nyimbo za mapenzi ambazo zimewahi imbwa na mabilioni ya ahadi za ndoa zinasema kuwa "Nakupenda na nitakupenda milele," Hakuna hata moja ya anaweza dumishwa ahadi hiyo pasipo na Mungu kumwaga upendo wake katika nafsi zetu zenye kupokea. Wacha tuweke sifa ya upendo katika mioyo yetu. Mbona watu wengi "watatoka" kwenye upendo na kuvunjika hadi chini kabisa? Watu ambao huamini kuwa upendo unaanzishwa nafsini mwetu mara nyingi wanaweza amka asubuhi na "kutohisi" kuhusishwa na wapenzi wao. Huanza kushuku kama uhusiano wao ni mzuri kwao tena na mara nyingi huanza kutafuta mtu mwingine ili kurejesha hisia hiyo. Mkopo wa kiini hiki cha Dura umefikia kikomo na sasa ni wakati wa kulipa.

Na vipi kuhusu mwanaume wa kweli ambaye alimaanishi kiapo chake cha kumpenda mke wake milele na ghafla anajipata kuwa amevutiwa na mwanamke mwingine. Hawezi taka kuhisi hivi lakini "hawezi jisaidia." Upendo unachanganyikiwa na tamaa za mwili, na hakuna shaka kwa uadilifu wake. Kisha anaanza kujiondoa kwa mpenzi wake sababu hisia za hatia kutokana na kutenda namna hii kunamzuia kuamini kwamba bado anaweza pendeka. Alifikiria kuwa anaweza dumisha mtiririko wa moyo wake, lakini sasa mtiririko wake umesitishwa na unakuja ukimvunja hadi chini alipoanzia, na ndoa yake imeisha. inakaa ajabu yoyote ambayo hupata furaha katika ndoa na hivyo ni ndoto kwa watu wengi?

Kwa minajili ya wale wanaohisi kana kwamba ndoa yao haifai tena, kumbuka kwamba upendo hutoka kwa moyo wa Mungu tu na unapatikana bure kwa wale

wanaoagiza kutoka kwake. Iwapo unahisi kwamba umepoteza upendo wako kwa mwenzako, mwagize Mungu akurejeshee. Atakurejeshea, kwa maana ameahidi.

> Nanyi mkiomba lo lote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa katika Mwana. (14) Kama mkiniomba lo lote kwa Jina Langu nitalifanya.'' John 14:13-14

## 3. Karibu na Moyo wa Mungu

Tunakimbia katika njia huru kwa kasi. Mpunguo wa Lorelle ulikuwa umekuwa mfumo endelevu. Hatukuta kuchelewa na hivyo basi, tulijifunga hospitalini. Yote yalikuwa mapya na ya kusisimua; karibuni tutapata kifungua mimba wetu. Tulinyiririka hadi kwenye wadi ya uzazi na muuguzi akatutazama mara moja na kusema, "Mmefurahi sana, mnafaa kwenda matembezi." Sawa, hilo lilitufanya tusiwe na shauku. Dakika arobaini baadaye tulirudi na sasa Lorelle hakuwa anatabasamu tena. Dakika zingine thelathini na tulifika kwenye kati ya uzazi haswa. Ndio, hakuna jina lingine la kuelezea, uchungu wa uzazi, uchungu mkubwa. Tulijaribu kukumbuka mbinu zote kutoka kwa darasa la kabla ya kujifungua lakini ilikuwa vigumu kusalia makini. Mipunguo hiyo iligonga kama gari la moshi la mizigo linalofika kikomo. Punde tuliposhughulikia mmoja mwingine ulikuwa juu yako moja kwa moja. Hatimaye, baada ya saa kumi na moja, tulimpokea kifungua mimba wetu mvulana, Michael.

Kuna picha ya kusisimua kweli, yangu na Lorelle baada tu ya kujifungua. Ni ya ajabu kabisa. Ameketi pale akitabasamu, kana kwamba yote ilikuwa ni kazi ya siku, na  ninacheza kwa upepo mwanana nikionekana karibu kuzimia. Nilipata heshimu nyingine na kubwa kwa wanawake siku hiyo. Lazima ni waambie nyinyi kina dada kuwa kumtazama mke wako akijifungua ni kazi ngumu kweli.

Ukimaliza kucheka, nitamalizia hoja yangu ☺. Hisia za dhiki za kumtazama umpendaye katika uchungu mwingi kama huo ni ajabu. Kwetu sisi wanaume, wakati wote tunakuwa na suluhisho la tatizo, lakini sikuwa na jibu wakati huu na iliuma. Niliomba tu, "Mungu, najua kuna sababu ya uchungu huu wote, lakini sasa hivi siwezi iona." Hakika nilikuwa na furaha ulipoisha.

Nilipomshika mwanangu kwa mara ya kwanza, ilikuwa kipindi cha milele. Niliyatazama macho yake, na alikuwa akiniangalia moja kwa moja, na ilikuwa ajabu. Nilipoendelea kuangalia chini katika kustaajabu, nilishikwa na hisia hii ya ndani ya hofu. Nilijua kuwa mwanangu alikuwa amewekewa mhuri wa hali kama yangu, hali ambayo hutoa changamoto kwa mamlaka, ambayo kiasili inaamua kuasi badala ya kutii. Nilijua kuwa nilikuwa na jukumu la kuongoza wasia huo na kumfunza upendo, utu wema, kutojipenda na utiifu. Baada ya haya yote, nilistaajabu, angeweza kuwa rafiki yangu? Kuna kitu kingeingia kati yetu na kututenganisha? Niliomba pale pale, "Oh Baba mpendwa uliye mbinguni, usiruhusu chochote kije kati ya mwanangu nami. Tuweze kuwa karibu wakati wote, na ninaomba kwamba aje kutambua mimi ni nani na awe rafiki yangu." Uzito wa ombi hilo unasalia ndani yangu. Ninauhisi mara nyingi, na bado naomba ombi hilo nikiamini kuwa Mungu atalifanya kuwa kweli.

Miaka minne baadaye nilikuwa katika siku ya Sabato tulivu nikitembea na kunena na Bwana, mbali na mahangaiko na shughuli za maisha. Nilikuwa nikiwaza kuhusu Baba yangu aliye mbinguni na upendo wake kwangu na jinsi ulivyo wa thamani. Ghafla, mawazo yangu yalirudi nyuma katika kuzaliwa kwa mwanangu na kufufua ile hamu ya kutotaka kutenganishwa naye na kuwa angenifahamu kwa kweli. Mazingira haya yalipita na katika utulivu nilisikia sauti nyororo na tulivu ndani ya mawazo yangu, na ilisema, "Hivyo ndivyo ninavyohisi kukuhusu." Sikujua nilie au nicheke, na niliiona ajabua sana kukubali. "Lakini Bwana, nilisema, "Unajua jinsi nilivyo, Unajua kwamba nimenena na kutenda mambo mengi maovu," na kwa hivyo niliendelea kupigana. Nilikuwa nikishangazwa na nafsi yangu kweli. Mimi ni mtu ambaye amemkubali Kristo kama Mkombozi wa nafsi yake na anaye amini kuwa dhambi zake zimesamehewa, lakini wakati Mungu alikuja karibu nami na kuniambia anavyohisi juu yangu, ilikuwa vigumu kukubali. Hatimaye nililia kwa nguvu "Oh asante, asante kwa kunipenda na asante kwa yale yote

umenitendea. Nakupenda sana." Katika hali halisi nilihisi kana kwamba nilikuwa nimeshikwa mikononi mwake. Singefurahia zaidi, nilitambua kuwa Baba yangu aliye mbinguni ananipenda sana kiasi ya kwamba hataki chochote kije kati yetu. Humuumiza akifikiria kwamba tunaweza tenganishwa, na anafanya kila awezalo ili kuzuia hilo lisitendeke.

Katika hali hii fadhila ya ajabu ya kuwa sehemu ya Ufalme wa Mungu ilidhihirishwa kwangu katika kiwango cha moyo wangu. Hivyo baada ya tukio hili niliongozwa katika mafungu kadhaa ya Bibilia ambayo kwa kweli yalifungua macho yangu na yakanifanya kumtukuza Mungu hata zaidi. Naomba kwamba umuhimu wa fungu hili ukuchome moyoni mwako na usiwahi kuacha. Hapa kuna dirisha wazi kabisa kwa ufalme wa Mungu.

> Mnajua kwamba shomoro watano huuzwa kwa senti mbili? Lakini Mungu hamsahau hata mmoja wao. (7) Naam, hata idadi ya nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa. Kwa hiyo msiogope, ninyi ni wa thamani kuliko mashomoro wengi. Luka 12:6,7

Yesu akielezea kanuni za ufalme wake. Katika fungu hili tuna mbinu ya kile huwafanya watu kuwa muhimu katika ufalme huo. Nini hicho ambacho huwafanya kuhesabika, huwafanya kufaa kitu, huwafanya wenye thamani? Kama masuala haya sio muhimu kwako, basi fungu hili halitakuwa na maana kubwa kwako, lakini bado sijapata mtu yeyote ambaye hapigani na masuala ya kujifaa wenyewe.

Yesu anaelezea thamani ya shomoro katika maelewano ya binadamu. Katika macho ya dunia shomoro hawa wana thamani ndogo. Yesu kisha anatoa tofauti na kusema, "Lakini Mungu hamsahau hata mmoja wao." Tofauti hapo ni kuwa kwa sababu Mungu hukumbuka shomoro, wana thamini sana katika ufalme wa Mungu. Yesu anapanua kanuni hii kwa kulinganisha jinsi Mungu anatufikiria ikilinganishwa na shomoro. "hata idadi ya nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa." Basi ni nini? Unajua yeyote ambaye anataka kujua zaidi kukuhusu hadi anafuatilia hesabu ya nywele zilizoko kichwani mwako? Kisha unakuja mstari muhimu: "Kwa hiyo msiogope, ninyi ni wa thamani kuliko mashomoro wengi." Unaona jinsi thamani na umuhimu unapatikana katika ufalme wa Mungu? Unakuja tu kwa kutambua kuwa Mungu kwa upendo anawaza kutuhusu kila wakati. Ni dhahiri kuwa tuko katika mawazo yake.

Anatupa uzima, anafanya mioyo yetu kupiga, na anamwaga upendo wake kikamilifu katika maisha yetu ili kwamba tuweze kufurahia maisha; na hutoa kwetu karama nyingi, vipaji na uwezo kwa uridhisho wetu, starehe na huduma kwa wengine. Hapa kuna siri ya ufalme wa Mungu, siri ya maana. Ni ufungua ambao hufungua ufalme wa utumwa wa kukosa maana na huzuni. Unao ujasiri wa kuamini?

Tukiwa bado mahali hapa, unajua kiwango ambacho Mungu anawaza kukuhusu? Sikiza hili…

> Ee Bwana, Mungu wangu, umefanya kwa wingi miujiza yako na mawazo yako kwetu; Hakuna awezaye kufananishwa nawe; Kama ningependa kuyatangaza na kuyahubiri, Ni mengi sana hayahesabiki. Zaburi 40:5

Kama thamani yako inaamuliwa na mawazo ya upendo ambao Mungu anao kwetu, basi fungu hili linatwambia kuwa hatuna thamani, kwa sababu linasema mipango na mawazo yake kwetu ni kuu kuliko yanavyoweza kutangazwa au kuhesabiwa. Inahisika vipi kukosa thamani? Lakini inaweza kuwa nzuri kama Imani yetu katika ukweli kuwa Mungu anatupenda bila kipimo, bila kuzingatia jinsi tulivyowema au waovu. Hii ni habari njema na ninashukuru kwayo. Hivyo unapojaribiwa kushuku thamani yako, angalia tu shomoro na uamini!

## 4. Ufalme wa Familia

Ni siku yenye joto baridi. Hali ya sherehe imejaza chumba. Harufu nzuri ya chakula chenye ladha inaahidi chipuko lenye ladha ya ponyesho la kweli. Kicheko kinatawala kadri hadithi za wakati uliopita zinanenwa. Zawadi zinabadilishanwa katika hewa ya furaha za kushangaza ikichanganyikana na upendo. Wajukuu wanararua tiba ya nyanya naye babu anatwambia jinsi tumekua warefu. Mara nyingi hii ndio hali tuliyokumbana nayo tulipowatembelea wazazi wetu wakuu. Ulikuwa wakati wa familia, wakati wa kuthibitisha pahali pako, wakati wa kuunganika na uwapendao, kugawanya zawadi; wakati wa thamani na muhimu wa kuwa pamoja.

Hakuna kitu muhimu zaidi kuliko hisia ya familia ya karibu kutulinda kutoka kwa taya za huzuni na kukosa maana ambazo zinapanuka kila siku. Familia inaweza kuwa pahali ambapo unakubalika jinsi ulivyo, mahali ambapo unaweza kuwa jinsi ulivyo, mahali ambapo unaweza samehewa makosa na kufurahia kushiriki tu katika maisha pamoja.

Yesu anatufungulia taswira muhimu ya ufalme wa Mungu alipotufunza jinsi ya kuomba. Yesu alisema, "Hivi, basi, ndivyo mnapaswa kuomba: ' Baba yetu aliye mbinguni…'" Yesu hakusema tuombe "Mungu mpendwa," au "Itukuzwe enzi," au "Mfalme mpendwa," kama sehemu yetu ya kwanza ya kurejelea, lakini badala, "Baba Yetu."

### UFALME WA MUNGU NI FAMILIA

Hili linaonekana kawaida kwa baadhi ya watu, lakini maana ya ufalme wa familia inafikiwa kwa mbali. Tutaangalia maana hizi katika sura ijayo.

Mara ya kwanza ambayo Mungu anazungumza na jamii ya mwanadamu ni katika Mathayo 3:17. Tangu mwanzo wa wakati hadi ubatizo wa Yesu, Mungu aliwasiliana na wanadamu kupitia kwa Mwanawe. Katika utimilifu wa urithi wa uungu wake, Yesu alikuwa Yehova aliyefungua Bahari ya Shamu, alikuwa Yehova aliyepiga kama radi kutoka Mlima Sinai na alikuwa Yehova aliyeongoza Yoshua katika inchi ya Ahadi. 1 Wakorintho 10:1-4. Wakati wa ubatizo wa Kristo, Mwana wa Mungu alifanyika Emmanueli – Mungu pamoja nasi. Hivyo sasa Baba ananena mara ya kwanza na maneno yake yana umuhimu wa kina (kama jinsi zilivyo), kwa kuwa pale pale Mungu huweka msingi halisi wa ufalme wake. “Huyi ndiye mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa naye.” Kuna njia nyingi ambazo Mungu angemtambulisha Mwanawe, kama vile, “Huyu ndiye muumbaji wa mbingu na nchi; msikilizeni,” au “Huyu ni mfalme, mtiini,” lakini Mungu alimtangaza Mwanawe kwa mtindo wa familia badala ya mtindo wa mfalme au mtawala. Tukichambua taarifa hii, tunagundua yafuatayo:

1. Huyu ni mwanangu
   = **Utambulisho**

2. Mpendwa wangu; Nimependezwa Naye.
   = **Thamani**

Katika ufalme wa Mungu, umuhimu na thamani zinaamuliwa na uhusiano wako na yeye. Hili ni tofauti kabisa na ufalme wa Shetani ambapo umuhimu na thamani unaamuliwa na mafanikio ya utendaji wetu na tulichoafikia, kama tunavyojihukumu na wengine wanaotuzunguka wanavyotuhukumu. Katika ufalme wa Mungu, Yeye ni Baba yetu nasi ni wana wake. Huo ni utambulisho wetu. Tunajulikana kwa yule ambaye sisi ni wake badala ya yale tunayotenda. Ukweli kuwa Mungu anatupenda, anaendelea kutumwagia mibaraka yake anatufikiria kila wakati, na anataka kuwa karibu nasi, unatupa hisia ya ajabu ya thamani. “Kwa hiyo msiogope, ninyi ni wa thamani kuliko shomoro wengi.”

Katika ufalme wa Mungu utambulisho wetu na thamani ni za kudumu kama Mungu mwenyewe – wa milele na habadiliki. Bila kuzingatia mafanikio au kushindwa, uhusiano unasalia daima na thamani yetu ni salama. Katika ufalme

wa Shetani thamani yetu ni kama usalama wa soko la hisa baada ya Septemba 11, 2001 – tete zaidi, ukosefu wa usalama kabisa na imefungwa katika mgongano. Tunaweza kuwa na uhakika kuwa tutafanikiwa wakati wote? Tunaweza kuwa salama kuwa watu wanaotuzunguka, wale tunaotazamia kwa kututia moyo na mwegemeo, kila wakati watapigia makofi jitihada zetu? Vigumu! Wale wenye masikio na wasikie, mtu mwenye hekima alijenga nyumba yake kwenye mwamba badala ya mchanga usongeao.

Kulinda utambulisho wetu binafsi na kujiokoa kutokana na kuingia katika maisha ya kukata tamaa, kufa moyo, kukosa maana na kifo, Mungu ameweka katika moyo wa ufalme wake sheria ambayo italinda uhusiano. Inashughulikia aina mbili za uhusiano: uhusiano baina yetu na Baba yetu wa mbinguni, na uhusiano baina ya kila mmoja wetu kama ndugu na dada katika ufalme wa Mungu. Hii ndio maana Yesu anasema:

> Yesu akamjibu, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote.' (38) Hii ndio amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. (39) Nayo ya pili ni kama hiyo, nayo ni hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' (40) Amri hizi mbili ndizo msingi wa Torati na manabii." Mathayo 22:37-40

Amri hizi mbili zimeundwa ili kulinda utambulisho wetu na thamani kama watoto wa Mungu. Amri hizi mbili kuu zinatoa, bila shaka, ufupisho wa Amri Kumi. Umewahi fikiria juu ya amri kumi kuwa muhimu katika kukuzuia kupoteza thamani yako mwenyewe? Ndani ya ufalme wa Mungu Amri kumi zinafahamika katika Muktadha wa uhusiano. kama utavunja uhusiano huo, unaharibu utambulisho wako, na unapoharibu utambulisho wako, kifo kinatamani kukukumbatia. Hakuna chochote cha kiholela katika taarifa ya Mungu kwamba mshahara wa dhambi ni mauti. Dhambi (ambayo Bibilia inafafanua kama uasi wa sheria katika 1 Yohana 3:4) huharibu utambulisho wetu na thamani. Wakati utambulisho na thamani vimetoweka, nafsi hutamani kifo. Hii ndio sababu hasa mbona huzuni na kujitoa uhai ni tatizo kubwa katika jamii leo. Jibu tu ni – dhambi. Unaweza ona mbona Mungu anachukia dhambi zaidi? Dhambi ni mwizi wa utambulisho wetu na thamani kama wana wa Mungu, na Mungu ameamua kuiangamiza.

Ufupisho wa haraka tu wa yale ambayo tumezungumzia:

1. Ufalme wa Mungu ni familia.
2. Mungu ni Baba yetu nasi ni wana wake.
3. Msingi wa utambulisho wetu na thamani ni uhusiano wetu kwa Mungu.
4. Ufalme wa Mungu ni ufalme wa mahusiano wenye msingi wa uhusiano kati yetu na Mungu na kati yetu na kila mmoja.
5. Uhusiano huu unalindwa na Amri Kumi.
6. Kuasi sheria huharibu utambulisho wetu na thamani.

## 5. Mgogoro wa Famila

Ningeweza kueleza kwa mtazamo usoni mwake kuwa alikuwa ameugua aina fulani ya kiwewe. Mfuko chini ya macho yake ulisaliti jaribio lake la kuonekana timamu. Nilimuuliza “kila kitu kiko sawa?”

“Mimi na mke wangu tumetengana,” alisema kwa uchungu. “Sikuona likija tu,” alisema akizama katika majuto. Tulizungumza kuhusu changamoto alizokuwa nazo na kisha akapayuka “Siwezi stahimili kuto waona watoto – inaniua tu,” ningeona kuwa alikuwa anang’ang’ana kujituliza, na nilihisi uchungu wake kwa kweli. Kwa bidii nilitamani kuwa ningeweza kumsaidia. Maoni yake ya mwisho yalikuwa “Sijui ni njia ipi iliyopo tena au ninakoelekea.”

Wale tu ambao wamekuwa katika eneo lililokunjama la utengano na talaka wataelewa hisia nyuma ya maneno hayo. Mshtuko, hasira na huzuni inayohisiwa na upande ambao hauko radhi mara nyingi umelinganishwa na hisia za kufiwa na mpenzi.[16] Uharibifu wa ukweli wa talaka humaanisha mengi zaidi ya kugawanya kwa mali tu, humaanisha kufanya upya utambulishao wako.[17]

---

[16]Nelly Zola and Renata Singer, *True Stories from the Land of Divorce*, (Pan Macmillian, Sydney, 1995) uk. 2.
[17]Ibid.

Waathiriwa wakuu, bila shaka, ni watoto. Kiwango cha hisia za uharibifu zinazopita moyoni mwa mtoto, sio tu wakati wa tukio lakini katika maisha yao yote, hakiwezi hesabika.

Jim Conway alitafiti mamia ya watu wazima ambao walikuwa watoto wa talaka, viwango vya hisia walizohisi vilielezewa kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Dhalili | 72% |
| Walihisi Dhaifu | 65% |
| Waliohisi Upweke | 61% |
| Waliohofu | 52% |
| Wenye Hasira | 50% |
| waliohisi Kutelekezwa | 48% |
| waliohisi Kukataliwa Kibinafsi | 40% |
| Waliohisi Kukosa Maana | 30% |

Kwa kuwa wahusika katika talaka kama watoto kuliwaacha watu hawa na mambo yafuatayo:

| | |
|---|---|
| Kutafuta kibali mara kwa mara | 58% |
| Kuzuia baadhi ya mambo yao ya siku za nyuma | 54% |
| Wanajihukumu vikali | 53% |
| Wanajichukulia makini sana | 47% |
| Wanaguswa sana na hali ambazo hawawezi kabiliana nazo | 42% |
| Bado wanamatatizo katika uhusiano | 40%[18] |

Ni ajabu yoyote kuwa Mungu anasema,"Nachukia talaka!"Malaki 2:16. Bila kuzingatia jinsi inatendeka, au nani anaondoka, kupoteza uhusiano wa familia kunaumiza kwa pande zote. Hakuna washindi wakati uhusiano wa familia unavunjika. Lakini hiki ndicho hasa kilitendeka mbinguni. Familia ya Mungu ilivunjwa vipande vipande na mgogoro wakati Mwanawe mpendwa wa kwanza kuumba aligeuka dhidi yake.

[18]Conway, uk. 31.

Bibilia inasema katika ufunuo 12:7, "Kulikuwa na vita mbinguni." Tunaposoma fungu hili tunaweza jaribiwa kufikiria kuwa hivi ni vita baina ya wafalme wawili na falme zao, lakini vita hivi vilikuwa mgawanyiko wa familia ya Mungu. Unaweza fikiria mara ya kwanza Mungu alipomuumba Lucifer na kwa utefu akamtazama mwanawe? Mungu alishirikisha moyo wake na nafsi yake na malaika huyu. Hakuwa amemwonyesha chochote ila tu upendo na kumpa fadhila ya kuhudumu sehemu ya juu ya serikali yake ya familia. Lakini sasa huyu mwanawe alikuwa akitema maneno ya hasira na uasi. Akienenda katika kivuli cha udanganyifu na uongo, alitia sumu katika mawazo ya watoto wengine wengi wa Mungu. Unaweza fikiria huzuni? Lucifer, aliyeumbwa mkamilifu, sasa alikuwa amejawa chuki na mauaji. Alikuwa amepindwa katika kumwangamiza Mwana wa milele wa Mungu, kwa sababu Yesu alidhihirisha kuwa Shetani alikuwa muuaji tangu mwanzo katika Yohana 8:44. Ukweli wa hisia hii ulionyeshwa msalabani Kalvari, ambapo Shetani alitumaini kumuondoa Yesu.

Nani anaweza fahamu hasara ambayo Mungu amehisi kumpoteza Mwanawe Lucifer. Tuna mwangui kutoka moyoni mwa Mungu katika kisa cha daudi na Absalomu.

> Naye mfalme akataabika sana, akapanda juu, akaingia kile chumba kilichokuwa juu ya lango, akalia; na katika kwenda kwake alisema hivi, "mwanangu Absalomu! Ee mwanangu! Mwanangu Absalomu! Laiti ningalikufa badala yako, Absalomu, mwanangu, mwanangu!"
> 2 Samweli 18:33

Absalomu, Mwana mzuri na mtanashati wa Daudi, alitaka kumuua babake na kuchukua ufalme wake, lakini jeshi la babake likalemea nguvu zake na Absalomu akauawa vitani. Badala ya furaha kwa ushindi huo, Daudi alilia kwa kumpoteza mwanawe muasi. Hakuna washindi wakati familia zinatawanyika.

Ni muhimu kukumbuka katika ufalme wa Mungu utambulisho wa mtu na thamani zimefungwa katika uhusiano wao na Mungu Muumbaji, Baba yetu wa mbinguni. Lucifer alipojiondoa katika uhusiano huo, alijinyonga kiakili na kihisia na kufungua mlango wa mafuriko yasiotarajiwa ya hisia za giza. Kabla ya uasi wa Lucifer, kama ungemuuliza – "Wewe ni nani?" angesema kwa utulivu shwari na kujiamini, "Mimi ni mwana wa Mungu, na ananipenda."

Mara tu Lucifer alipomkataa Babake, kama ungemuuliza swali hilo hilo. “Wewe ni nani Lucifer?” angesema nini? Hakuwa na utambulisho tena, alikuwa ameuharibu. Utambulisho wowote ambao angejaribu kujitengenezea tangia hapo, haunge, haungejaza ombwe na hisia za hasara aliyoishuhudia kutokana na kuvunja uhusiano wake wa karibu na Baba yake wa mbinguni.

Mara nyingi alitamani angeweza kurejesha ambacho alikuwa amepoteza, lakini kiburi chake hakingemruhusu. Zaidi ya hilo, ndani yake hangeamini kuwa angeweza kusamehewa baada ya shaba yake ya ukosefu wa shukurani na uasi wa wazi. Lucifer, sasa Shetani, ambalo linamaanisha “mpinzani”, anasimama peke yake. Hakuna yeyote wa kumshikilia, hakuna umbo la mzazi wa kugeukia, na hakuna pahali pakuita nyumbani. Sasa shetani ameisha kwa hisia za kukosa maana: ukosefu wa usalama, hofu, utupu, wivu, kujihesabia haki, kiburi, hasira, na roho ya kutawala.

Shetani hakujua njia iliyokuwepo tena. lazima angetengeneza utambulisho wake upya na kwa kiasi fulani alainishe utupu huo, ukosefu wa maana huo, hukwo kutokuwa chochote alikohisi ndani yake. Kama mtoto yeyote anaye hisi kukosa maana, Shetani anabeba alama zote za ukosefu wa usalama, hofu, kuchanganyikiwa na hitaji la kukata tamaa kwa kibali kutoka kwa yeyote anayeweza kupata. Anaomba makini, na kuridhisha utupu, hali yake potoshu inatamani kuabudiwa, kupigiwa magoti na kupendwa – chochote cha kuondoa maumivu, upweke na kukosa maana – chochote. Hali hii ya kusikitisha kwa kushangaza inaonyeshwa katika wimbo sinema iitwayo “city of Angels”:

**Fungu 1**

Tumia wakati wako wote ukisubiri nafasi hiyo ya pili
kwa pumziko ambalo litaifanya sawa
Daima kuna sababu ya kuhisi hufai kabisa
Na ni vigumu mwisho wa siku
Nahitaji kuondoka ora ondoleo nzuri
kumbukumbu za tiririka kutoka kwa vena zangu
Wacha niwe tupu. Oh na uzito pengine
Nitapata amani kiasi usiku

**Fungu 2**

umechoka na msatari laini, na kila mahali unapogeuka

Kuna tai na wezi nyuma yako
Mawimbi yanazidi kufurukuta, endelea kuunda uongo
Ndipo upate yale yote unayokosa
Haileti tofauti, kukwepa fursa moja ya mwisho
Ni rahisi kuamini katika uwendawazimu huu mtamu
Oh Huzuni hii tukufu ambayo uniweka magotini.

Kwa vile Shetani alikuwa amekataa uhusiano kama msingi wa thamani, hangeweza kuanzisha ufalme wenye msingi wa uhusiano. Kulikuwa na uchaguzi mmoja uliosalia kwake. Julikana na yale ambayo unatenda badala ya yule wewe ni wake. Ufalme huu hauwezi kuwepo kama kila mmoja anakiri kuwa uzima wote, hekima na upendo hutoka kwa Mungu. Hivyo Shetani alizua kanuni ya "nguvu za ndani," ndiposa kumshusha Mungu kuwa nguvu ambayo haiwezi kuwa na uhusiano binafsi. Nguvu ambayo unaweza tumia na kukiuka utakavyo. Ufalme wa Shetani ni ufalme wa nguvu na matendo na kutafuta radhi. Mada yake kuu ni kutowajibikia mtu yeyote, tunza wale wana umuhimu kwako.

Ufalme wake umepotea, bila shaka, kwa sababu nguvu za uzima zinazoudumisha ni za aliyehai na siku moja hatia ya kumkataa itavunja uhai wa wale ambao kwa usumbufu wanakataa kukiri utambulisho wao kama wana wa Mungu. Umepotea kwa sababu hakuna chochote kinachoweza ondoa maumivu na hasara ambayo huja kutoka kwa kukataa utambulisho huo. Hapa tunajifunza ukweli wa methali, "Hakuna pumziko kwa waovu."

Tukigeuka katika Bustani ya Edeni katika muktadha huu, tunaona kuwa kwa nje Shetani anaonekana mwenye hila na mjanja anapotafuta kuzuia kufukuzwa kwake kutoka mbinguni. Lakini moyoni ndani kumejaa utupu na ukosefu wa usalama zinazojitahidi kutengeneza utambulisho mpya na kuepuka tofauti inayozidi kupanua ukosefu wa tumaini.

## 6. Jahanamu Duniani

Inakuwa moja ya hali za kuzunja moyo zaidi katika maisha. Inaweza kuwa imechukua miaka, lakini kwa wakati umetengeneza urafiki imara na mtu. Mtu ambaye umekuja kufurahia kupitisha wakati naye. Gafla unagundua kuwa rafiki yako kidogo tabia zake ni za ajabu. Unajaribu kupuuza na kujiambia kuwa unafikiria mambo na kuwa hakuna jambo la kweli. Lakini ushahidi unazidi kujitokeza kadri muda unavyopita, na hatimaye unahisi umelazimika kumuuliza rafiki yako kinachoendelea. Baada ya kikao kile ambacho kinakaa kana kwamba ni mwaka ili kuondoa ukuta wa jiwe, unagundua kwamba mtu mwingine amekuwa akimwathiri rafiki yako dhidi yako, jambo ambalo limewapelekea kueleza matendo yako kwa njia ambayo inakuacha kama umeudhika.

Hakika sababu itahanikiza na unaweza kwa haraka suluhisha kutoelewana huku, lakini sivyo! Unapojaribu kutoa maelezo yenye mantiki unahukumiwa bila aibu kwa kujaribu kujitetea ili kuficha ukweli. Katika kiwango hiki moja wapo ya hisia inaweza kupiku: kuumizwa, maumivu, hasira au hata uharibifu ambao rafiki yako anaweza amini kwa urahisi kuwa mtu mwingine bila wewe kuwahi sema neno kwake, yeye mwenyewe akutetete! Kupasuka kwa ukimya wako (ambao unatumika) unatoa ishara kwa "rafiki" yako kuwa walikuwa sawa na kuwa yote yaliyosemwa kukuhusu yalikuwa kweli. Sema kuhusu kuongeza matusi kwa jeraha!

Pengine unaposoma aya hizo mbili za mwisho, kumbukumbu chungu imejitokeza unapothibitisha ukweli wa mazingira haya ambayo yamejirudia

tena na tena tangia mwanzo wa wakati hapa duniani. Hata ninapoandika na kumbuka tukio kama hilo kwangu, nakoma na kuuliza tena, "Mbona?"

Ninauhakika wengi wetu wana vidonda kutokana na aina sawa ya kukataliwa, na ninakisia wanaweza kwa njia ndogo tusaidia kuelewa jinsi Mungu alihisi wakati Adamu na Hawa walikula tunda kutoka kwa mti wa ujuzi. Ni moja wapo ya ajabu kuu ya maisha kuwa maneno ya mgeni yanaweza tenganisha marafiki bora.

Mara nyingi nimefikiri Mungu akimtazama kwa karibu binti yake Hawa alipojipata katikati ya bustani, ghafla akashiriki katika dayolojia na "mgeni." Baada ya wakati huo wote ambao Mungu alikuwa amewekeza kwa Hawa, akimuonyesha ishara zisizohesabika za upendo wake, angejishikilia kwa usalama na upendo wa Baba yake wa Mbinguni au kukumbatia maneno ya Shetani kupitia kwa nyoka? Mbona Mungu hakuingilia na kumtuma malaika kuzuia kugawanyika kwa uhusiano wao? Nakisia kuwa kuna maswali mengi ya "mbona" ya kujibu katika hatua hii. Hatuna wakati wala nafasi ya kuyaangazia hayo yote, na kwa kweli baadhi yao hayawezi angaziwa kikamilifu hadi tumuone uso kwa uso, jibu kuu ni Upendo.

Upendo hutupa fadhila ya kuchagua hata wakati ambao uchaguzi unaweza kumuumiza kwa ukali mpaji wa uchaguzi. Kama mungu angekuwa na mazoea ya kuingilia kila wakati wana wake walikuwa nusra kuchukua mwelekeo usio sawa, basi ukweli hawangekuwa na uchaguzi kabisa. Kuna wakati wa maagizo na marekebisho, lakini bado unakuja wakati ambao kimya cha mpaji wa uchaguzi kinadhabitisha maelezo yote ya "Nakupenda" ametamka, kwa sababu upendo bila uchaguzi sio upendo kabisa. Huu ni ukweli ambao wazazi wengi wanashindana nao wanaposhughulikia watoto wao. Kama baada ya maagizo na maelekezo watoto wetu bado wanachagua kinyume chetu, je, tunawaacha kujikomboa uchungu wa kukataliwa? Au tunabaki kimya na kuomboleza, kuwaruhusu katika uchaguzi wa kutukataa? Ni uchaguzi mgumu kwa mzazi yeyote.

Mungu, akivikwa katika nguvu za upendo, kwa kimya anamtazama Hawa, binti wake wa thamani, akawa chombo cha kumharibu mwanake mpendwa Adamu. Kwa sasa kiwango cha maumivu katika moyo wa Mungu lazima kiwe ni cha ajabu. Je, maumivu moyoni mwa Mungu ya kumpoteza bintiye

yatamfanya kuingilia ili kumuokoa Adamu? Hapana. Upendo wa kiungu huhuzunisha kwa kina na husubiri katika kimya, kudhibitisha bila swali kuwa ni Mungu wa uhuru na uchaguzi huru. Ataruhusu Adamu kujichagulia mwenyewe. Tunapozungumza kuhusu majaribu, tafadhali tusiruhusu fikira potovu kuwa Mungu anatazama bila kujali uendeleo wa jaribu kutoka kwa usalama wa mbinguni kuona kama Adamu na Hawa wanakile kinahitajika ili kuwa katika kundi la mbinguni. Mungu alikuwa akijaribiwa kama Adamu na Hawa. Kwa maana Mungu anajua kama Adamu na Hawa wataanguka, basi lazima atimize ahadi iliyoamuliwa kabla ya uumbaji wa ulimwengu.[19] kupeana uhai wa Mwanawe – Yesu Kristo. Kristo atawaonyesha jinsi Baba yake alivyo kweli; atachukua hatia yao juu yake yeye mwenyewe na kuiruhusu ivunje uhai wake badala ya wao. Yote haya Mungu aliyajua kikamilifu alipowatazama kimya Hawa na Adamu wakichagua kinyume naye. Ni upendo wa namna gani ulikuwa katika kimya hicho? Onyesho hili la upendo utaondoa milele wazo la uongo kuwa mungu aliongozwa na masilahi ya kibinafsi katika kuwashughulikia wazazi wetu wa asili.

Tunajadili katika sura 1 falsafa ambayo Adamu na Hawa walikuwa wakikumbatia walipokula kutoka kwa mti huo na tuna jadili katika sura tangulizi mchanganyiko wa kutisha wa hisia ambazo zilipelekea Shetani kuleta dhana kuwa tunaweza ishi bila Mungu na kutengeneza utambulisho wetu wenyewe kwa yale tunatimiza. Hata wakati juisi ya tumbo la Adamu na Hawa ilikuwa ikisiaga tunda, wingu la kuuguza la kukosa maana na hatia lilikuwa likifunika mawazo yao, likifungia upendo huo, furaha, na uhusiano wenye furaha kati ya Mungu na mwanadamu. Laana ya mti wa kiini cha dura ilikuwa imeanza kazi yake ya ndani, na katika kipindi kifupi Adamu na Hawa walijawa na hatia na hofu. Wao, pamoja na Shetani na malaika zake, walikuwa na mauaji ya kiakili na kihisia. Walikuwa wamepoteza utambulisho wao na thamani, na hakuna kitu ambacho wangefanya kurejesha. Hawangejirejesha katika fadhili za Mungu. Walikuwa wamevunja uhusiano wao na Mungu tu ndiye angeurejesha. Ukweli huu unajieleza wenyewe hata tunaporejelea maisha yetu wenyewe. Kama mtu anakiuka uhusiano nasi, nguvu za kurejesha uhusiano huu huwa kwa upande ambao haujakiuka; upande ambao umekiuka umesalimisha mamlaka yoyote katika uhusiano.

---

[19]1 Petro 1:20; Ufunuo 13:8

Katika sehemu hii ni muhimu kukumbuka kile tuliangalia katika sura 2. Mungu ndiye chanzo cha uzima, hekima na furaha. Adamu na Hawa wamejiondoa kutoka kwa chanzo hicho kwa kuamini uongo ambao wanamiliki yote haya ndani yao. Nguvu zao za kufikiria haziwezi tumika tena bila ubinafsi au lengo. Mawazo yao yako katika umoja na ya Shetani. Hawana uwezo wa kufunua uongo ambao Shetani anawaambia. Shetani anaanza kuwajaza nadharia za uongo kuhusu tabia ya Mungu. Wakati huo huo Shetani anawaambia Adamu na Hawa kuwa sio wema. Anawaambia kwamba wanastahili kufa na kuwa ni watu wasio na maana. Shetani bado ameinamia jahanamu katika kuharibu maana yetu ya utambulisho, na hufanya hili kwa kutuambia uongo kuhusu Mungu na uongo kutuhusu. Kadiri tunavyo amini uongo kumhusu Mungu na uongo kutuhusu, hatuwezi unganishwa kwa Mungu. Njia pekee ya kurejea katika uhusiano wetu na Mungu ni kujua kwa kweli tabia yake kama inavyodhihirishwa na Mwanawe.

Mgeni ametenganisha marafiki bora. Mungu anakuja kuwatembelea na anaita Adamu na Hawa, lakini sauti ambaye waliitambua kuwa tamu kabisa ulimwenguni, sasa inawafanya wajifiche kwa hofu na kukata tamaa. Mpango wa Shetani umefanikiwa!

Fikiria ukija nyumbani siku moja kutoka kazini, kwa furaha ukitarajia ibada ya furaha ambayo umenjenga na mwanao. Kila jioni mwanao hukimbia akipitia mlango wa mbele akiimba, “Baba, Baba,” na kisha anajirusha mikononi mwako kwa kumbatio tefu. Unaposogea nyumbani unapata kwamba mwanao mpendwa hajaja kukusalimia. Kwa mshangao, unaingia mlango wa mbele na kisha unasikia kilio cha hofu kikiandamana na nyayo ndogo zikikimbia kwa kasi bustanini kujificha. Jambo fulani limevunja uhusiano. Palipo kuwa na upendo, sasa pana hofu. Hakuna baba wa kweli anaye furahia watoto wake wakimkimbia na kuichungulia sauti yake. Inaumiza. Ni maafa kuwa dhambi inaweza tufanya tuwe na hofu ya mtu atupendaye zaidi, mkarimu, mtulivu, na apendaye uhuru katika ulimwengu.

Mungu anakumbwa na taharuki kubwa. Atawakaribiaje Adamu na Hawa sasa na wanaisikiza sauti nyingine? Kila neno ambalo Mungu ananena sasa linafasiriwa kwa nuru ya uovu. Wanajua kuwa wanahatia, lakini sasa hawana usalama na thamani ya kukubali kuwa wamekosa, baada ya kukubali mawazo ya uongo kumhusu Mungu, ambaye ni chanzo cha uzima na hekima.

Wakiongozwa na roho wa hatia na ukosefu wa usalama wamekuwa pekutevu. Wameipoteza nguvu ya kufikiria kiuaminifu.

Nilishangaa kwa upendo wa Mungu ulioonyeshwa katika utulivu wake. Mungu anamwita Adamu, "Uko wapi?" sio kwa sababu hakujua ila kumruhusu Adamu kukabiliana na jambo hilo. *Wapi mawazo yako Adamu? Nini kimetendeka kwa utambulisho wako?* Njia za kimwili zinawakilisha za kiroho, na kujificha kimwili kwa Adamu na Hawa kunaonyesha wazi kujificha ambako kunatendeka katika mawazo yao. Wamejivika udanganyifu ili kuepuka kukabiliana na ukweli ambao unaonekana kuogopesha. Mungu anajaribu kuwasaidia kutambua tatizo ili aweze kuleta suluhisho lenye Baraka kwao.

Adamu anajibu swali kwa kumwambia Mungu kuwa alihofu kwa sababu alikuwa uchi. Ungamo hili linavutia kwa nuru ya Mwanzo 2:25. "Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya." Adamu alikuwa uchi kabla ya kula tunda lakini hakuona haya. Wazo hapa ni kuwa Adamu sasa anaona haya. Neno la Kiebrania (buwsh) pia linamaanisha kuchanganyikiwa, kufadhaika na kusikitishwa. Adamu alikuwa amejaa kuchanganyikiwa, hatia na kukata tamaa. Alikuwa amechanganyikiwa kuhusu kuwa yeye alikuwa nani na alihisi hatia juu ya kile alichokuwa amekitenda. Mungu sasa anatafuta kuingiza kidole chake katika uzito wa maumivu ya Adamu. "*Nani alikwambia* kuwa uko uchi?" Mungu anamnyosha Adamu kwa kidudumtu cha uongo alioambiwa. Kwa namna nyingine "Nani anakufanya unikimbie?" "Nani ameingia kati yangu nawe?"

Adamu ananenewa moja kwa moja, "Ulikula tunda kutoka kwa mti niliokuagiza usile kutoka kwake?" hili ni swali rahisi ambalo lilihitaji ndio au la tu. Lakini sasa kwa kuwa mawazo ya Adamu yalimuona Mungu kama mbinafsi na mwenye kulipiza kisasi na yeye mwenyewe kuwa mpumbazu na asiye na maana anajumulisha mbili na mbili na katika mawazo yake anapata 64. Adamu anaamini kuwa iwapo atasema Ndio, ataadhibiwa kikatili, anaamini ataadhibiwa mara mbili, moja ya kula kutoka kwa mti na moja ya kudanganya. Akiamini hakuna njia ya kuepuka, Adamu anatafuta kujilinda na kujihalalisha.

"Huyu **mwanamke u**liyenipa, **ndiye** aliyenipa matunda ya mti huo, nikala." alimtuhumu. Mwanaume anahatia dhahiri lakini anatupa lawama juu ya Hawa na hatimaye kwa Mungu. Hebu fikiria mshtuko wa Hawa kwa mwanaume huyu ambaye kwa mda mchache uliopita alikuwa ameahidi kukabiliana naye chochote kitakachotokea, lakini kwa tatizo la kwanza ananguka kifudifudi machoni pake! Dhambi haiwezi ikatoa mtu mwenye umbo la kishujaa ambaye anajitoa bila ubinafsi kuwasaidia wengine. Daima husababisha tokeo la kila mtu kuwa binafsi.

Hatutaki tukose mfumo unaoendelea hapa. Itikio la Adamu linaongozwa na hatia na ukosefu wa usalama, yakiunganishwa na kuelewa visivyo tabia ya Mungu, vyote vikiwekwa pamoja na kiwango kikubwa cha kiburi. Sasa kwa vile hajioni kama mwana wa Mungu tena, lazima akubaliane na falsafa, "Kama siwezi jisimamia mimi mwenyewe, hakuna mwingine anaweza nisimamia!" anafikiria hivi kwa sababu anaamini kuwa hana baba tena. Hapa ndipo penye kuvunjika moyo pakubwa kwa dhambi: Ni jinsi gani Mungu anamuonyesha Adamu kuwa ana picha mbaya kumhusu Baba yake na kuwa sio ati hana maana na mpumbavu? Ni jinsi gani Adamu anaweza pewa tathmini ya hali yake wakati amepoteza nguvu za kufikiria kimantiki? Mungu pekee ndiye chanzo cha hekima ya kweli na Adamu amejitenga na chanzo hicho. Na hata kama Adamu atafikiria, kufikiria kwake kutakuwekaje huru kutoka kwa mchanganyiko wa hatia na kiburi ambao kwa ukali unakataa kila kitu kinachofanana na ukweli? Adama hawezi mkabili Mungu akimwambia amekosea, hata kama inafanywa kwa upendo kwa manufaa yake, kwa sababu ukosefu wa usalama wake unatawala mafikira yake.

Ni ombi langu la kweli kwamba utaona Adamu na Hawa waliokuwa wamejitenga kutoka kwa Mungu kipindi kimoja, walikuwa wamepotea bila matumaini kwamba walikuwa karibu kupita kiasi cha kukombolewa. Walikuwa wametawaliwa na roho ya Shetani. Mioyoni mwao mlikuwa na mbegu ambayo mwishowe ingepelekea wana wao kujiunga na malaika waovu katikaurafiki wa kukata tamaa uliyopindwa kwa mauaji ya Mwana wa Mungu katika Yerusalemi. Ingawaje haikudhihirishwa kikamilifu, mioyo yao haikutaka chochote kuhusiana na Mungu au ufalme wake; bila kugundua kwa kweli walimchukia.

Katika kiwango hiki unaweza jaribiwa kusema, "Ngoja kidogo, unachukua hili mbali kiasi. Nagundua kuwa walikuwa na tatizo, lakini kusema walikuwa

wanamchukia Mungu kabisa ni kutia mambo chumvi." Kwa kujibu naweza sema kuwa lazima tuendelee kukumbuka kuwa wema, na upendo na hekima vyote hutoka kwa Mungu. Haitoki mioyoni mwa wanadamu. Iwapo tutasahau hoja hii muhimu, hatuwezi soma kisa hiki kiukweli na pia hatuwezi jielewa kiukweli. Bibilia inaeleza hoja hii kwa uwazi kabisa. Tazama mafungu yafuatayo:

> Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Warumi 8:7
>
> "Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja. (11) Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu. Warumi 3:10,11
>
> Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Yeremia 17:9

Bibilia inatamka kuwa mioyo yetu katika hali yake halisi, inamchukia au ina uadui na Mungu. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii na ni vigumu kwa akili zetu kujiondoa katika hali hii. Nimegundua katika tajriba yangu, na katika tajriba ya watu wengi ambao nimeshiriki nao, kuwa kuna roho iliyokolea yakupinga ukweli huu. Roho hii ya kupinga kuwa hali halisi ya mwanadamu inamchukia Mungu kabisa, ni mwangui wa moja kwa moja wa pingamizi ambayo Adamu alidhihirisha kwa Mungu, alipomlaumu Hawa na Mungu kuliko kuchukua jukumu la kushindwa kwake. Ukosefu wa usalama wa Adamu ni urithi wetu na hatuweza kuwa katika ukweli tena kuliko angeweza. Kama utajipata ukipinga wazo hili, basi jiulize mbona unahisi namna hiyo? Kama una usalama ndani yako basi taarifa hiyo haitakuhusu kabisa. Ukosefu wa usalama na utupu wa Adamu ni urithi wetu. Haya ndiyo yote ambayo tunaweza pata kwake, hakuna lingine zaidi.

Kama unaweza kubaliana na ukweli huu kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, basi uko tayari kwa uponyaji. Katika muktadha wa mpango wa Mungu wa kutukomboa, kuna uhuru mkubwa wa kugundua kuwa hauwezi tende chochote chema. Unaweza wacha kujaribu. Unaweza wacha kujigonga wakati hali yako ya uovu inajitokeza na kumpiga mtu kihisia au kimwili, lakini naenda mbele yangu; tutahifadhi hili kwa sura ifuatayo.

Tukirejea kwa Adamu na Hawa, tunaweza ona kwamba kuvunja kikwazo kati ya mwanadamu na Mungu inaweza kuwa kazi kubwa sana. Ahueni yao, na ahueni ya wana wao, itahitaji mambo kadhaa:

1. Njia ya kuipa jamii ya mwanadamu hekima ya kutambua hali yao ya kukata tamaa, pamoja na mbinu kwao ya kuathiriwa na mwelekeo sawa bila kukiuka uhuru wao wa uchaguzi.

2. Njia ya kuwaonyesha kuwa walikuwa na mtazamo mbaya wa tabia na ufalme wa Mungu na kwa namna fulani kuwaonyesha kuwa ukweli anawapenda.

3. Njia ya kuondoa hisia yao ya hatia na ukosefu wa usalama na kuwarejeshea utambulisho wao wa kweli na thamani kama wana wa Mungu.

4. Njia ya kurudisha hisia yao ya kusudi, sababu yao ya kuwepo au hatima.

5. Hayo yote ya hapo juu yanahitaji muda. Adamu na Hawa walikuwa wamepoteza maisha yao wenyewe, basi walihitaji mfumo wa kuegemezea uzima wao ili kuwapa muda wa kuchagua na kuamua.

6. Tunapofanya haya yote, Mungu lazima adumishe hisia ya haki, hawezi puuza uasi wao na kusema ni sawa. Ingawa Mungu katika huruma zake haruhusu matokeo kamilifu ya uchaguzi wao kuwaangukia, Adamu na Hawa lazima wafahamu matokeo ya uchaguzi wao ili waanze kuthamini kosa la yale walilotenda.

Kuna hoja muhimu tunayohitaji kutengeneza hapa. Mungu kwa mshangao. Baba na Mwanawe walikuwa tayari wameamua watakachofanya iwapo watafika katika kiwango hiki. Mpango tayari ulikuwepo – mpango ambao ulikuwa mpana vya kutosha ili kuweza kukabiliana na hali hii ya kukata tamaa.

## 7. Mstari wa Maisha ya Mbinguni

Katika jitihada za kuelezea umbo la juu la upendo wa kibinadamu unoawezekana, Wagiriki walianzisha hadithi ya Admetus na Alcestis.[20] Mtume Paulo anataja hadithi hii katika kitabu cha Warumi.

> Hakika, ni vigumu mtu ye yote kufa kwa ajili ya mwenye haki, ingawa inawezekana mtu akathubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. Warumi 5:7

Mfalme Admetus alijulikana sana kwa ukarimu na haki yake, na alikuwa anapendwa katika ufalme wake wote. Mungu Apollo alikuwa ametolewa mlimani Olympus na babake Jupiter na akaambiwa lazima aweke kando utakatifu wake na kuwa mwanamume na kuwahudumia watu kama mtumwa. Alipokuja duniani, mfalme Admetus alijipata kuwa mwombaji masikini na akajihurumia. Alijilisha na akamfanya mchungaji wa kondoo wake na akamtunza kama mwanawe. Baada ya miezi 12 Apollo alibadilishwa katika hali yake ya uungu na akamshukuru Admetus kwa kumsaidia na kumwambia "Iwapo utahitaji usaidizi wangu katika siku za usoni niagize."

Baada ya wakati Fulani Apollo alirudi kwa Admetus kumuelezea kuwa Hades, mungu wa ulimwengu wa chini, angekuja hivi karibuni kumdai. Apollo alisema kuwa alifanya mpango na mke wake Persephone, mke wa Hades,

[20]https://en.wikipedia.org/wiki/Admetus

kwamba kama mtu angepatikana wa kufa kwa niaba yake basi hangehitaji kufa.

Admetus aliienda kwa wazazi wake na kuwauliza kama wangependelea kuchukua pahali pake. Walisema, “Tunakupenda mwanetu, wewe ni mtu mzuri na mkarimu, lakini tunapenda maisha yetu zaidi, hatuwezi kufa kwa ajili yako.” Mfalme alizunguka katika ufalme wake wote akitafuta mtu ambaye atajitola kufa kwa niaba yake na hakupata yeyote. Admetus alijiiuzulu kwa hatima yake na wakati huo mke wake, Alcestis, akamlilia Apollo, “Oh mpendwa Apollo, umembariki mume wangu, na ukaongeza umaarufu wake na bahati ilianguka katika ufalme wetu. Admetus ni mtu mzuri, na watu wake wanamhitaji zaidi, kwamba anafaa kuishi! Nitakufa kwa niaba yake, ili aweze kuishi.” Alipojitokeza mbele za Persephone alimhurumia, na akamwambia anaweza ishi tena kama tokea na uaminifu aliokuwa ameonyesha kwa mume wake. Na basi ndivyo hivyo kwamba Admetus na Alcestis waliongezeka katika miaka, na ndivyo pia alivyotenda Apollo aliwatuza kwa uaminifu wao, na hatimaye wakati kifo kilikuja katika uzee wao, walikuwa tayari kwake.

“Hii,” akasema mwanafalsafa wa Kigiriki, “Ni aina kuu ya upendo ambao – kwamba mtu anaweza utoa uhai wake kwa sababu ya marafiki!” Watu wengi huunganisha hadithi hii na maneno ya Yesu aliposema:

> Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Yohana 15:13

Ila huu sio usemi wa urefu wa upendo wa Mungu, lakini badala yake onyesho la mipaka ya upendo wa mwanadamu. Mtume anatofautisha hadithi hii ya mipaka ya upendo wa mwanadamu na anatwambia:

> Hakika, ni vigumu mtu ye yote kufa kwa ajili ya mwenye haki, ingawa inawezekana mtu akathubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. (8) Lakini Mungu anaudhihirisha upendo Wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. (9) Basi, kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki kwa damu Yake, si zaidi sana tutaokolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu kwa Yeye! (10) Kwa kuwa kama tulipokuwa adui wa Mungu tulipatanishwa naye kwa njia ya kifo cha Mwanawe, si

> zaidi sana tukiisha kupatanishwa, tutaokolewa kwa uzima Wake. Warumi 5:7-10

Mungu alidhihirisha kina cha Upendo wake katika kumruhusu Mwanawe kujeruhiwa na uasi wetu na kupondwa na maovu yetu. Alimtoa mwanawe kwa adui zake, ambao walimchukia na kumdharau, kutokana na upendo wake mkuu na huruma kwao. Huu sio ubinadamu ila upendo wa Uungu.[21]

Kabla ya uumbaji wa jamii ya mwanadamu, Mungu na Mwanawe walikuwa katika mazungumzo ya kina ambayo Bibilia inaita ushauri wa amani.[22] Wakati huo, mpango uliwekwa wa kile kingefanyika iwapo jamii ya mwanadamu ingechagua kinyume chake. Sasa ilikuwa wakati wa kutenda. Nani anaweza kadiria kusononeka kwa Mungu? Ataruhusu Mwanawe kuwa kibadala cha Adamu na Hawa na kulipia matokeo ya uchaguzi wao? Atamruhusu Mwanawe kuchukua juu yake ukosefu wao wa thamani na ukosefu wa matumaini na kuubeba hadi kaburini? Atamruhusu Mwanawe kuteseka upotovu wa utambulisho kabisa na mgawanyiko wa Uwana wake ambao ungetoa moyoni mwake maneno, “Mbona umeniacha?”

Ninapo andika maneno haya, mwanangu ameketi kwa Amani mkabala kidogo nami. Ninageuka kuuangalia uso wake mzuri nahisi hali ya furaha na upendo ukitoka moyoni mwangu kwake. Kisha najaribu kufikiria nikijiweka pahali pa Mungu, kumruhusu mwanangu kuchuka adhabu ya nafsi ya kufa kwa kikundi cha watu ambao sasa wananichukia na kila kitu ninachosimamia. Ninaungama kuwa akili yangu inafunga mawazo hayo tu. Siwezi hata ruhusu nafsi yangu kuwaza kuyahusu. Ninajua hata mawazo kuyahusu ni machungu zaidi kwangu kukabiliana nayo jinsi yalivyo yanaweza nifanya nizimie! Mawazo yangu yalirejea kwa Mungu na taharuki yake na ninahisi mtulivu. Ni nahisi undani wa hisia ya shukurani kwake kwa kuruhusu litendeke, nikijua kuwa mimi ni mmoja wa watu wale ambao, walipokuwa adui wa Mungu, alitoa uhai kupitia kwa dhabihu ya badala ya Mwana wa Mungu. Wazo hili daima hunifanya

---

[21]Kwa maelezo zaidi tazama *The Word That Turned the World Upside Down* by Robert Wieland. http://father of love.info/download/view/863

[22]Zekaria 6:13

kukoma na kumwabudu kwa shukurani kwa upendo wake usiokuwa na mipaka na kafara.

Nimestaajabu kuwa Mwana wa Mungu, ambaye baadaye alifanyika Yesu mwanadamu, alikuwa tayari kufanya hili kwa ajili yetu. Bibilia inatwambia kwamba Mungu anajua mwisho tangia mwanzo, na Baba alishiriki maarifa haya na Mwanawe. Wakati dhambi ilipoathiri ulimwengu, Alijua dhahiri utakapoelekea. Kristo angeona kilichokuwa kikimsubiria alipokuja duniani: kukataliwa, kupigwa, kukejeliwa, kuchukiwa, kulaaniwa na kuapishwa, uchi na giza msalabani, kukosa thamani kwa mabilioni ya nafsi ikikusanyika juu yake, na kusanyiko la kosa na huzuni ya maelfu ya vizazi. Aliyaona yote na ila Mwana wa Mungu anasema, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu."[23] Mwana wangu hakuzembea kuitikia kuja, lakini badala yake, alitaka kuja. Moyo wake, kama moyo wa Babake, unatamani kurejesha wana wake katika ukamilifu wa furaha ambao utakuwa hatima yao. Ni Mungu wa namna gani huyu? Ni nani wa kumlinganisha naye na ni maneno yepi yanatosha kumutukuza?

Tunagundua katika sura ya mwisho kwamba Adamu na Hawa walihitaji mfumo wa kuegemezea uzima na uwezo wa kutambua ukweli kutoka kwa kosa; walihitaji usaidizi wa kuona ukweli kumhusu na kugundua, na kuanika, na kukataa uongo ambao Shetani alikuwa akiwaambia. Walihitaji dira ya maadili kuwasaidia kutambua kaskazini ya kweli ya kiroho.

Vitu hivi vyote vingetolewa kupitia kwa karama ya Mwana wa Mungu kwa ulimwengu. Hili lilikuwa limeambiwa kwa Adamu na Hawa katika Mwanzo 3:15. Akimhutubia Shetani moja kwa moja, Mungu alisema yafuatayo:

> Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino. Mwanzo 3:15

Fungu hili limejaa ahadi na matumaini. Mungu alisema ataweka uadui kati ya Shetani na mwanamke. Mungu anapozungumza juu ya mwanamke, Anazungumza kuhusu yote yatakayotoka kwake, kwa njia nyingine familia

---

[23]Zaburi 40:8

yote ya mwanadamu. Neno uadui humaanisha chuki au adui.[24] Mungu angeweka kitu moyoni mwa familia ya mwanadamu ambacho huchukia uovu na kutamani mema na ukweli. Kuna sababu moja tu mbona Mungu angefanya hili, na hiyo ni kwa sababu Mwanawe angeunganisha familia ya mwanadamu kupitia kwa uhai wake na kifo akiwa duniani. Hili ndilo linamaanishwa na uadui uliopo kati ya uzao wa mwanamke na uzao wa Shetani au wana wake. Paulo, katika kitabu cha Warumi, anarejelea chuki hii ya uovu kama neema au nguvu katika kifungu kifuatacho:

> Lakini ile karama iliyotolewa haikuwa kama lile kosa. Kwa maana ikiwa watu wengi walikufa kwa sababu ya kosa la mtu mmoja, zaidi sana neema ya Mungu na ile karama iliyokuja kwa neema ya mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo, imezidi kuwa nyingi kwa ajili ya wengi. Warumi 5:15

Uwezo wa kuchagua yaliyomema huja moja kwa moja kutoka kwa uadui huu ambao Mungu ameweka mioyoni mwetu kupitia karama ya Mwanawe. Karama hiyo hiyo hutoa karama ya uzima inayohitajika zaidi.[25] Paulo pia anarejelea ukweli huu katika sura hiyo ya Warumi:

> Kwa hiyo, kama vile kosa la mtu mmoja lilivyoleta hukumu kwa watu wote, vivyo hivyo pia kwa tendo la mtu mmoja la haki huleta kuhesabiwa haki kule kuletako uzima kwa wote. Warumi 5:18

Huu ni ukweli wa ajabu ambao unaweza leta Amani na furaha bila kipimo. Ukweli huo hapo juu unamaanisha kuwa kila hewa unayopumua (kama unamwamini Mwana wa Mungu na dhabihu yake au la) imekuja moja kwa moja kutoka kwa Yesu Kristo. Ni uzima wake ambao hufanya moyo wako kupiga na hukufanya upumue na unakufanya kuwa hai. Kazi zote ambazo kwa upande wetu zilionekana kama zisizo za hiari kwake kwa kweli ni za hiari. Yeye ni moyo wa kweli usemao:

---

[24] *Vines Expository Dictionary* - Enmity

[25] Tunaporejerea maisha hapa, tunazungumzia kuhusu maisha ya majaribio, sio maisha ya milele. Mungu amempa kila mtu uhai katika dunia hii kuchagua au kukataa ukweli kuhusu Mungu na Ufalme wake.

> …ili wanadamu wamtafute na huenda wakamfikia ingawa kwa kupapasa – papasa ijapokuwa kwa kweli hakai mbali na kila mmoja wetu. (28)'Kwa kuwa katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu'. Matendo 17:27,28a

Mungu hayuko mbali nasi sote kwa sababu tunadumishwa na maisha ya Yesu Kristo kwa nguvu za upatanishi wake kwetu kupitia kwa kifo chake Msalabani. Kama unajihisi mbali na Mungu ukweli ni kwamba hayuko mbali nawe. Unapaswa tu kuhisi mshipa wako kujua kwamba hajakuacha.

Ongeza katika hili ukweli huu kuwa Mungu huweka ndani yetu hamu ya kutaka kufanya mema na hamu ya kupinga maovu, basi hakika tuna mengi ya kushukuru kwayo. Fikiria kuhusu wakati umejaribiwa kufanya maovu na kisha ukafikiria uzuri wake na haukuufanya. Hii ni karama ambayo Mungu amekupa, uadui dhidi ya maovu. Haijalishi kama unamwamini Mungu au la, bado unapewa karama hii kupitia kwa Yesu unapchagua kuitenda. Tunaambiwa katika maandiko kuwa Mungu hufanya mvua kuwanyeshea wema na waovu.[26] Fikiria ni mara ngapi shetani ameweka mawazo ya uovu katika akili za mtu kutenda jambo kwako au kuchukua mali yako, na uadui unaowekwa mioyoni mwao na Mungu huwaonya wasiutende. Bila shaka bado tuna uchaguzi wa kukataa kisababishi hicho na kuendelea na kutenda uovu, lakini kama uadui huo haungekuepo hakuna hata mmoja wetu angeweza kuacha kutenda mawazo ya uovu ambayo yamewekwa ndani ya akili zetu.

Ni Baba wa ajabu namna gani kufanya haya yote kwetu! Sisi kama taifa la watu tulikuwa tumepotea na katika utumwa wa njia za uovu za Shetani. Tulikuwa tumepita kiwango cha kujiokoa wenyewe, tumepotea katika mateso na uharibifu kabisa. Lakini Baba yetu tefu wa mbinguni alikataa kutuachilia. Ametupa kitu cha thamani zaidi alichonacho – Mwanawe. Yesu atasalia kuwa mmoja wa familia ya mwanadamu na mmoja wetu. Ni dhabihu ambayo itakuwa mada kuu ya kujifunza na kutafakari katika umilele wote.

Unapowazia kuhusu mambo haya, unahisi vipi kuhusu yale yote ambayo Mungu amekutendea? Roho wake anakuvuta kwake na uweze kuamini ukweli

[26]Mathayo 5:48

kumhusu. Anataka ufahamu anakupenda sana na amekupa kila kitu ili kukurejesha kwake. Siwezi pinga upendo wa namna hii, ni waajabu kunilazimisha. Wewe je?

## 8. Kulinganisha Falme Mbili

Kabla ya kuendelea itasaidia sana kuwa na muhtasari wa falme mbili zilizopo ulimwenguni kwa sasa; Ufalme wa milele wa Mungu na ufalme wa Shetani, ambazo ziliwasilishwa kwa Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni. Tukiwaza kwa nukta kinachofafanua ufalme, kuna sifa tatu tunazohitaji kuzingatia:

1. **SERIKALI**: Mfumo ambao ufalme unatawaliwa kwao mfano, demokrasia au udikteta.
2. **SARAFU**: Mfumo wa thamani ambao kwao raia wa ufalme wanaweza badilishana bidhaa zao.
3. **URAIA**: Njia ya kuamua jinsi mtu anaweza kuwa mhusika wa ufalme.

Tunaweza tofautishi falme hizi mbili kwa njia ifuatayo:

| | Ufalme wa Mungu | Ufalme wa Shetani |
|---|---|---|
| SERIKALI | Familia | Wenye nguvu |
| SARAFU | Upendo/Huruma/Uhuru wa kuamua /Kumwamini Mungu | Uwezo/Mali/Nguvu /Kujiamini |
| URAIA | Mwana wa Mungu | Utendaji na mafanikio |

Serikali ya Mungu imejengeka kwa msingi wa mfumo wa familia. Kichwa cha serikali ni Baba. Uhusiano kati ya kiongozi na raia wake ni wa karibu na wa siri. Kwa upande mwingine ufalme wa shetani ni kuhusu kuwa mwenye nguvu. Wenye nguvu zaidi ni wale wanaotawala. Hata katika demokrasia, wale wenye nguvu katika kutangaza ujumbe wao na wenye nguvu katika kuwashawishi wapiga kura ndio watapaa uongozini.

Muundo msingi wa ufalme wa Mungu ni nguvu za mahusiano yake. Upendo ni sarafu ya mbinguni. Raia wako salama katika upendo wa Baba yao na hawahitaji kudhibitisha karama au thamani yao. Wanaweza furahia uwepo wa kila moja pasi na  kuwa na lengo fiche. Kujifunza kumjua Mungu ni furaha ya juu na azimio kuu[27], na kwa sababu ufahamu wa Mungu na hekima na tabia hazina mwisho, uwepo wa furaha hii hautaisha. Kila wakati kutakuwa na jambo la kujifunza kumhusu. Raia wake hujifunza kumhusu moja kwa moja au kupitia kwa vitu ambavyo ameviumba. Kwa hivyo kuangaliana na kutafiti maumbile na ulimwengu pia ni sehemu ya furaha ya kuwepo katika ufalme huu. Kwa kuwa imetambulikana wazi kuwa vyote hutoka kwa Baba yetu, maumbile yote humwabudu kwa furaha na shukurani.[28]

Kinyume na huu, Ufalme wa Shetani umejengeka kwa msingi wa mali. Thamani huja kutoka kwa yale tunayotimiza, hivyo ukusanyaji wa mali ni muhimu kwa kuwa na thamana. Mali hizi zinaweza kuwa vifaa, akili, au mahusiano. Kadri jumba lilivyokubwa, ndivyo unavyomiliki vitu vingi, na ndivyo ulivyo na thamani. Kadri kiwango cha elimu kilivyo juu, ndivyo sehemu ya kazi uliyonayo ilivyo juu, ndiyo ilivyo juu thamani unayomiliki. Watu unaohusiana nao ni muhimu sana kwa sababu mtu anaweza kuwa mali kubwa kwa sababu yako. Ufalme wa Shetani huamini kuwa watu wanao utawala ndani, kwa hivyo kumiliki watu kunaweza kukufanya uwe na nguvu. Mahusiano na watu yanakuwa kifaa ambacho tunapata zaidi. Hili hufanya haja ya kutaka kuwadhibiti watu muhimu zaidi. Kuna njia nyingi za kudhibiti watu wengine. Kuwa mwema na rafiki ni maarufu zaidi. Inatumika na wauzaji kila wakati. Kutenda matendo makuu kunaweza wavutia watu wengi wakufuate, na iwapo hili halitafanikiwa unaweza tumia nguvu, usaliti na vitisho kudhibiti watu na kupata utii wao. Hii ndio sababu mbona mahusiano mengi yamejawa na uchungu na huzuni hivi leo,

---


[27]Wafilipi 3:9,10

[28]Ufunuo 14:6,7; Ufunuo 4:1-9

kwa sababu mara nyingi watu wameunganika pamoja kuongeza karama na thamani yao.

Tofauti nyingine ambayo tumebainisha ni ile ya uraia. Katika ufalme wa Mungu unahesabiwa raia tu kwa kuwa mwana wa Mungu. Bila kujali hali hizo au ugumu wa maisha, ukweli huu haubadiliki. Uraia wako ni salama katika uhusiano wako kwa Mungu kama Baba yako. Katika ufalme wa Shetani unahesabiwa kuwa raia kwa kufanya au kutofanya. Mafanikio na uzembe utakupa uraia mradi tu unaangazia juu ya kufanya na kutenda. Katika ufalme huu unaamka kila asubuhi na kufikiria kile ambacho lazima kiafikiwe siku hiyo ili uweze kuhisi vizuri juu yako wewe mwenyewe kama watu wanazuia juhudi zako za kutimiza, unakatizwa tamaa na kukasirika. Kama utafika mwisho wa siku na kuhisi kuwa haujatimiza mengi, unahisi utupu na pengine unahuzunika ama kuazimia makubwa. Maisha ni mzunguko unaozunguka kwenye kiburi na kukosa maana. Unapotimiza unajawa na kiburi na unapokosa kutimiza unahisi kukosa maana. Maisha kati ya mafanikio na kushindwa ni pengine maamuzi yaliyochafuliwa ya kutimiza, au kinyume chake uoga kuwa kile ambacho umepata kitakuponyoka. Ni mzunguko ambao hauishi hadi ufe au ubadilishe ufalme.


*Mzunguko wa Hisia katika Ufalme wa Shetani*



Mzunguko huu ni matokeo mepesi ya kuamini kuwa tunazo nguvu ndani yetu wenyewe. Iwapo tumepewa nguvu basi hatumtegemei yeyote na hatupati thamani kwa yeyote. Lazima tupalilie na tuzalishe thamani yetu wenyewe. Kila fanikio linatutambulisha na kila kushindwa kunatupeleka karibu na kukosa thamani.

Nakumbuka pambano moyoni mwangu nilipoanza kufanya uwasilishaji. Nilihisi nimebarikiwa nilipowaongoza watu kwenye ukweli wa Biblia, lakini niliposimama mlangoni nikisalimia watu wakitoka nilijipata nikitaka waniambie kuwa nilifanya vyema, na kuhalalisha nilichokuwa nimefanya. Kadri nilivyohubiri vizuri ndivyo moyo wangu ulivyotaka kibali. Nilijua kuwa ni kosa kufikiria jinsi hii, hivyo kwa muda watu waliponiambia nilinena vizuri, Ningesema "Mshukuru Mungu, usinishukuru", lakini mara nyingi ilionekana sio stadi na wakati mwingine watu walihisi kuwa nilikuwa nawafukuza. Tunapotambua kuwa vitu vyote hutoka kwa Mungu na kuwa anatuthamini kando na kila kitu tunachofanya, basi tuko huru kufanikiwa na kushindwa bila wasiwasi wowote kuhusu kuhisi kukosa maana na kuhisi hitaji la uthibitisho kutoka kwa wengine.

*Mzunguko wa Hisia katika Ufalme wa Mungu*




Ni muhimu kukumbuka kuwa wakati wahusika katika ufalme wa Mungu hawapati thamani yao kutoka kwa mafanikio, bado wanafanikiwa. Kwa kweli

wana uwezo wa kuafikia hata zaidi kwa sababu iwapo watashindwa hawatakabiliana na hofu ya kukosa maana. Bado wanapendwa, bado ni wana wa Mungu fauka ya iwapo wamefanikiwa au kushindwa. Ufalme wa Mungu unakupa njia nzuri zaidi ya kufanikisha uwezo wako kamili bila kuacha mahusiano yako katika hali mbaya na thamani yako kuharibiwa.

Tumeelezea kwa kifupi hali ya falme hizi mbili. Katika sehemu hizo zingine za kitabu tutaelezea jinsi falme hizi zilivyoendelea katika wigo la historia ya mwanadamu na mapambano ambayo mara nyingi tunakumbana nayo katika kuishi kati yazo mbili. Falme zote hutupa uhuru, falme zote hutuahidi mengi, lakini ni ufalme upi ambao utakuacha na maana ya ndani ya umuhimu na thamani ambayo haitikisiki?

## 9. Moyo wa Babeli

"Tulikosea wapi?" Kilio cha kuvunjwa moyo cha baba aliyekuwa akijitahidi kuelewa ukweli ambao sasa anaushuhudia. Tumekuwa na hali nzuri ya familia na anajua tunampenda" anaendelea baba akitafuta kwa ndani maelezo kadhaa ya mbona ametiwa katika hatia ya kuuza dawa za kulevya, wizi, na mauaji.

Kilio hiki cha kuvunja moyo kimetamkwa mara nyingi sana zaidi ya vile tunavyoweza kufikiria; wazazi ambao wanaishi na aibu na uchungu wa mwana ambaye ameanguka kwa maisha ya maasi na uovu. Mwanzo wa kilio cha moyo uliovunjika unapatikana kwa wazazi wetu wa kwanza katika sikitiko la mwana wao wa kwanza Kaini. Wazazi watajua furaha ya Adamu na Hawa walioihisi walipombeba mtoto Kaini mikononi mwao. Tunda la

upendo wao lilikuwa kwao kwa kubeba na kufurahia. Wakati Hawa alibembeleza furushi lake Jipya. Alilia, “Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.”[29] Hawa aliamini kwamba Kaini atakuwa mbegu ya ahadi iliyotajwa katika Mwanzo 3:15 ambaye ataleta uponyaji na baraka katika mataifa yote. Aha kama hayo yangelikuwa ya kweli lakini dhihaka chungu kwa Hawa ni kwamba urithi wa Kaini ungelimletea huzuni, uharibifu na vifo vya mamillion. Kaini alikuwa kiongozi wa kikundi cha waabudu ambao wanafanya mambo yao ya kiroho vile wanavyotaka. Kundi hili ndilo kubwa kati ya umati wa watu duniani, ni umati wa watu ambao Bibilia baadaye inawapa jina *Babeli*. Katika sura hii tutachunguza kwa undani roho ambayo inawaongoza watu hawa na jinsi tunavyohusishwa mimi na wewe.

“Baba, mbona tunahitaji kumuua mwana kondoo asiye na hatia?” Kuchinjwa kwa mwana kondoo kulibuniwa na kuhifadhiwa katika familia ya wanadamu asili ya hisia zao kwa Kristo na kwa hivyo hitaji lao la kutubu. Inafunua gharama ambayo Mungu alikubali kulipa ili sisi tuwe na hali yetu, na kwa kupitia Roho aliyetupa, tuombe msamaha. Je ni karama ya kushangaza vipi iliyotolewa kwa wokovu wetu? Ilikuwa kanuni ya dini inayotuelekeza kwa mateso ya Kristo Wakati wa kafara. Pia ilielekeza mbele kwa tumaini wakati Kristo atakuja duniani kumfunua Baba.

Tena ilituelekeza nyuma kwa aibu ambayo wanadamu wamemfanyia Kristo tangu kuanguka huko Edeni. Pia ilikuwa ni ukumbusho wa faraja kuhusu upendo wa kustaajabisha wa Mungu. Pia ilikuwa ni ukumbusho wa uchungu kwa wanadamu kutokuwa na shukrani na ubinafsi. Kujihusisha katika hudumu hii kwa mara nyingi kunazua hisia tofauti. Kumtazama mwana kondoo asiye na hatia na kutazama mateso yake akiwa kimya ingetuonyesha gharama ya ubinafsi na ukaidi.

Kwa wale ambao wanaotazama uso wa Mwana Kondoo wa kweli wa Mungu, tumaini la kila siku litachanganywa na mateso ya nafsi ambayo inayokuja kwa kufahamu kile asili ya wanadamu inamfanyia Kristo. Jibu la asili la wanadamu kwa msalaba ni kuandika upya mwanzo wa wanadamu

[29] Usomaji halis wa Mwanzo 4:1

kwa kukana kwamba hakujawahi kuwa na kuanguka, au kuweka hitaji la kifo kwa Mungu ili kuridhisha hasira yake kwa dhambi.

Kwa visa vingi, msalaba unabadilishwa kutoka kwa mwanga na kufanywa giza, au vibaya zaidi kuonyeshwa kama mfano wa tumaini lakini kwa kweli kufanywa mfano wa kufanyiza kwa hila kunako leta machukizo.

Baada ya miaka mingi ya kuona wazazi wake wakimchinja kondoo na kuona machozi yao na huzuni iliyochanganywa na tumaini, ustahimilivu na imani yao kwa mbegu itakayo kuja, Kaini aliamua hangeendelea kuvumilia hitaji la unyenyekevu na toba. Kwa kutazama kutofaulu kwa mwanadamu kunako funuliwa na mwana kondoo aliyechinjwa, Kaini alichagua kutokumbuka upendo mkuu wa Mungu katika karama hiyo. Kwa Kaini, mwana kondoo alizua kutokuwa na ulinzi, moja ya urithi wa kuzaliwa kwake alioupata kutoka kwa babake ambaye alipokea kwa Shetani. Kwa Kaini, mwana kondoo alimwambia kukataliwa kwake na Mungu kwa haki yake, na tabia yake haikukubaliwa na Mungu. Kwa kweli, Shetani alimshawishi Kaini apige hatua ya kutoka kwa kumchinja mwana kondoo kwa ibada yake, na kuweka kwa njia nyingine uhusiano wake na Mungu kwa kutoa hitaji la kutubu na kazi yake.

Bibilia inatwambia kwamba Kaini alileta kafara ya matunda kwa Bwana.[30] Pia tunaambiwa kwamba Kaini alikuwa ni mkulima ambaye alikuza vyakula kama kazi yake. Kafara ya Kaini ilikuwa ishara ya juhudi zake kupata heshima kwa Mungu kwa kazi ya mikono yake. Alibadili ibada yake kutoka kwa imani ya unyenyekevu hadi maonyesho ya kiburi, kutoka kwa imani ya urafiki hadi mkataba wa kufurahisha.

Dini hiyo ilipuuza jambo la hakika kwamba tunauwezo wa maafikiano na Mungu; hatuna uhai wetu wenyewe wa kupumzikia na kukutana na Mungu katika masharti yetu. Huzuni ni kwamba Kaini alisahau hili. Shetani alimahidi uhuru kwa kumtoa kwa kusadikishwa dhambi na mwana kondo, lakini kwa kumtoa kondoo dini ya Kaini ilibadilika kutoka kwa uhusiano wa kiimani na Mungu wa kweli hadi imani ya utendaji wa ibada ya mungu iliyo bununiwa na yeye. Katika badiliko hili, Kaini alikubaliana na sumu ya mti wa kiini wa

---

[30] Mwanzo 4:3

Dura, alichukua ndege ya nyiririko ya kazi wakati ambapo mwanzo alihisi msisimuko wa uhuru. Ilikuwa ni jambo la mda kabla ndege hiyo ya nyiririko ifike kikomo na kupata ajali ya kuanguka chini.

Katika sura ya 5 tuliangalia baadhi ya kovu za hisia ambazo zinaletwa na kuvunjika kwa uhusiano wa kifamilia. Huu ndio muhtasari:

- Mara kwa mara kutafuta idhini.
- Wanajipatia hukumu kali.
- Hasira zao zina panda juu katika hali wasio weza kudhibiti – hivi ni kusema wanapenda sana kudhibiti.
- Wana shida na uhusiano.[31]

Wakati Kaini alienda mbali na mpango ulioteuliwa na Mungu kumtumikia, alikuwa mbali na Mungu; uhusiano wake wa kifamilia uliovunjika kabisa. Umbali huu ulitia moto uhaba wa usalama wake; Roho wa Mungu hangeweza kutuliza hofu yake au hangeweza kukanusha uongo wa Shetani. Upweke huu uliongezeka tu, na hisia za aibu ziliongezeka. Kama Shetani, Kaini angejitahidi bure kujaza pengo la hisia za kuvunjika kwa uhusiano na Mungu. Ijapokuwa alijitahidi sana, hangeliweza kuondoa hisia za ndani za upweke mpaka kwa hisia angelimrudia Mungu, ufalme Wake na mpango wake.

Misukosuko ya hisia za Kaini hivi karibuni zingeibuka. Ilifanyika katika kipindi kilichoteuliwa cha kafara, wakati Kaini na nduguye Habili walienda kumuabudu Mungu. Mungu alikubali Kafara ya Habili ya mwana kondoo aliyeteketezwa kwa moto, lakini aliacha kafara ya Kaini bila kuguswa. Hivyo pekee ndivyo ilivyohitajika kumtuma Kaini hasirani. Dhambi haifikirii sana. Kaini hafuatili maagizo na ana wasiwasi wa kutisha wakati mambo yanapo muendea mrama.

Hebu tafakari kwenda dukani na kuchukua viungo vyote vya kutengeneza mkate. Unamuuliza mwenye duka vile unavyo fanywa na anakupa orodha ya kupeleka nyumbani. Kila kitu cha enda shwari hadi wakati unaponusa chachu na unaamua kwamba mkate utakuwa bora bila chachu. Unauweka katika tanuri na baada ya mda mchache una mkate wa kuhuzunisha uliobondeka. Je,

[31] Conway, 31

kutakuwa na maana ukipaa kwa hasira na ukimbie mpaka kwa mwenye duka na kumtusi kwa sababu ya kutotengeneza mkate mzuri? Vigumu! Lakini hivi ndivyo Kaini alimfanyia Mungu.

Kaini anafikia sehemu ambayo hawezi rudi. Akiwa amekubali ufalme wa Shetani ambapo thamani yake inaamuliwa na nguvu zake na utendaji na uwezo wa kuelekezwa na unapunguwa kwa haraka. Kaini anajua ametenda jambo baya, lakini moyo wa mwanadamu ni mdanganyifu na unaweza kwa urahisi jidanganya, baadala ya kujiwasilisha kwa Mungu kwa unyenyekevu, alikuwa mkali. Kwa upole Mungu anatafuta kumsaidia kumrekebisha na anamuelekeza kwa karama ya ahadi ya Mwana Wake, lakini Kaini hasikii maonyo. Hisia zake za uasi zinakua na ufalme wa giza tayari umekamilisha jaribio lililo faulu kwa mwanadamu.

Na sasa moyo wa Kaini umetekwa na nguvu za hisia ambazo Shetani alizoachilia huko mbiguni. Anataka dhibitisho kutoka kwa Mungu lakini kwa kulingana na vile alivyotaka. Hii hali yake ya kutokuwa na maana iliongezeka hadi katika hatua ambapo alikuwa tayari kulipuka. Amepatikana katika hali mbaya ya tamaa ya dhibitisho kutoka kwa mamlaka ya juu kuridhisha tamaa yake ya kukubaliwa na thamani yake, na tena alitaka kupuuza kuwa vitu vyote vinatoka kwa Mungu na anastahili kwa unyenyekevu ashukuru kwa sababu ya upendo wake wa kumtoa Mwana kondoo. Akiwa bado anapata nguvu kwa sababu ya "kufedheheshwa mbele ya umma" mbele ya Habili, alianza kujibizana naye. Habili anamshawishi Kaini kuhusu njia yake ya ibada na anamsihi arudi katika mpango wa Mungu. Hili ndilo Kaini alikuwa akilihitaji. Kitu kilimuuma ndani. Hisia zake za kutokuwa na maana zilimpeleka hadi hatua ya kwamba hakujali tena, na wakati huo ulipofika, Shetani alipewa uhuru wa kuingia na kudhibiti. Shetani anamjaza Kaini na chuki nyingi juu ya nduguye, uhusiano wa kifamilia unasahaulika, Na ufalme wa Shetani sasa unajidhihirisha. Mbingu yote iliangalia wakati mauaji ya kwanza yalipotendeka, maangamizo ya kwanza ya uhusiano wa kwanza mtakatifu na wenye thamani. Kwa hivyo, hili ndilo lilotokea wakati sheria ya Mungu ilipovunjwa! Mbingu ilitweta na hata Shetani na malaika wake lazima walihisi ganzi kwa mda mchache walipoona mwili bila uhai wa Habili ukibadilisha mchanga kuwa mwekundu kwa damu yake.

Shetani anatikisha hofu ya kisa hiki, ili ahakikisha kuwa mtumwa wake anaweka hisia ya hatia ndani sana kwa Kaini ili asije akaamini Mungu angeliweza kumsamehe. Huu ndio uwazimu wa Shetani, anatuahidi uhuru na raha katika kumfuata kwa uasi, na wakati tunapoasi, ni sauti yake inayotaka kwa Mungu maangamizo. Na wakati huo huo ni sauti yake inatunong'onezea katika roho zetu kwamba sisi ni wenye dhambi kabisa na waasi wasio kubaliwa tena na Mungu; ni sauti yake ndiyo inayoongeza hisia zetu hadi hatua ambayo tunataka kufa. Ni huzuni kiasi gani ya kwamba huyo malaika mzuri kubadilika na kuwa mharabu myonge. Sasa vile Kaini amevuka mpaka kabisa, hana kinga ya nafsi yake Shetani anamfanya alie, "Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki."[32] Haya ni mambo ya huzuni yanayo weza kufikiriwa. Mungu alimjia Kaini si kumuacha bali kumrudisha. Alimuuliza Kaini pahali nduguye alikuweko, si kumshtaki, bali kumpatia Kaini fursa ya kutubu na amrudie Mungu. Huzuni ni kwamba Kaini alinena maneno ya maombolezo, "dhambi zangu ni nyingi kuliko za kusamehewa." Aliamini uongo wa Shetani kuliko neno la Mungu. Alipanda kwa hivyo sasa lazima avune.

Katika fungu la 11 la Mwanzo 4, Mungu anatangaza laana. Katika sehemu ya mwisho ya laana, Mungu anamwaambia Kaini kwamba atakuwa mtoro na hatakuwa na kikao duniani. Maneno haya yanamzungumzia Yule ambaye anayetingika na kukongoja, inapeana hisia za mtu ambaye hana tumaini na siku za baadaye. Laana hii haikufanyishwa na Mungu kwa kuacha baadhi ya nguvu za mbingu, bali hiyo laana ilikuwa ni ya asili ya kukataa ufalme wa familia ya Mungu, asili ya kukataa uhusiano wa karibu. Nafsi yake iliteseka kwa sababu aliumbwa kwa uhusiano. Lakini moyo wake ulichagua njia nyingine- akawa ana hamu ya upendo Ijapokuwa aliwakataa wale waliokuwa karibu naye. Alikuwa anataka uhusiano wa karibu lakini hakuwaruhusu watu waje katika sehemu ya siri ya moyo wake pahali kutokuwa na thamani kulikuwa na makaazi. Alikuwa anataka marafiki lakini alihofia mpinzani wa uwezo wake. Hapa ndipo ukweli wa msemo unapatikana "Hapana amani kwa waovu; asema Mungu wangu." [33]

---

[32] Mwanzo 4:13 – Marginal reading.

[33] Isaya 57:20

Bibilia inatuambia kwamba Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana.[34] Aliishi bila hisia za Mungu kuwa karibu na yeye. Kwa kuamini kwamba dhambi zake zilimfunga nje ya Mungu, yeye kwa kweli alimfungia Mungu nje ya maisha yake. Na akiwa na hitaji kubwa la idhini na thamani, alianza kujenga mji. Angeliwakusanya watu karibu naye na awe kiongozi wao. Angelijenga mijengo mikubwa na apate thamani yake kwa kile alichokifikia. Angelijizungusha na kazi ya mikono yake na kuzuia katika fahamu yake, kama vile inavyowezekana, ushahidi wa kazi ya Mungu. Angelijishugulisha na kazi nyingi hadi hatua ambayo hana mda wakujiuliza kuhusu hali ya nafsi yake.

Na kaini alikuwa ni chombo cha kuanzisha ufalme wa Shetani duniani, Kwa kupitia kwake kizazi cha watu kiliendelea ambao walionyesha ishara zote za kutokuwa na kinga na kutokuwa na thamani. Walikuwa ni wanaotafuta mamlaka na vyeo, wakiendeleza roho ya kudhibiti ambayo ilikuwa na chuki ya upinzani wowote, katika harakati za kutafuta utambulisho usiokuwa na mwisho kando na Mungu aliyeziumba mbingu na nchi. Wakati ambapo Shetani anawaweka watu kutafuta thamani ndani yao kuliko mikononi mwa mkuu wa uhusiano na Mungu binafsi, angiliwadhibiti. Na hivyo amefanya. Tangu hapo awali Shetani amekuwa na darasa la watu alilowanasa akiziweka pamoja roho zisizokuwa na thamani, zisizokuwa na kinga dhidi yake na akitafuta kutawala dunia.

Tumesoma kiini cha Babeli. Moyo ulioteswa unaotafuta utambulisho na thamani kwa kile kitendacho, kutafuta dhibitisho, na ikijaribu kudanganya vile hali ilivyo ili isitishwe. Katika sura inayofuata tutafuatilia maendeleo ya moyo huu wa mwili katika historia ya mwanadamu.

---

[34] Mwanzo 4:16

# Sehemu 2. Hatima Mmoja
# – Utambulisho Kurejeshwa

## 10. Kuvunja Minyororo ya (Kiini cha Dura) Duracell

Kulikuwa kimya kwa mda mrefu walipokumbatiana. Wingi wa hisia zilienda kwa undani, lakini wote walijua mda umefika. Kuanzia siku za milele Baba na Mwana Walikuwa na ushirika wa karibu, na ushirika ulikuwa karibu kuwa na dhiki na mwishowe kuvunjika. Mwana wa Mungu alikuwa aanze kazi yake ya kuwarudisha wana wake na binti zake wa kibinadamu. Wote, Baba na Mwana walifahamu hatari na garama husika lakini upendo unawaendesha wote.

Kwa wakati mfupi, Baba na Mwana waliangalia siku za usoni na kwa macho ya kinabii walitazama kazi ikifunuka. Kudharauliwa, kukataliwa, kuchukiwa, kutemewa mate, kupigwa teke, kichapo, na misumari yote haungelinganisha na huo wakati mbaya ambapo kulikuwa kimya mbinguni na duniani Baba na

Mwana wakitengana. Mwana aliona millennia ya hatia, mateso, uasi na kutokuwa na thamani ya kuishi amekwisha wekewa na anaangalia ili ajione ametikiswa kama jani, amepasuliwa na kuraruliwa na hisia za uso wa Baba uliofichwa uliosababishwa na dhambi. Baba yuko pamoja na Mwana katika giza lakini ni Mwana anaye beba hisia za upweke katika uoga wa kifo. [35]

Kukumbatiana kuna kazwa- Inawezekanaje Baba amtoe kwa hatima hii? Kwa kiwango cha kindani, wote wanamenyana na uwezekano wa kutofua dafu na kupotea milele kwa nguvu za dhambi. Mwana wa Mungu angelichukua asili ya kibinadamu mwenyewe na kupeana fursa ya mwanya wa dirisha kwa mpinzani wake mkuu, Shetani, ili amweze. Hakukuwa na dhamana ya kufaulu. Je wangeliweza Kujihusisha na hatari kali. Je, wangelikaribishaje mpango wa kupumua? Walakini upendo ndio unao waendesha.

Kimya kwa mda mrefu kilioonekana milele mwishowe kinaisha; Wote wanakubalia kutekeleza mpango huo. Mwana anasonga mwisho wa mbingu, kisha anangalia uso wa upendo wa Baba na anaenda.

Katika sura ya 6 Tuliangalia orodha ndefu iliyo na changamoto ambayo Mungu alistahili kufanywa kama angeliokoa wana wake na binti Zake duniani. Katika sura ya tisa tuliona kuendelea kwa ufalme wa Shetani katika moyo wa mwanadamu na vile Shetani anatutawala kupitia hisia zetu za kutokuwa na thamani. Kama Yesu angelivunja hizo nguvu. Lazima angelitoa hizo hisia za kutokuwa na thamani. Ni lazima aunganishe tena hisia zetu za utambulisho kama wana wa Mungu na ashinde utambulisho wa uongo unaotokana na mti wa kiini cha Dura.

Hisia za ndani za kutazamia lazima zilinasa moyo wa Shetani alivyo waangalia malaika wakiimba wimbo wa furaha kwa wachungaji wa kondoo kwamba Masihi amekuja. Hiyo nyota ing'aayo iliyowaongoza mamajuzi hadi horini haikuongeza faraja. Unaweza tafakari alipomtazama huyu mtoto mdogo alijua kwamba yuko vitani. Hakuweza Kuvunja hiyo amani tulivu iliyokuwa juu ya mtoto, ambaye angeliweza kuwafanyia kila mtoto mwenye thamani. Ilishangaza, mwana alifanywa na mwili na damu lakini amani ya ndani ilikuwa

35 Waebrania 2:9

juu ya huyu mwana ambaye hangeliweza kamwe kumsumbua. Shetani alijua yuko katika shida.

Shida hii ilikuwa moyoni mwa Herode na tunapewa dirisha la mtikisiko uliokoroga ulimwengu wa kiroho wa giza. Hisia za kutokuwa na kinga zilimfanya Herode kunaswa kwa urahisi na Shetani, mshtuko na hofu na kampeni dhidi ya ufalme wa mbinguni. Angelimtoa kabla ya mashindano kamili kuanza. Lakini amani imara ya mtoto Mfalme haikuwekwa kwengine. Riziki ilitoa njia ya kutoroka kwake ili afunue ukweli kuhusu babaye, kumfunua kiongozi wa giza, na katika mwili wa kibinadamu avunje Minyororo ya kutokuwa na kinga iliyoshika kizazi cha wanadamu kilichopotea.

Maisha ya Yesu yanaweza kufanywa kwa muhtasari kwa maneno haya:

> Yeye aliyenituma yu pamoja nami, hajaniacha, kwa kuwa siku zote nafanya mapenzi Yake.' Yohana 8:29

Haikujalisha kile Shetani alifanya, angeliweza Kuvunja hizo hisia za heshima na ujasiri. Kristo alishikilia urithi wake kama Mwana wa Mungu mshikamano ambao ulimshangaza mkuu wa giza. Shetani alikasirika katika juhudi zake za bure kumfanya Kristo atende dhambi. Hatimaye mtu ambaye angelimpinga Shetani. Baada ya miaka elfu nne ya kufaulu kwa kila mtu. Shetani anagonga ukuta wa mawe wa nafsi ya mwanadamu ambaye anaujasiri kuhusu Wana Wake kwa Mungu. Hali ya Mwana wa Mungu ndiyo ilikuwa muhimu kwa ushindi; Kuwa Mwana wa Mungu ndio ilikuwa boma na kinga la hakika kuhusu mvua ya kutokuwa na hakika ambayo iliyokuwa ikizamisha kizazi cha wanadamu, kwa hivyo kuwa Mwana wa Mungu ndiyo ilikuwa kiini cha mapambano kati ya Kristo na mpinzani wake.

Mji wa Nazareti umepata mapigo ya msisimuko. Habari ya mbatizaji inaenea kwa haraka. Mtangulizi wa Masihi alikuja, na ujumbe unapofika katika duka la seremala mnyenyekevu, Yesu alijua kwamba wakati wa kumtukuza Baba umewadia. Anaweka Patasi na msumeno chini, anamkumbatia mamake kisha anaelekea Yordani.

Yesu anauhakika kuhusu kuwa Mwana, lakini vita vijavyo jangwani vitamjaribu kuliko binadamu yeyote amewahi kujaribiwa. Milango ya taabu ya

wanadamu itaachiliwa na kuelekezwa Kwake kama Bwawa lililopasuka. Yesu lazima akumbane na nguvu za mwanadamu kutokuwa na thamani na abaki imara. Kama angeliweza kusimama imara basi kwa mara ya kwanza mtu angeliweza kuvunja Minyororo ya kiini cha Dura. Alivyo viteka nyara kwa sababu ya ushindi wake vitakuwa urithi wa wale wanaomwamini.

Vita jangwani vilikuwa ni msingi wa kazi ya msalaba. Je, kafara ilikuwa na maana gani kama nafsi ya mwanadamu haingeweza kuvunja Minyororo ya kutokuwa na kitu? Je, ufunuo mzuri wa upendo unafaida gani kama hakuna mwanamume, mwanamke, au mtoto ambaye anauwezo wa kukubali karama? - hakuna! Kutokuwa na thamani au kutokuwa na kitu cha kiini cha Dura lazima kushindwe na vilivyo tekwa nyara viwekwe mikononi mwa kizazi cha binadamu ili wote wawezeshwe kukubali karama ya msalaba isiyokuwa na kifani na kwa kweli waamini kwamba Mungu anawapenda na kuwasamehe.

Baba anajua kile kinacho kuja na atatia nguvu mkono wa Mwana wake kwa vita, si kwa kujionyesha kwa hali ya juu, si kwa kutumia jeshi lililo na silaha. Hakuna baadhi ya hizi zingeliweza kukutana na adui anaye kuja. Mungu anatoa silaha yake bora - uwezeshaji unaokuja kutokana na uhusiano wenyewe kwa wenyewe. Yesu anapotoka majini, na njiwa anateremka, na mbingu ina funguka na Yesu anasikia vizuri sauti ya Baba Yake, **"Huyu ni mwanangu mpendwa ambaye ninapendezwa naye."** Haya ni maneno makali ambayo Baba angelimkabidhi Mwana Wake ya kufanya vita. Akiwa salama katika maneno ya Baba Yake, angelipambana na huyo adui na avunje Minyororo ya dhambi kwa niaba yetu ambayo hatungeweza kuvunja, umuhimu wa kauli hii unaenda kwa undani kuliko vile wengi wangelidhania. Ukweli ambao Mungu anakubali mmoja wa wanadamu unatupatia tumaini la ajabu kwa sisi sote. Kwa kupitia kwa Yesu, Mungu anatufikia sisi sote na anatuambia sisi ni wana Wake wapendwa. Kama tunatumaini kukubali karama ya msalaba ni lazima tusikie maneno hayo, "Huyu ni mwanangu mpendwa ambaye ninapendezwa naye." Ni vigumu kupokea zawadi kutoka kwa adui bila kushangaa kama haijachanganywa na sumu au ina masharti, na zawadi kutoka kwa mmoja wa familia inakubalika vile ilivyo – zawadi, safi na rahisi. Hakuna njia nyingine ya kukaribia msalaba ila ya daraja ya imani yetu thabiti kuhusu uwana wetu au ubinti wetu kwa Mungu. Njia zingine zote zitatuongoza kwa njia ya kufuata sheria au leseni ya dhambi.

Maneno hayo kutoka mbinguni lazima yalimkasirisha Shetani. Kumbusho la vile alikuwa lakini sasa hayuko hivyo - mwana! Ilikuwa ni ukumbusho wa vile yuko bure na hana kitu. Likini kiburi hakifi kwa urahisi, na kwa hivyo Shetani anajitayarisha kutoa majaribu yake kwa Yesu huko jangwani.

Imenakiliwa katika Bibilia kuwa Yesu "alikuwa jangwani siku arubaini, akijaribiwa na Shetani." [36] Nafikiria watu wengi wanapata dakika kumi peke yake za majaribu mara kwa mara zikiwalemea, ukiachwa siku arubaini! Shetani amekuwa na miaka elfu nne ya kufanya mazoezi ya kujaribu ili aipate vizuri na unaweza kuhakikishiwa kwamba Yesu alikuwa akilengwa na kila silaha kutoka kuzimuni. Nani anaweza kufahamu undani wa hivi vita? Ulimwengu wote ulishika mkusanyiko wa pumzi yao wakati Shetani akimweka Mwana wa Mungu ngumi baada ya ngumi. Lakini sisi tulikuwa tumelala, tukiwa tumesahau msimamo wa ushindi uliofanywa na Yesu ili kutuweka huru. Kama Yesu angefaulu, sisi sote tungepondwa na Minyororo ya kutokuwa na kitu. Yesu tu ndiye alikuwa ni tumaini letu la kutoboa giza.

Nikifikia hatua kama hii inanilazimu kusimama na kumfikiria. Niseme nini? Moyo wangu umejaa hadi ukingoni na furaha ya shukurani kwa juhudi zake bila kuchoka huyu Mfalme wa nguvu kwa kutusaidia katika dhambi zetu katika hali mbaya. Ni kama baba au mama ambaye angelikimbia kupitia nyumba inayoteketea kumnusuru mtoto anaye chomeka. Alikuwa karibu apondwe akilini lakini angeweza kuachilia hali yake ya kuwa Mwana wa Mungu. Huyu mtu anafanya kitu ndani yangu kulia "Niko na thamani. Hakuna mtu anayeweza kufanya hivi kama kweli hawajali!" Nakuambia upendo huu unanivuta kwa njia ambayo siwezi kukataa. Ninamkataa lakini anajuhudi kuniliko!

Wakati Yesu yuko katika mazingira magumu – kuchoka, njaa, upweke, vitu vyote ambavyo vinawafanya wanadamu kukata tamaa - Shetani anakuja kumsulubisha kwa mambo haya. "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, ambia haya mawe ya geuke kuwa mkate." [37] Hilo jaribio lilikuwa la nini isipokuwa kuwa Mwana wa Mungu? Yesu hakuambiwa ni kwa mda gani atakuwa jangwani; nakala haisemi kwamba aliambiwa baada ya siku arubaini jangwani

---

36 Marko 1:13

37 Mathayo 4:3 NIV

yote yataisha. Yesu alikuwa huko nje na hakuna kunguru ambaye alikuja kumlisha. Hakukuwa na mkate kutoka mbinguni. Labda alikuwa amefanya makosa kuhusu sauti iliyotoka mbinguni? “Babako hangependa ubaki katika hali hii. Hebu fanya kitu juu ya hali hii” Shetani alimnong’onezea.

Shetani alikuwa akitumia njia ya hamu ya chakula ili kuvunja imani ya Yesu kwa neno la Babake. Siku arubaini hapo awali, Mungu alisema “Huyu ni mwanangu mpendwa ambaye ninapendezwa naye.” Kama Yesu angeligeuza mawe kuwa mikate basi angelikuwa na tashwishi kuhusu kuwa kwake Mwana wa Mungu, na hiyo tashwishi ilikuwa imetosha kuchafua utambulisho wake. Zaidi ya hayo, Kumwambia Yesu abadilishe mawe kuwa mkate ili kuthibitisha alikuwa nani ilikuwa mlango wa hakika wa ufalme wa Shetani – utambulisho kupitia utendaji na mafanikio.

Je wangapi kati yetu ambao hawajaanguka katika mtego huu wa kuthibitisha thamani yetu kwa mafanikio yetu. Kuongozwa kuonyeshwa ya kwamba una kila kinacho hitajika kufika juu. Kupuuza usingizi na kupumzika na kushinda yote saa ya sala na kusoma Bibilia, kukaa sana ofisini na kukosa saa nzuri ya familia – ili kuongezwa cheo au fedha za ziada. Kwa nini tunajisukuma sana? Kwa visa vingi ninaona tunajaribu kusuluhisha, “Kama wewe ni mwana au ni binti ya Mungu, fanya kitu kikuu ili kuthibitisha.”

Je, unapata wakati unapo amka asubuhi na ungependa uwe na mda mchache wa kutafakari na kuwa na Mungu. Na kichwa chako kina anza kujawa na vitu vinavyostahili kufanywa hiyo siku, hadi inafika wakati hauwezi kuchukua mengine na unaachilia na maombi ya dakika tano na unataka kwenda kuanza siku. Je, hili linakufanyikia? Kwa nini? Kama umefika mwisho wa siku na umepata haujafikia mengi sana, lakini umetosheka na una furaha, au unahisi kuudhika na pia una dhiki kidogo? Je unakata tamaa kwa “kupoteza mda” ukilala katika kitanda cha wagonjwa, ambapo ungekuwa unatoa vitu katika orodha vitu vya kutekeleza, Hivi vitu vyote vina tuelekeza katika ukweli kwamba sote isipokuwa hata mmoja tumeanguka katika majaribu ya Shetani ilikuthibitisha utambulisho na thamani kwa kile tunachotenda. Kwa sababu ya ukweli ya kwamba ndani yetu tunabeba kutokuwa na usalama tuliopitishiwa kutoka kwa Adamu na Hawa, tunalengwa kwa urahisi kwa kutaka kufanya majani ya mti wa kiroho na kiakili ili tujisitiri. Mtu anayekosa usalama kila siku atajibu changamoto ya utambulisho wakati mtu aliye salama

hatajishughulisha. Inanikumbusha wakati mmoja nilikuwa natembea na rafiki yangu aliyekuwa na mbwa mdogo. Tulipita karibu na makao ya jirani yangu ambaye alikuwa na mbwa mdogo zaidi. Mbwa mdogo alikuwa akibweka na kupiga na kukimbia hapa na pale ili kutambulika na yule mbwa mdogo. Yule mbwa mdogo hakugeuza kichwa chake ili kumwangalia yule mbwa mdogo zaidi. Nilihisi kwamba mbwa mdogo alikuwa akisema, "Kuja wewe mbwa mkubwa wangu nitapambana nawe ili kumwonyesha bwana wangu kwamba naweza kumpiga mbwa mkubwa kama wewe." Mbwa mkubwa alikuwa na ujasiri kuhusu vile alivyokuwa na hakujibu changamoto, ni nini ingelimuongezea thamani yake.

Ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba Yesu ilibidi aende jangwani kujaribiwa. Familia ya wanadamu ilikuwa inamtaka mtu ambaye angelionyesha kwamba aliamini kwamba yeye ni mwana wa Mungu kwa sababu Mungu amesema baadala ya kutaka kuonyeshwa kwa matendo yake aliyoyafanya. Ulimwengu ulikuwa unamhitaji Daudi ilikupambana na Goliathi asiye weza kushindwa, wakutokuwa na thamani ambaye anatufunga kwa dhambi zetu na kutufanya watumwa wa Ibilisi.

Kwa kweli kisa cha majaribu ya Yesu jangwani kinafanana sana na kisa cha Daudi na Goliathi:

1. Shetani kama kiumbe cha kiroho, na hali nzuri juu ya Yesu aliyepungukiwa na asili ya mwanadamu. 1 Samueli 17:33

2. Yesu aliwakilisha wanadamu wote na ushindi wa Kristo ulimaanisha uhuru kwetu sisi kama vile Shetani alivyosimamia nguvu zote za giza na ushindi wake ulimaanisha kwamba tungebaki watumwa wa nguvu za giza.1Samueli 17:9

3. Yesu alikuwa siku arubaini jangwani akikumbana na dharau na majaribu ya Shetani kama vile Goliathi alidharau Israeli siku arubaini. 1 Samueli 17:16

4. Shetani/Goliathi walikuja kwa nguvu zao wenyewe lakini Yesu/ Daudi walikuja kwa jina la Bwana kumfunua Baba na kumfichua yeye ambaye aliyetukana jeshi la Mungu aliyehai. 1 Samueli 17:45

5. Silaha ambazo Yesu alitumia zilikuwa dhaifu kulingana na kiwango cha dunia- aliamini maneno ya Mungu akitumia hayo maneno kwa usahihi kufichua fikira za Shetani.

Usambamba ni wa ajabu, siwezi kujizui bali kujiweka kama hayo majeshi ya Israeli wanaosimama upande wa mlima, wakimsikia Goliathi akimkufuru Mungu wangu, dini yangu, na mimi pia. "Mungu wako yuko wapi? Kwa nini usipigane nami kama yeye ana nguvu, wewe ni mnyonge na bure na aibu kwa Mungu wako? Kusikia matusi haya kwa siku arubaini yatanifanya niwe na dhiki. Hebu angalia ukubwa wake! Silaha zake zinang'a katika mwanga wa jua na sauti yake kuu ikiwa bado inatoa matusi pande zote za bonde. Hali inaonekana bila tumaini, na kuna hisia za kuzama kwa utumwa. Je, kuna tofauti leo? Tuna matusi ya Shetani kuhusu kutokuwa na uwezo na unyonge wetu. Majaribu yake yanaonekana yenye nguvu na tunaanguka kwayo kila mara. Na kuna hizo hisia za kuzama kwa utumwa. Kuna wale ambao wanahubiri kwamba utumwa wetu hautaisha kwamba dhambi kila siku itatuteka; Ni huzuni ya utumwa wa dhambi. Mwana wa Daudi yuko katika kambi yetu. Ametufungua kwa Minyororo ya Ibilisi. Ushindi wake jangwani ni ushindi wa familia ya wanadamu. Unaweza kufikiria ya kwamba lazima ukumbane na Goliathi, au unaweza kuangalia kwa mshangao ukiwa upande wa mlima na Yesu akiwa kiongozi katika majaribu. Kama unaamini tayari una ushindi kwa ajili ya Yesu, baada ya kutumaini kwamba atakuokua, basi umepata msalaba wa imani.

Nina furaha ya kwamba Mwana wa Daudi ameniweka huru kutokana na kutokuwa na nguvu na thamani. Ametoa moyo wa kuasi na kiburi. Ameweka miguu yangu katika mwamba usiotingisika unaojulikana kama mwana wa Mungu. Yeye mwenyewe amekumbana na tashwishi kwa niaba yangu na akanishindia kwa imani ya neno la Baba yetu. Imbeni na mfurahi nami enyi wana na binti za Mungu. Yesu alizivunja kwa mshindo Minyororo ya Kiini cha Dura na kutufanya tukubalike katika mpendwa.

## 11. Kufungua Malango ya mbingu.

Kipande cha mwanga kinapasua giza kuonyesha kwamba alfajiri imefika. Pia inaonyesha kwamba wakati wakazi inayostahili kuanza. Mapigo ya moyo yanaongezeka, pumzi inafupika, wakati, maandalizi yanafanywa kwa ajili ya safari. Wakianza safari alfajiri, Moyo wa Ibrahimu umejawa na kumbukumbu. Anakumbuka kumshika Isaka kwa mara ya kwanza na hisia kubwa sana za furaha zilizotolewa baada ya kungoja kwa mda mrefu. Kumbukumbu za Isaka mdogo akirukaruka katika kitanda cha babake na akimkaribia akisikiza kwa makini hadithi za Adamu na Hawa na zenginezo, imekuwa kama mzigo mzito mabegani akitafakari kasi iliyoko mbele yake, alivyosikia Mungu akisema:

> "Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmoja wapo nitakaokuambia. Mwanzo 22:2

Mungu alinena na Ibrahimu sasa anaita nguvu zake zote ili atii amri zake. Hukuna maelezo wala sababu aliyopewa, amri tu. Miaka yote Ibrahimu alitembea na Mungu, Alijifunza kutokataa amri zake. Alifikia kuamini kwamba Mungu anajua kilicho kizuri na Alikuwa njia iliyo salama ya kufuata. Lakini njia ilikua ngumu, ngumu isiyoweza kufikiriwa!

Ni nani anayeweza kuelewa mapampano yaliyokuwa yakikamata fikira za Ibrahimu. Angelifurahia kuwa kafara baadala ya mtoto wake. Hakuna kitu hangefanya kumuokoa mwana wake katika kisa hicho. Adamu anapumua kwa

nguvu na anapambana kuficha uchungu wake kwa Isaka. Hii inakuwa kama ndoto mbaya ambayo hivi karibuni itapita. Ukweli unamuingilia Isaka akiuliza, "Baba, tuko na kuni na moto, je kafara iko wapi? mshale unagonga moyo wa Ibrahimu. Je atamjibu vipi? Maombi ya haraka yanamwendea Mungu ili kupata hekima, kisha Ibrahimu anajibu, "Mungu atatoa kafara" [38]

Juu ya mlima, Ibrahimu kwa uchungu anamfunulia Isaka kuelewa kwake amri za Mungu. Isaka alikuwa kijana mdogo ambaye angelimshinda babake kisha akimbie na akimbie kabisa lakini Isaka Alijifunza nidhamu ya utiifu na anawacha dhamira yake kwa hekima ya baba yake.

Mbingu yote inaangalia wakati Ibrahimu anamtayarisha mwana wake, mwana wake wa thamani kwa mda huo wa mwisho. Fikira za kibinadamu zinaachilia betri la majadiliano dhidi ya imani, lakini Ibrahimu akisimama kama mti wa mwerezi katika kimbunga cha upepo, anainama lakini hakubali kushindwa bali ameamua kutekeleza ufahamu wake kwa ombi alilopewa. [39]

Kila kitu kiko tayari na Ibrahimu anamwaangalia chini mwana wake. Uchungu unapasua moyo wake na nguvu zake zinaanza kuisha, lakini anashikilia. Anaomba na anaweka fikira zake kupiga kwa kisu ambacho kitamaliza maisha ya mwana wake mwenye thamani.

Wakati huo sauti inasikika "Ibrahimu! Usiweke mikono yako juu ya huyu mtoto, kwa maana sasa najua unamcha Mungu."

Wakati ninapotafakari hadithi hii, Siwezi kujizuia bali kujiweka katika viatu vya Ibrahimu na mwana wangu kwa viatu vya Isaka. Ninajaribu kushika kuelewa shida alioihisi, lakini hiyo picha kwa haraka inasimamishwa. Kuna kitu ndani kabisa ambacho kinafika juu na kuzuia picha kumaliza kutengenezwa. Kihisia fikira zangu haziwezi kushika mkasa huo.

Kushika hofu na kafara ya Yesu msalabani tunahitaji kuonyeshwa undani wa uhusiano kati ya Baba na Mwana. Hiyo ni muhimu sana katika ufalme Wao. Ni mfano kati Yao, kiini cha mtazamo wao wa maisha kati Yao ambao

---

38 Mwanzo 22:7-8

39Angalia *Agape* Ukurasa 24 – Ibrahimu na chukizo la ukiwa. Katika baba wa upendo.info(fatheroflove.info)

unaofunua upendo ambao wako nao kati yao. Kama hatutaongeza mtazamo huu wa uhusiano basi tumepotoka katika kidokezi hiki.

> ‘‘Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele Yohana 3:16

Mateso ya uhusiano wa thamani ndilo jambo la uharibifu ambalo mtu anaweza kushuhudia. Fikira za kutengana kwa huo umoja tunaopenda ndio uoga uliofungwa ndani ya mioyo ya kila nafsi yetu. Ninapata ya kwamba baada ya kuwa mbali na familia yangu kwa wiki moja kwa kazi ya kuhubiri, moyo wangu unatamani kuwa nyumbani na wale ni wapendao.

Hakuna kitu hapa duniani ambacho naweza kubadilisha na familia yangu. Hata wazo hilo linanifanya kuwa mgonjwa, na tukitazama moyo wa Mungu, vile imefunuliwa katika Bibilia, tunapata yakuwa Mungu Baba yetu na Mwana Wake walikubali kuhatarisha uhusiano wao, ili mimi na wewe tunaweza kupitia malango ya mbinguni na tuunganishwe tena na Muumba wetu na Mwanawe.

Mtu anaweza jibu, “ Ndio, lakini Yesu alijua atafufuka  tena na aunganike na Babake, kwa hivyo haikuwa mbaya hivyo.” Kama umetumbuiza mawazo haya, “Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha?” Wakati hatia ya uasi wa dunia ilisukumwa kwake na upendo wa basi ninakushauri umuulize Yesu vile alivyohisi wakati alipopiga nduru,  Babake ulifichwa kwa wanadamu kutoamini msamaha wa Mungu wa dhambi, Yesu alitafuta kwa uweusi ilikupata uso wa upendo ambao ulikuwa furaha Yake tangu milele, lakini dhambi ilificha uso wa Babake hadi alihisi alitenganishwa naye kabisa. Tumaini lake lilimezwa, kifo tu ndicho kilikuwa kinamngoja; alihisi kwamba atatenganishwa milele na yule aliyekuwa akimpenda na ndio maana alilia, “Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha?” Hebu fikiria hilo kwa dakika moja; ni uhamasisho wa ajabu! Mungu hakumuacha Mwanawe, bali uzito wa dhambi zetu juu ya Yesu ulimfanya  ahisi vile wenye dhambi wangelihisi kwa sababu ya hatia.

Katika sura ya 9 tulisoma kuhusu Kaini aliyelia, “dhambi zangu ni nyingi kuliko vile naweza kusamehewa” Yesu alibeba haya msalabani kwa ajili yetu,

dhambi zetu zinatufanya tuhisi kwamba Mungu yuko dhidi yetu na anahamu ya kutuua kwa dhambi zetu, lakini Mungu alipongeza upendo Wake kwetu na alimuacha Mwana wake apitie uzoefu huu kwa ajili yetu ili tuammini tunaweza samehewa.

Haya yote yanaomba swala, je, Mungu anatilia mkazo kiasi gani kuja vizuizi kati Yake na sisi? Katika historia ya Ibrahimu na Isaka tunaona picha ya Mungu na Mwana wake.

Ni asili yetu pamoja na Ibrahimu, kufikiria kwamba Mungu alitaka kumuua Mwana wake. Mungu alimuambia Ibrahimu amtoe mwana wake kafara, na Ibrahimu alielewa hii inamaanisha kumuua mwana wake kwa sababu hii inaonyesha mawazo yetu sisi wanadamu kuhusu hukumu ya dhambi.

Kwa hakika vile Mungu alimzuia Ibrahimu kumuua mwanawe inamaanisha kwamba ilikuwa si nia yake, lakini katika hali hii Ibrahimu alionyesha imani kwamba alikuwa tayari kuacha yote aliyokuwa akipenda ili amchukue Mungu. Wakati Mungu alipopeana kondoo wakiume kama badilisho, tunaona yakuwa Mungu alipeana badilisho la fikira za mwanadamu kuhusu hukumu. Mungu alikubali Mwana Wake atengwe na Yeye ilitukubali kwamba tumesamehewa dhambi zetu.

Katika tetemeko na giza la siku hiyo ya kutisha wakati upendo mkuu ambao haujawahi kuwa ulifarakishwa kwa ajili ya dhambi zetu, ninasikia kilio cha Baba, "Mwana Wangu, Mwana Wangu, nitawezaje kukuacha?" Nitakuacha aje uende?" Hii ni kuzimuni papa hapa. Wote Baba na Mwana wameona kuzimu kwa kufarikishwa kwa uhusiano wao kwa ajili yetu. Walilipia garama ambayo tunaelewa inastahili kulipiwa. Je, nini kiini cha kuzimu kinaweza kuwa bali ni kile kinyume cha ufalme wa Mungu kinasimamia kwa upendo na uhusiano wa karibu?

Je hii inamaanisha nini kwetu? Inamaanisha ya kwamba Mwana wa Mungu ameonja hofu ya utengano kwa upendo wa kiungu kwa niaba yetu, ili sisi isitupate tena. "Kuko wapi Ewe mauti kushinda kwako? Uko wapi Ewe mauti uchungu wako?" [40]

40 1 Wakorintho 15:55

Sasa hakuna kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu? Kwa sababu ya kile Yesu na Mungu wametutendea. Kafara na sadaka ilikuwa haihitajiki na Mungu, lakini ili tujuwe tumesamehewa Mungu alilipa garama ya juu.

Mbawa za malango ya mbingu yanatufungukia kwa sababu Mwana wa Mungu alipitia kupondwa kwa uzito wa kuzimuni ili kufunga malango yake. Hatuhitaji kuingia pale na kupitia kilio na kusaga meno, kama vile itawafanyikia wale ambao wamekana kile ambacho Yesu ametutendea na wanajifarikisha na upendo wa Mungu.

Chanagamoto ambayo imebaki kwetu sisi sasa ni kufanya hiyo safari katika mioyo yetu katika hali ambayo tunahisi bila bei, dharaulifu na kushurutisha, (kutafuta utambulisho kwa kile tunachofanya) tumrudie mwenye uhai, pahali ambapo upendo unatungoja na tunajua sisi ni wana Wake wapendwa. Ijapokuwa Yesu alifungua malango a mbinguni kwetu, lazima tufanye safari kutoka ufalme wa kiini cha Dura hadi ufalme wa Mungu, kutoka utambulisho kwa yale tunayoyafanya binafsi kufaulu hadi utambulisho kwa njia ya kuwa wana wa Mungu au kwa njia nyinigne kutoka kwa wokovu kwa kupitia matendo hadi wokovu kwa imani. Sehemu ambazo zime baki kwa kitabu hiki zitaaangazia changamoto na mapendeleo ya safari hii.

# Sehemu ya 3 – Safari ya Kurudi Kuwa Mwana

## 12. Maisha yanayo Wezeshwa na Kiini cha Dura.

Hewa ya matumaini inapenya na kuenea kote kwenye chumba. Nimekaa na wanafunzi wenzangu katika pahali pa kusikiza hotuba na tunahamu ya kusikia jina tunalolijua. Shule ilikuwa ikipeana tuzo tofauti tofauti kwa wanafunzi waliofanya bora mwakani. Katika tukio hili, nilicheza mchezo mdogo wakufurahisha mawazoni.Nilifanya bidii mwaka huo wa masomo yangu na vile nilijiambia kwamba haijalishi, ndani yangu hamu ilikuwa. “Umefanya bidii mwaka huu, unaweza pata tuzo inayofuata... hakuna, mtu mwingine atashinda… lakina una fursa.” Wakati ulipowadia jina kutangazwa, moyo wangu ukaanza kudunda kwa haraka kwa matazamio na ninasikia jina; si langu bali la mmoja wa marafiki zangu.

Hii ndio sehemu ya kufurahisha, nje ninampigia rafiki yangu makofi kwa kufaulu kwake, ndani jambo tofauti linatendeka:” kwa nini alipata hiyo? Nilifanya bidii kumliko, siwezi kuamini kwamba wangelimpatia. Aa ninafikiria ninajua kwa nini. Ana uhusiano na mmoja wa walimu na ndio maana walimchagua. Matokeo yalifanyiwa hila! Si kile unachojua bali ni yule unayemjua. Wakati huo ninapiga makofi na kutabasamu ni kijaribu kuwa shwari. Wingu linaanza kutanda na kwa saa chache zilizosalia ni naanza kuhisi huzuni na kukasirika kidogo. Ni siku nyingine ya maisha yanayowezeshwa na kiini cha Dura.

Haimchukui mtoto mda mrefu kujua kwamba kama anastahili kuwa na thamani inampasa awe wa kwanza kwa wale anaotoshana nao. Karibu katika

ulimwengu wa kulinganisha. Je, umewahi kuingia katika mtego wa kumnunulia mmoja wa watoto wako kitu katika ukumbusho wa siku yake ya kuzaliwa na hakuna kitu kwa wengine? Kwa kawaida mambo hayawi sawa na mtoto aliyenyanyaswa anapiga kelele kama kasuku " Si vizuri," akiwa na machozi akipiga nduru na saa zengine akiwa na hamaki. Na tena kuna mashindano ya "niangalie" Unamuangalia mmoja wa watoto wako katika mchezo wa kuteleza na unatabasamu akienda chini. Na nyuma yako unasikia sauti "niangalie" Naunapigwa na kamba ya "niangalie" kama bunduki. Kila "uniangalie" inaongezeka kwa sauti na nguvu. Kisha unaketi kula maakuli ya adhuhuri. Kisha unasikia huu wimbo mtamu mdogo, "Amepata nyingi kuniliko, si sawa, nahitaji nyingi zaidi." Hiki ndicho kiini cha maisha yanayo wezeshwa na Kiini cha Dura. Tukiendele kuzeeka tunajaribu kuwa bora kidogo, lakini kujilinganisha na kuhudumiwa kinafanya kitovu cha kuweko kwa wanadamu.

Mitaala mingi ya shule inaelewa hitaji hili la kulinganishana na hitaji la kutumikiwa. Kuwekwa pamoja na wenzako mbali na mazingira ya nyumbani kunapeana utamaduni halisi wa kutia ndani mafunzo ya kiini cha Dura. Miaka 12 itakuwa mbio za kulinganishana kwa kile ambacho mtu anafanya bora au mengine ili kumwezesha mtu kufaulu na kuwa na siku za usoni zinazong'aa na za furaha. Tamaduni nyingi zinapendelea wale walio werevu. Uerevu wa kulinganishwa ni jambo ambalo litakupeleka mbali. Je umewahi kujiuliza ni kwa nini watoto ambao wanao wezo kuhifadhi na kurudisha elimu wana tunukiwa zaidi ya wengine kuliko wale ambao wana talanta ya mikono yao? [41] Umewahi fikiria kuruhusiwa kujiunga na chuo kikuu kwa sababu unajua kutunza shamba vizuri au kujua kutengeneza mtambo wa gari? Kuna mahali pa watu walio na ujuzi huo, lakini bahati inapenda kuweka masomo juu ya fungu.

Mwaka baada ya mwaka watoto wanaleta cheti cha habari ya masosmo yao, na wanaendeleza mafikara juu yao kulingana na cheti hicho. Nimeshuhudia visa vingi ambavyo watu wana talanta kwa mikono yao lakini wanang'ang'ana na masomo. Kwa sababu hiyo unawapata wakijidunisha na matamshi kama

---

[41] Utamaduni wa magharibi umejengeka katika misingi ya utamaduni wa Wagiriki ambao ulikuwa wa kielimu badala ya vitendo. Sio ajali kwamba mnyama katika Ufunuo 13 anaelezewa akiongoza ulimwengu wote kimsingi alikuwa chui ambaye anawakilisha Ugiriki.

“Hiyo imenishinda,” au “Singeweza kufanya hivyo,” au wazi “Mimi ni mjinga kufanya hivyo.” Lakini usiogope njia zingine za kufaulu. Kila shule ina michezo ambayo inawaruhusu watoto kuendeleza kujilinganisha kwa njia ya michezo ya mbio ambayo kwa matumaini itawaletea siku moja uwezo na fahari kwa yale ambayo wanatamani. Tunajua kwamba spoti ni mchezo kweli? Hebu waambie mashabiki wa soka wakiingereza ambao wanaotembea kwa ubaya mitaani wakati wa kombe la dunia. Je, pia yule ambaye anaangalia timu yake ya kriketi ikishindwa kombe la dunia? Kwa sababu ya hiyo alikuwa na mshtuko wa moyo na akafa kabla ya mchezo kuisha. Na ni kwa nini wanaspoti wengi wanalipwa mamilioni ya madola kwa mwaka kwa kupiga teke kipande cha ngozi karibu ili kufanya vizuri katikati ya mangongo mawili? Spoti ni biashara kubwa kwa sababu inapeana njia moja rahisi ya kupata manufaa kwa mafanikio na kutumikiwa ambayo mtu angelipenda kupata. Ni mfumo bora wa kulisha kiini cha dura na kuwa imani kwamba tunaweza kupata thamani kwa uhusiano baadala ya mafanikio.

Kitu cha kufurahisha kuhusu spoti ni kwamba hata kama utafanya vizuri lakini ukiwa wapili hakuna ambaye atalikumbuka jina lako, kihemko kiwewe cha kupoteza kinaweza kuumiza. Ninakumbuka kumuona mwanasoka akibomoka chini akilia kama mtoto kwa sababu ya kushindwa kufunga penalti ambayo ilifanya timu yake kutopata kombe. Nakumbuka kummuona kocha wake akimsaidia kutoka uwanjani na kushangaa vile alihisi thamani yake wakati huo. Lakini hata hivyo ilikuwa ni mchezo tu. Ndio ilikuwa mchezo wa kufa na kupona kuhusu mapambano ya thamani na kukubalika. Ninaweza kuorodhesha miungu mingine ambayo tunafiria inayoweza kutuonyesha neema na kutupatia kufaulu na furaha ambayo  tuna hamu nazo. Kuna ulimwengu wa urembo wa kiwiliwili. Ulimwengu wa kukata koo ambapo mtu anaweza kushinda au kupoteza umaarufu kulingana na ukubwa wa mfupa wa shavu au kifua. Je, unawajua ni wasichana wangapi ambao wamelia hadi usiku wa usingizi kwa sababu hawakupata alama nzuri kimasomo?

Hivi karibuni ugonjwa wa anorexia ambao una wasukuma wanawake na kuwafanya wasile ili wawe na miili midogo. Je, uliwengu wa kutengeneza mali, hali ya kazi au kuwa na nyumba karibu na mji? Nimefanya kwa kampuni kazi za offisi kwa miaka michache na ni vizuri kuangalia vile watu wanavyolipwa, unaweza pia kujuaa cheo cha mtu kwa mfano wa ubora viti vya  ofisi yake na dirisha likiangalia chini mtaani. Mkubwa chumba kingine kama ofisi yake na

dirisha likianangalia chini mtaani. Yuko na kiti cha ngozi na sehemu ya kuwekelea mikono, yuko na meza ya mbao ya thamani kuu na kifaa cha hesabu (tarikilishi) kimekalia meza. Anaye mfuata pia ana ofisi yake lakini mtazamo wa dirisha lake si mzuri na kiti chake si kizuri na tarakilishi yake si ya haraka. Na mwengine anayemfuata ofisi yake imegawanywa na kiti chake hakina mkono. Na tena hana simu na dirisha lake hauwezi kuonea nje. Unaweza kucheka ukifikiria haya. Lakini ni biashara muhimu katika ulimwengu wa kampuni. Viti na meza za ofisi nzuri kutumika ukijilinganisha na wengine.

Orodha ya fursa ya kujilinganisha haishi katika dunia ya kiini cha Dura, lakini zikiorodheshwa zinaingia katika vikundi vifuatavyo:

1. Kiwango cha elimu
2. Uwezo wa kimchezo kama wa mbio
3. Uwezo wa muziki na utunzi
4. Cheo cha kazi/ kiwango cha mshahara
5. Kiwiliwili au maungo
6. Mali
7. uraia wako ni katika nchi gani.

Hii ndiyo miungu dunia inayoabudu na inamatumaini itawasaidia. Ni mabwana ambao hawataki mchezo na hupenda watu kuwanyenyekea kama ungependa mapendeleo nao. Hawa wangependa uotoe kafara familia na marafiki na kama umebahatika utakuwa na wakati wako wa kutukuzwa kabla haujafifia kuwa kitu bure. Sisi sote tunakuwa watumwa kwa hii miungu kwa uwezo wa kiini cha Dura, na ni kutoka kwa hii miungu Mungu wa mbinguni angependa kutuokoa.

## 13. Ngazi ya kwenda Mbinguni

Siku zilikuwa zinakuwa fupi na baridi; msimu wa baridi ulikuwa unawadia. Ilikuwa ni wakati wakutengeneza fungu la kuni ili kuziweka pahali pa moto katika baridi inayouma, ambayo ilikuwa karibu kushuka chini ya bonde dogo la furaha. Mtu wa nyumba alikuwa na shuguli nyingi za kuchanja kuni na alipoangalia pembeni aliona jozi ya viatu vidogo. Na alitazama juu akaona kijana mdogo wa kiume ambaye alikuwa akitazama kila alichokuwa akitende. Akasema "Baba yangu anaweza kuchanja kuni haraka kuliko hivyo." "Hivyo ni kweli?" akajibu huyo mtu akishangazwa na ujasiri wa mtoto huyo." kweli anaweza! Baba yangu anaweza kufanya kila kitu. Yeye ni mzuri kati ya walioko." "Vema unabahati kuwa na baba kama huyo."

Huo ndio ulikuwa uchache wa utoto wangu. Hizi zilikuwa siku ambazo mamangu na babangu hawangefanya makosa na walikuwa watu wazuri sana wakufikiriwa. Katika njia zingine ingekuwa ni vyema kubaki katika hali hiyo chache, lakini haingewezekana hivyo. Baada ya wakati mdogo shuleni nilianza kujizatiti katika hali ya kulinganisha. Ninakumbuka kwa furaha, uzoefu wangu mwingi wa kwanza shuleni. Kulikuwa na uwerevu na michezo na shughuli nyingi, kwa jumla ilikuwa ikifurahisha. Kuna wakati ambapo siku za usoni zilisongezwa mbele na ningelishuhudia uchungu mtamu wa kionjo cha ufalme wa kiini cha Dura.

Nilipokuwa miaka saba familia yangu ilihama kwenda mji mpya na nilikuwa nikihisi njia zangu kwa kundi jipya la watoto. Nilishika urafiki kwa haraka pia

nilipatana na watu wabaya. Nilikuwa na msingi imara kama mtoto, na watoto wakorofi wangelipata fursa ya kunisumbua kwa sababu nilikuwa na mwelekeo mzuri kuwaliko. “Mnene hivi,” “Albato mnene” na “Mtoa ute” ni baadhi ya majina ambayo ninayoweza kukumbuka. Ilikuwa uzoefu mbaya ambao wengi wetu tumekutana nao tukiwa watoto. Hii ilifanyika siku baada ya siku. Adui wa nafsi alikuwa akitumia watu hawa kuharibu garama yangu. Wakati wa kwenda shule siku moja niliamua kwamba nimepata ya kutosha. “Mama, sitoki nje ya gari. Siendi shuleni.” “Kweli wewe ni kijana wangu.” “Hapana, si kijana wako!” tukiingia ndani, niliona jozi za kuogofya wakitazama kama tai tayari kushambulia mawindo yake. Mama alifungua mlango akijaribu kunitoa. Nilipiga mateke, nikipinga na kupiga nduru nikishikilia kiti cha gari. Je, huu ulikuwa mfano wa mtoto mkorofi? Labda hivyo. Lakini wakati hali yangu ya utambulisho ilikuwa ikifanywa ubapa, nilikuwa naenda kuchukua suluhisho kali ili nijiokoe. Siwezi kukumbuka kilichotendeka lakini uchokozi huo ulikoma. Hapa ndipo kulikuwa na kionjo cha kile kilichosalia mbeleni.

Ukatili unao dhihirika kwa watoto ni matokeo ya kutoongozwa kutokana na mafunzo ya Shetani katika ufalme wake wa kulinganishana. Tunaweza kwa mara nyingine kusimasima tukipumbazwa na ubinafsi na kutokuwa na shukrani ambazo zinatokana kwa watoto. Je, tunaweza kuwa kiasili tuachane na tabia hizo? La, Kama vile tumejifunza hakuna mtu anayeacha ufalme huu bila msaada kutoka kwa mwana wa Daudi. Tukizeeka tunakuwa wajanja na waliosafika. Wakati nilipofika katika ya shule ya upili, niliratibiwa vizuri. Nilikuwa ninajifunza kumuabudu mungu wa elimu, mungu wa michezo na mungu wa maungo. Nilikuwa nataka kumuabudu mungu wa fedha lakini nilikuwa sina kazi! Kila kilicho nizingira kilikuwa kinaniambia ilikuwa inabidi nitie bidii ili niwe wa kwanza. Kujikaza na kufanikiwa. Nilijifunza kwamba washindi wanakubaliwa na waloshindwa ni bure.

Wakati mwingi lengo langu kutaka kufanya vizuri ilikuwa kwa sababu ya kutaka kuwa wa kwanza  si kwa sababu ya kufurahia kile nilichokuwa nikisoma. Ningeliona sinema katika runinga ambayo ingetilia mkazo Imani hii. Wanaofanya mchezo wa kuigiza wanaume wangefanya jambo la kufaulu ambalo lilitarajiwa kuyeyusha moyo wa mwanamke mdogo. Hii ilinifunza kwamba uhusiano ni jambo ambalo unalolifanikisha na mwanamke mdogo alikuwa kama tuzo si kama rafiki.

Si kwamba ungesema hivyo bali ilikuwa ikifanyika akilini. Huu ulikuwa wakati wa kuota ndoto. Kwa mara nyingi ningelala kitandani na kuota kushindia Australia mchezo wa kriketi au kufunga bao la mwisho au kuhatarisha maisha kwenda kumnusuru msichana mdogo ambaye maisha yake yamo hatarini. Ndoto hizi zilikuwa ni msingi wa vitu nilivyokuwa na thamini.

Kila mara nilipoota ndivyo nilijitahidi ili kufanikisha malengo hayo. Sehemu ngumu ni kwamba singeweza kufanikisha malengo hayo katika sehemu tambarare. Ilikuwa ni lazima nishinde watu. Nilikuwa nataka marafiki zangu pia nilikuwa nataka ndoto zangu kwanza. Ningelikuwa mwenye adabu kama ndoto zangu zilikuwa hazimo hatarini. Na kama nilihisi ndoto zangu zinatiwa changamoto, ilikuwa vita!

Nilifanya vizuri kufanikisha malengo yangu. Nilifanya vizuri kwa michezo na masomoni; kweli mbili kwa tatu si mbaya. Tena nikaanza kuingia sehemu nyingine. Nilipofika juu ilibidi nijaribu kubaki huko. Kulikuwa na mtazamo juu ya mabega yangu na pia kulinda cheo changu. Na pia kuna matarajio ya sifa. Wakati nilichonga sifa, je, iwapo nilifanya vibaya? Hiyo ingekuwa ya kuogofya, kwa hivyo niliamua nisiteleze. Hii iliendelea kwa kipindi kichache mpaka nikatambua kwamba ilikuwa ni vigumu kufanikisha malengo yangu yote.

Hii ilileta mlipuko wa hasira! Nafikiria nilihisi kusalitiwa. Niliwatumikia mabwana wangu vizuri na sasa walikuwa wakinizomea. Nilikazwa katika mtindo ambao haungeweza kamwe kunipa thamani yangu nzuri ya kudumu kwa hivyo nilikuwa na hamaki.

Watu wengi wanajikakamua kuelewa hasira na uharibifu unaoonyeshwa na vijana na kwa nini wanataka kujitia kitanzi au wanaelekea kunywa pombe na kutumia mihadarati. Na amini ni kwa sababu wametambua ya kwamba hawatafanikisha ndoto zao kwa kupitia njia walizofunzwa. Hawatawahi kuwa wakubwa machoni pa wengine kwa hivyo wanajiharibu.

Nakumbuka siku nilikuwa ninacheza mchezo wa vikapu. Mchezo ulikuwa mkali na kulikuwa na shinikizo. Yule ambaye niliyekuwa nikimlinda aliendambele na akainua mpira juu ambao niliufikia nikauchukua kwa njia safi kutoka mikononi mwake. Na kwa kutoamini kwangu nilisikia mwaamuzi

akipuliza kipenga na neno lilikuwa “kosa” Nilijua sikumgusa, na kwa ghafla hasira ikanipanda ndani yangu, hamaki ambayo mtindo mbaya ambao ulioniahidi ulimwengu haukunipa chochote.

Nikamvamia muamuzi nikisimama na yeye incha mbili kutoka usoni mwake na nikaongeza sauti kwa kiwango cha juu. Kitu kiliniwasha ndani yangu na singeliweza kujizuia. Nilitolewa kwa haraka uwanjani na nikapigwa marufuku kushiriki tena mashindanoni. Nilipotoka naamini Mungu aliniongelesha. Nilijiuliza, “Ni nini mbaya nawe wewe mtu? Karibu uipoteza huko nje; ulipoteza kujizuia!” Ilikuwa ni mara ya kwanza ambapo kwa ukweli ilibidi nijiangalie na nijiulize ninaelekea wapi. Mungu alikuwa akinivuta nitafute kitu chema. Nilianza kuhisi lazima kuwe na njia mwafaka.

Adui wa nafsi yangu pia aligundua hivyo na alijaribu kunisukuma kwa undani ili kudhibitisha thamani yangu. Kama mvutaji wa sigara ambaye anayehisi ni wakati wakuacha na amerudi na kuvuta sigara mara mbili zaidi. Nilianza kutoka wakati ndoto zangu zilififia na nikaanza kuwa mtu wa hasira. Wakati mwingine mamangu alikuja katika chumba changu akalalamika kuhusu hali hiyo ya kuhuzunisha. Wacha niseme kwamba ilikuwa chini ya kiasi vile vumba vya vijana wadogo vinavyostahili kuwa. Nilisikia kupandwa na hasira kwa sababu aliingia katika chumba changu kuja kuniamrisha. Niliamua niachilie mfululizo wa maneno yaliyochaguliwa chini ya pumzi yangu na kumwambia aniache peke yangu.

Nifuraha kuona njia nyingi ambazo Mungu anamfikia mtu. Wengi wa marafiki zangu wanawaita mama zao kwa jina la kudunisha. Babangu aliweza kunifunza adabu kwa wazazi wangu, na nikaapa sitaweza kumzungumzia mamangu kama vile marafiki zangu walivyokuwa wakifanya. Nilivyosema maneno hayo ni kama kipande cha mwisho cha adabu kilikuwa kikinitoka. Nilishtuka kwamba naweza kusema hivyo vitu na huzuni yangu ilienda kwa undani. Nilikuwa nafikia pahali ambapo sikujali tena, na hapo ni pahala pabaya kuweko. Nilikuwa na hisia hizi kwamba nilikuwa nimefikia njia panda. Njia hiyo panda ilikuwa ikinikaribisha na taya zake zikipiga miayo zikija na mvinyo, wanawake na muziki. Na hiyo sehemu nyingine ilikuwa njia nyembamba ya Bibilia. Je nitafuata dini ambayo wazazi wangu walinifunza au kuduwaa kwa njia panda kama commet inayong’aa? Sikuona haja ya kujifanya mkristo tena. Ilikuwa wazi kwangu kwamba sikuwa mkristo tena na kweli sijawahi kuwa, ijapokuwa

nililelewa katika mazingira ya Kikristo. Ilikuwa Kristo au Shetani. Shukrani, nilichagua kujaribu kutafuta Yesu wa kweli wa Bibilia.

Niliamua nitasoma kitabu ambacho kimekuwa nyumbani kwetu kwa miaka mingi. Kiliitwa Hatua kwa Kristo. Sasa jina la kitabu hicho lilifaa kikamilifu mahitaji yangu. Nilianza kusoma na njaa na hamu sana ya kumpata. Ilibidi ni pate ngazi ya kwenda mbinguni, kwa sababu singewezana na ufalme wa Shetani tena. Hapo awali katika kitabu mwandishi alifafanua kwamba Yesu alikuja kuondoa uongo ya kwamba kizazi cha binadamu kilimuaibisha Mungu, na vile kutuonyesha ya kwamba Mungu anatupenda. Nilikunywa maneno hayo kama dunia iliyopasuka na kupata mvua wakati wa kiangazi. Mwandishi alinialika nifikirie kuhusu Yesu katika shamba la Gethsemani na kumfuata hadi msalabani.

Wakati nilipokuwa nikitafakari visa hivi, kwa ghafla nilihisi kwamba nilikuwa nikisimama na kumwangalia. Umbo hilo msalabani lilionekana la kweli, na nilipata hisia hizi za nguvu kwamba alikuwa anaangikwa hapo kwa sababu Alinipenda mimi na aliona hamu yangu ya huzuni ya kutaka kutorokea ufalme wa Shetani. Wakati nilipo mtazama hapo, nilihisi shukurani kuu kwamba alikubali kuniokoa na nikahisi uzito wa dhambi, mashaka na fadhaa na uoga niliobeba miaka hiyo yote uliniondokea. Amani iliingia kwa moyo wangu kama vile sijawahi kuhisi mbeleni, kisha nikalia kiliio cha furaha. Mwana wa Daudi alipenya katikati ya giza langu na mwanga wa siku

## 14. Miungu Ifananayo, Majina Tofauti.

Chumba kilikuwa hai na shughuli, kicheko, muziki, na furaha ya ujanani. Mbele ya chumba kulikuwa na vifa viwili vya kutoa sauti vikitoa mdundo wa muziki katika nakala mpya ya bendi za rock. Nilipanga karamu ili kusherehekea pamoja na marafiki zangu – lakini nilijaribu. Nilienda nikakaa pembeni mwachumba ambapo moja wa vijana alijaribu kusimulia kisa katika sinema iliyotoka hivi karibuni. Nilikaa chini ili kujaribu kuvuta hewa hiyo, lakini kuna kitu ambacho hakikukuwa kizuri. Niliamka nikaenda nyuma kuungana na "Romeo" wadogo ambao walikuwa wakizungumzia ujasiri wao wakuwanasa wanawake wanaowapenda wa ndoto zao. La, sikufurahia hiyo pia. Kijana, ni nini mbaya na mimi? Muziki ulikuwa ukianza kuniingia katika mishipa ya fahamu zangu, niliangalia upande mwingine wa chumba ni kaona sehemu ya kisa katika kanda ya sinema iliyokuwa ikicheza, ambayo ilikuwa mbaya. Mawazo yakanijia kama gari la moshi libebalo mizigo, na chukia kitu hiki!

Akili yangu ikaanza kwenda kasi na visa hivyo. Hadi sasa haya ndiyo yaliyokuwa maelezo yangu ya raha na sasa singependa tena. Kuna kitu kilishika moyo wangu na kufanya vigumu kufurahia. Katika sehemu moja kutoka kuzimuni kulikuja, fikara zilizofichika kwamba maisha yangu ya anasa yaliisha na sitaweza kujifurahisha tena. Nilikimbia mbele ya nyumba hadi nyasi ya mbele ni katikisa ngumi hewani na kulia, "umeharibu maisha yangu!" Ilikuwa ni wiki ya salama baada ya 'uzoefu wangu wa barabara ya Damaski' na Yesu. Maisha yangu yaligeuzwa katika kichwa chake. Sijawahi kushuhudia amani maishani mwangu na Bibilia ilianza kuwa hai. Nilikuwa nikiinywa yote ndani na kushuhudia

uhuru ambao sijawahi kujua hapo awali. Wakati Yesu aliingia maishani mwangu, mabadiliko yalikuwa niyaghafla. Nilikuja kugundua ya kwamba lugha zangu zingine zilikuwa si nzuri. Kwamba matani yangu mengine yalikuwa machafu, na hali yangu ya maisha ilikuwa haiambatani na njia mpya ambayo nilikuwa nikielekea. Nilikuwa katika safari ya ufalme mpya, nilikuwa kama ninaenda nchi geni na ilikuwa ichukuwe mda wa kurekebisha.

Ilikuwa si mpaka, usiku wa karamu hiyo ndipo nilipogundua mabadiliko makali yalikuwa ya kiendelea. Kwa kuwa Yesu alikuwa amenasa moyo wangu kwa upendo, singeweza kumkataa alipoita. Usiku wa karamu hiyo wakati ninadhania nilikuwa nikitenda jema. Nilihisi alikuwa akiniita mbali na hayo maisha. Kwa sababu sikujua lingine lolote niliogopa kwamba nitabadilisha na haitakuwa tamu. Nirahisi kuogopa usiyoyajua hata kama unajua ni vizuri. Kwa shukrani nilichagua kumtegemea kristo ya kwamba atanishughulikia na ilikuwa ni vyema kumuamini kuliko hisia zangu.

Wakati nilipomkubali kristo kama mwokozi wangu nilielea kwa wiki kadhaa. Nilihisi kuwa karibu na Yeye na hiyo imebaki kuwa nami hadi leo. Yesu amenifungulia malango ya mbingu, na sasa atanisaidia kutoa mbegu za kiini cha Dura. Alinisaidia kung'oa kwa mizizi hiyo ya falsafa ya maisha ambayo iliyofanya kutimiliza jambo na kufanikisha kuwa katikati ya mtindo ni nao thamini. Ni safari ambayo kila mtoto wa Adamu lazima achukue. Njia ambayo itatufanya tufanikiwe ni kuweka macho yetu katika mwanga wa msalaba nakwa unyenyekevu kufuata nyayo za Mwokozi wetu katika mafunzo ya ufalme mpya.

Nilianza kuhudhuria mkutano wa maombi na marafiki zangu. Katika usiku huo wa kwanza tulipopiga magoti pamoja nilihisi Roho wa Mungu mzuri akituzingira, lakini kulikuwa na roho katika maisha yangu ya zamani aliyekuwa akinisumbua. Tulipoomba katika duara, wazo lilinigonga: “Siwezi kuomba kama hawa watu, wanajua kuzungumza.” mawazo yangu yalikuwa yamefungwa katika fikara hii na wakati huo mviringo wa maombi ulivyonikaribia moyo wangu ukaanza kudunda kwa upesi. Hivi karibuni itakuwa zamu yangu na kila mtu atakuwa akinisikiza. Lakini ngoja kidogo, huu ulikuwa mkutano kuhusu Yesu si mimi!

Hapa ndipo laana ya kiini cha mti wa Dura. Ijapokuwa nilikuwa nimempatia Yesu moyo wangu na nilikuwa ninatafuta kumfuata, mafunzo ya maisha ya kale bado yalikuwa yakinifuata na yalikuwa tayari kunivuta nyuma na kunifanya niwe katikati ya kila kitu, ilikufanya kutekeleza kwangu vitu iwe ni kiini cha maombi bali si uhusiano na Mungu wangu kwa maombi.

Wakati nilianza kusoma Bibilia, nilihisi kutoridhika ijapokuwa nililelewa katika mazingira ya Kikristo, nilifahamu misamiati ya Bibilia ambayo bado sikuwa nimehitimu kutoka utotoni. Nilipenda kusikia kile nilichofundishwa na katika fikira zangu kitu kilikuwa kikinifanya nishughulikie mambo madogo madogo zikaniambia,"Mbona wanaweza kuangalia hayo mafungu kwa urahisi, niliomba nisiwe wa mwisho ambaye kila mtu alikuwa akimsubiri. Itakuwa ni aibu gani! Miaka ya mafundisho niliyoyapata kwa kujilinganisha na wengine yalianza kuchipuka katika safari  yangu mpya ya ukristo. Ilikuwa ni rahisi Roho wa Yesu kunisadikisha kuhusu lugha yangu na maisha yangu, lakini ilinichukua mda kujua vile kamba za mizizi ya kiini cha Dura zilivyoingia.

Nilivyoendelea na safari yangu nilianza kuwa na upendo wa ndani kwa Bibilia. Ilikuwa ni njia nzuri kujifunza kuhusu shuja wangu ambaye aliyetoa maisha yake kwangu mimi. Nilipenda kujifunza kuhusu Yesu na ilikuwa ni baraka, lakini maisha yangu ya zamani yalikuwa yakini fuata tayari kuninasa tena. Nilikuja kugundua kwamba watu waliokaribu yangu walikuwa na ujuzi mdogo wa Bibilia kuniliko. Kujua kwangu kwa Bibilia kulinipa ujasiri na kwa haraka nilianza kuchukua makundi madogo halafu makubwa kwa kujifunza Bibilia. Tena ilikuwa baraka kwangu na kwa wale ambao walikuwa wamenizingira. Lakini nilianza pole pole na kwa imara kurudi nyuma kwa jukwaa la thamani la kujifanikisha kuliko uhusiano. Ilifanyika pole pole na bila kujua, lakini inafanyika. Kwa macho ya nyuma ninaona hayo kwa wengi wetu kwamba tuko na miungu inayofanana lakini majina tofauti. Ukiangalia jedwali ambalo liko hapa chini, utaona vile ni rahisi kuamini Bibilia na kuishi kama watu wa dunia. Si maanishi kuishi maisha mabaya, bali kupata thamani kwa kufanikisha kwa kile unacho tenda.

| Katika dunia | Katika kanisa |
|---|---|
| Elimu | Elimu ya Bibilia |
| Ewezo wa kimchezo | Uwezo wa kutoa hotuba |
| Talanta ya utunzi | Huduma ya uimbaji |

| | |
|---|---|
| Hali ya kazi | Ofisi za kanisa |
| Mali | Karama za kiroho |
| Umbo au kiwiliwili | Gwaridi la makanisa |
| Uzalendo | utunzi/kugeuka |

Kwa wengi, kutembea kwetu na Kristo kumetekwa nyara na nguvu za ndani za kiini cha Dura. Nikiangalia kanisa leo nina ona miungu ambayo tunataka tutorokee duniani imetupata kanisani. Wamejivika kwa mavazi ya nuru na wamewakumbatia kama marafiki wema. Matokeo yasiyoweza kuepukwa ni hasira, uchungu na kupigana makanisani. Ni rahisi kuonekana mnyenyekevu kanisani, lakini je, mbona yule mwengine anayekaa upande mwingine wakanisa ambaye hataki kuzungumza nawe kwa sababu ulisema kitu juu yao nyuma ya mgongo wao na ikawafikia? Je, mbona mcheza kinanda ambaye alienda kanisa lingine kwa sababu aliambiwa kucheza kwake ni kwa hali ya chini?

Je mbona askari wa mafundisho ya dini anayetembea huku na huko kanisani kuwatafuta wale ambao hawaambatani na maelezo yao ya kidesturi, ili wawafukuze kanisani? Je, mbona wale wa maendeleo ambao wanatafuta kuteka nyara kamati ya ibada ili wawalete kila mtu mtindo mpya wa kuabudu na ole wao wasiopenda mitindo hiyo? Orodha haina mwisho na adui mkuu wa nafsi anajua akiwaweka watu wacheze kulingana na sauti yake, bado wote ni wa ufalme wake. Sababu za nguvu ambazo za onyesha bado tumeathiriwa na hayo mafunzo ya ufalme wa Shetani ni mgawanyiko au utengano wa hali ya juu na kutokuwa na upendo wa kikristo kanisani na juhudi nyingi ni vile tunavyohusiana sisi kwa sisi katika kanisa.

Ni jambo la kushangaza kwamba udanganyifu huu wa kutoa miungu duniani na kuipeleka kanisani ni jambo la mtu binafsi na limefanyika kanisani kama kundi kijumla. Katika karne ya nne wakati mfalme Konstatino alipokubali ukristo, kulikuwa na badiliko la kijografia lililotendeka katika kanisa la Kikristo. Na wakati mmoja ambao unashangaza ni kwamba sanamu nyingi za miungu ya kipagani ambayo ilikuwa Pantheoni ililetwa katika kanisa la Kikristo na majina yalibadilishwa na ya watu katika Bibilia kama Musa, Daudi, na Petero. Miungu ile ile lakini majina tofauti!

Haijalishi vile utaivalisha nguo, bado ni ya kipagani, ni nini tunaweza kusema leo? Ni jambo moja kulishambulia kanisa kwa kuacha mafundisho ya Bibilia ya mitume na pia ni jambo linguine kuona mafundisho hayo yakifanya kazi katika maisha yetu. Ni

vizuri kuanza na kibanzi katika macho yetu kabla ya kuenda kwa boriti lililo machoni pa ndugu zetu.

Ni jambo la kupendeza kujifunza safari za wafuasi wenye bidii wa Kristo - wanafunzi wake. Jambo la mamlaka na cheo lilikuwa kila mara likiinua kichwa chake juu. Hebu tutazame sehemu chache katika mandiko:

> Wakati huo, wanafunzi wakamjia Yesu na kumwuliza "Je, nani aliye mkuu kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni?" Mathayo 18:1

Hapa pana sababu moja na ni sababu moja kwa nini wanafunzi walikuwa wakiuliza swali hilo – faida ya ubinafsi. Wanafunzi waliamini kuwa Yesu ni Masihi, Kristo. Walikuwa wamefurahi na wameshika sana imani yao juu yake; wengine walikuwa wako tayari kufa kwa ajili yake, lakini kama vile nilivyokuwa nikijitayarisha kuomba na mawazo yangu yalitoka kwa uhusiano wangu hadi kutimiza kitendo mimi mwenyewe katika maombi, wanafunzi walitoka kwa uhusiano na Masihi hadi kwa vyeo vyao katika ufalme wake mpya.

> Kisha Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, wakaja mbele alikokuwa na kumwambia, "Mwalimu, tunataka utufanyie lo lote tutakalokuomba." (36) Naye akawaambia, "Je, mwataka niwafanyie jambo gani?" (37) Wakamwambia, "Tupe kukaa mmoja upande Wako wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto katika utukufu Wako. Marko 10: 35-37

Mungu wa vyeo na daraja aliipita mafunzo ya ufalme mpya ambao Yakobo na Yohana walikuwa wakijifunza, na walimuuliza Yesu kama wangelikaa katika mkono wake wakushoto na wa kulia katika ufalme wake. Ni shukrani, Yesu hakuchoshwa na kuanguka kwao kila mara ili kuachilia mafundisho ya zamani. Alielewa kwamba kuona kwa undani vile mafundisho ya ufalme wa Shetani yalivyokita mizizi kwa undani. Na shida inayotukumba wakati tukiachilia mafunzo ya zamani kuchukua kipao mbele, yafuatayo yanatendeka:

> Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia hayo wakaanza kuwakasirikia Yakobo na Yohana. Marko 10:41

Wakati mafunzo ya ufalme wa kale unapotutawala sisi, mafarakano kila siku yatakuwa matokeo. Ndio maana Yakobo na Yohana waliwafanya wanafunzi kukasirika. Kwa nini? kwa sababu walikuwa wakituma ujumbe, "Sisi ni bora

kuwaliko" Hawakumaanisha kufanya hivyo lakini hayo ndiyo matokeo ya kila siku. Yesu alichukua fursa hii kuwaelezea na kupanua mawazo yao vile ufalme wa mbinguni ukotofauti na ule ambao wamelelewa ndani yake. Wangelijifunza kufikiria kwa njia tofauti.

> Yesu akawaita wanafunzi Wake pamoja akawaambia, "Mnafahamu kuwa watawala wa watu Mataifa huwatawala watu kwa nguvu, nao wenye vyeo huwaonyesha mamlaka yao. (43) Lakini sivyo kwenu. Badala yake ye yete anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi wenu (44) na ye yote anayetaka kuwa wa kwanza, hana budi kuwa mtumwa wa wote. (45) Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai Wake kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi. Marko 10:42-45

Wacha maneno haya yasikike milele katika masikio yetu kama ungelitaka kuwa mkubwa katika ufalme wa Mungu basi lazima ujifunze kufurahi kuwatumikia wengine baadala ya kuvuta watu kwa ila kisha kuwatawala. Yesu anatuambia kwamba wapagani (wayunani) hutawala watu kwa nguvu wakionyesha ni nani mtawala. Geni kiasi, hii roho ndio inatawala kanisa na wafuasi ambao wanapenda kulazimisha uongozi na mamlaka yao kwa kanisa. Miaka elfu mbili imepita na wengi wetu bado hawaelewi mafunzo ya msingi.

Mbona adui wa nafsi anapata kuwa rahisi kutuvuta nyuma katika njia zetu za zamani za kufikiria? Kama nilivyo sema hapo awali ni kutokuwa na usalama wa ndani ndiyo unaomfanya Shetani kupata kuwa ni rahisi kutujaribu ili tujidhibitishe na kujionyesha. Hadi tuelewe vile tunavyopata thamani yetu tutapata ni vigumu kushinda kujaribu kugeuza mawe kuwa mikate kuonyesha tuko bora.

Kuna kitu ambacho ninakipata ni cha kutisha kuhusu mafunzo ya kiini cha Dura kwamba inatushika tunashikamana. Yesu alikuwa mwalimu mzuri ambaye ulimwengu huu haujawahi ona. Aliishi miaka mitatu na wanafunzi wake akiwafundisha kuhusu ufalme wa mbingu, na tunapata baada ya haya yote usiku ule wa kusulubishwa kwake wanafunzi bado walikuwa wanatawaliwa na mafunzo ya maisha ya kale.

> Vivyo hivyo baada ya kula, akachukua kile kikombe akasema, “Kikombe hiki ni agano jipya katika damu Yangu, imwagikayo kwa ajili yenu. (21) Lakini mkono wake huyo atakaenisaliti uko hapa mezani pamoja nami. (22) Mwana wa Adamu anakwenda Zake kama ilivyokusudiwa, lakini ole wake mtu huyo atakayenisaliti.” (23) Wakaanza kuulizana wao kwa wao, ni nani miongoni mwetu anayeweza kufanya jambo hilo? Mabishano Kuhusu Ukuu 24 Pia yakazuka mabishano katikati ya wanafunzi kwamba ni nani anayeonekana kuwa mkuu wa wote miongoni mwao. Luka 22:20-24

Usiku huo upendo mkuu ulivyokuwa ukidhihirishwa ulimwengu haujawahi ona, wale waliokuwa karibu na Yesu waliojuaa mengi zaidi ya ufalme huu kuliko yoyote walikuwa wakibishana kuhusu ni nani mkubwa kuliko wote. Huzuni ambayo Yesu aliihisi lazima ilikuwa kubwa! Je, kunauwezekano sisi ambao ni wafuasi wa Yesu tunafanya makosa hayo tena kama vile wanafunzi wake – wafuasi waliokuwa na moyo wa bidii, tunasukumana kwa nguvu sisi wenyewe ni nani mkuu?

Kuna kitu kibaya zaidi kuliko kutawaliwa na kiini cha Dura, duniani nikutawaliwa na mafunzo hayo kanisani. Mungu atusaidie ili tuwekwe huru kutokana na mafundisho ya kibinafsi ili tushuhudie furaha kamili ya ufalme wake.

## 15. Unasoma Jinsi Gani?

Leo inaenda kuwa siku muhimu. Umejawa na matarajio na furaha kwa ajili ya tarajio ambalo liko mbele. Kiongozi wa kampuni kubwa amefurahishwa na uvumbuzi uliotengeneza na anafikiria kuvitengeneza kwa ajili ya soko la nchi za kigeni duniani. Umeamua mkutane kwa chakula cha adhuhuri katika hoteli nzuri ndogo. Kwa sababu hamjawahi kukutana, una uoga kidogo na unajaribu kuangalia kila sehemu kujaribu kumtambua huyu mtu ni nani ambaye anaenda kubadilisha ndoto zako kuwa za kweli. Mwishowe amefika na unamsalimia ukitingisha mkono wake kwa nguvu na nyote munaenda kwa hoteli hiyo na mnapata nafasi yenu. Ili kujuwana mwenzako anakuuliza kuhusu familia yako, na pahali ambapo unaishi na vile watoto wako wanavyofanya shuleni. Kila kitu kinaendelea vizuri ijapokuwa mtu nyuma yako ambaye anakunywa mchuzi wake kwa kishindo. Mara ya kwanza ulijifanya hausiki, lakini mara kidogo anaanza kukasirishwa. "Watu wengine wanastahili kujifunza tabia nzuri" unajifikiria, na unapuuza ili mazungumzo yenu ya sifadhaishwe. Mazungumzo yako na mfanyi biashara mtarajiwa yanaendelea vizuri, na uko katika kumuelezea uzuri zaidi wa uvumbuzi wako halafu kwa ghafla yule mtu nyuma yako anapiga mbweu ambalo karibu litetemeshe vyombo katika meza yenu. Macho yote yemeelekezwa kwa mtu machachari huyu ambaye anaaonekana hana muenendo mzuri kabisa. Chumba kimejawa na sauti za kuchekelea upumbavu na wengine kicheko ambacho mdomo umefungwa ili kupunguza sauti iliyochanganyika na machukizo na kuchafua moyo. Mwishowe mwenye hoteli anakuja na

kumwambia mtu huyo atokee, akisema watu kama yeye hawajaruhusiwa katika hoteli.

Jambo la kushangaza huyu mtu alikuwa amekaa katika hoteli ambayo ilikuwa inaonyesha utamaduni wa kichini, hakuna mtu angelifunga macho. Kwa kweli wenyeji pamoja na wageni wote wangeliona aibu kama haungelifanya hivyo. Pia katika tamaduni za kichina ikiwa unataka kumsalimia mtu kwa kumtikisa mikono na hamjawahi kukutana na yeye hapo awali au kuzungumza kuhusu familia katika maakuli ya jioni itaonekana kwamba ni fidhuli.[42]

Ni jambo la kushangaza kwamba tabia zingine zinaweza kuchukuliwa kwa njia nyingine tofauti kulingana na utamaduni au mtazamo wako wa kidunia pahali utokako. Hii haiko tofauti tukiangalia utamaduni wa ufalme wa Mungu dhidi ya ufalme wa Shetani. Imani ya Kikristo ina msingi mmoja , Yesu Kristo, na walakini tukichunguza vikundi kwa wingi na kupita kiasi ambao wanaolichukuwa jina la Yesu tunashangazwa kupata ya kwamba kuna ukinzani ambao uko katika msingi mmoja. Safari ya ufalme wa Mungu unahusu kuhamisha utamaduni na kuhamisha mtazamo wa kidunia. Katika sura ambayo imepita tulinzungumzia ugumu ambao tunaokumbana nao kwa kujifunza kufikiria njia za mbinguni.

Ugumu mkubwa wa safari ya Kikristo inazunguka mzunguko vile tunavyolisogea karibu neno la Mungu pahali tumefunzwa fanikisha na cheo, lakini tukisonga katika ufalme wa Mungu ni muhimu sana tukiacha mawazo yetu na kuacha Roho wa Mungu atufunze jinsi tunavyo stahili kusoma neno la Mungu. Huzuni ni kwamba hivi haijakuwa hivyo, na wingi wa ukinzani, mafundisho ya imani yasiyopatana na yale yaliyotangazwa na kanisa na ugomvi yaliyopatikana katika imani ya Kikristo na kwa historia yanatoka moja kwa moja kwenye Bibilia na kiunzi kikiwa ni kiini cha Dura baadala ya kiunzi cha mbinguni ambacho kinaangazia uhusiano wa kweli na wa karibu.

Yesu anatoa hoja hii akizungumza na wakili katika kitabu cha Luka. Wakili anamuuliza, “Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?” Yesu anajibu, “Imeandikwa nini katika torati?” Ili kuenda kwa undani zaidi anauliza, “Unaisoma je?” [43]

---

[42] http://www.chinawestexchange.com/Chinese/Culture/customs.htm

43 Luka 10:25,26

Yesu haulizi unasoma nini; anauliza unasomaje; au unatafsiri vipi kile unachosoma? Hili ndilo swala nyeti kwa wale ambao wanataka kuchukua safari kutoka kwa kiini cha Dura duniani hadi uhusiano wa kimbingu – Unasoma je?

Swali kuhusu uzima wa milele ndilo swali muhumu kuliko maswala yote katika safari ya Kikristo. Sehemu unayoshikilia na watu ambao unaochangamana nao inaonyesha dhahiri shairi thamani yako duniani. Ukilinganisha, kila mtu katika ufalme wa Mungu ni mwana wa Mungu na anastahili heshima na adabu. Tukifuatilia mazungumzo wakili anataka kutafsiri maandiko kutimia ya kale baadala ya kisasa.

Anampatia Yesu jibu sahihi, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote, tena mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe."[44]

Yesu anaema ukitafsiri "Fanya hivyo kwa hakika na utaishi," Wakili alipogundua hiyo inamaanisha nini alitaka kugeuza maana kwa kuuliza "Jirani yangu ni nani?" Maana ya maandiko haya ni rahisi lakini moyo wa mwanadamu umeathiriwa na kiini cha Dura na inajifanya ni vigumu kuelewa, kwa sababu haitaki kuachilia la kale na kukumbatia kamili jipya. Hapa kuna sababu ya ukristo kwa wingi ambao umekufa, wanaamini ufalme wa Kristo lakini wanaishi kulingana na ufalme wa Shetani na matokeo ni machafuko, ubatilisho na uovu.

Imani ya Kikristo yote imechafuka kwa jambo la wokovu kwa sababu Bibilia inafunza wakristo waliotiwa nguvu kwa neema wataishi kulingana na amri kumi za Mungu. Lakini wengi wetu twakaribia amri kumi kwa kiini cha Dura; tunataka tuzitimize ili tupate wokovu, baadala ya kuona amri kumi kama maelezo ya ahadi za uhusiano ambao utafanyika kati ya Mungu na wana Wake.

Kwa kinyume, na kinachopendelewa, tunaona umati wote ambao wanaona ni vigumu kutekeleza wajibu wa sheria, baadala ya kuingia kwa imani katika uhusiano, wanatangaza kutunza sheria ni vigumu kwa hivyo hawafurahi uhuru wa ushindi unaopatikana kwa Yesu. Kama ungependa kutekeleza au haupendi kutekeleza, jambo ni kutekeleza badala ya uhusiano. Hakuna kati ya haya makundi yatakayoingia katika ufalme wa mbinguni hadi wazikumbatie amri

44 Luka 10:27

kumi kati kulingana na imani ambayo msingi wake ni uhusiano na Yule aliyetufia.

Kwa yale makundi ambayo yanachukua msimamo wa kutotekeleza na ugumu wa ushindi katika safari ya Kikristo, hivi karibuni inafuata ya kwamba mungu wao hawezi kutimiza. Ukichanganya mtindo huu na kuwa na hamu ya kutambulika na sila kushangaza kupata wasomi, walimu na waumini ambao wanakataa uwezo wa Mungu kuumba dunia hii kwa siku sita. Kama vile wakili anapeana jibu kwamba anastahili kumpenda jirani yake kisha anauliza, "Jirani yangu ni nani?" Ndivyo wasomi leo wanasema, "Ndiyo tunaamini uumbaji wa siku sita, lakini ni siku za aina gani? Uovu kwa kawaida unatafuta njia ya kugeuza maandiko ili yaende kulingana nao; kumuamini Kristo lakini kuishi kulingana na ulimwengu.

Wakati ambapo mtu amepoteza imani yake kwa Mungu ambaye anaweza kuumba moyo mpya na amejifunza kuuliza maswali ya ujanja kuhusu kauli wazi za maandiko, basi ni rahisi kukumbatia na kukubali ushoga kama kanuni ya Kikristo na pia kukataa majukumu ya kiume na kike nyumbani na kanisani ambayo Bibilia kwa wazi inatutandazia mbele yetu. Mafunzo haya ni geni kwa ufalme wa mbinguni. Thamani kila siku ni ya uhusiano na si ya cheo.

Tunaweza kuorodhesha fundisho baada ya lingine katika Bibilia ambao limegeuzwa na kubadilishwa ili kufurahisha mafundisho ya mamlaka, cheo na utekelezaji, lakini nafikiria hoja hii imefanywa kuwa wazi kama tunadai kuwa wafuasi wa Yesu basi tutatafuta kutafsiri maandiko kulingana na mafundisho ya ufalme wake baadala ya ufalme ambao sote tumetoka kwao.

# 16. Sio Mtumishi Tena

Ilikuwa ni moja wapo ya nyakati muhimu. Mtoto wangu wa kiume wa miaka sita alikuwa akisafiri nami katika gari. Tulikuwa na mazungumzo ya ndani ya maana, vema, ndani sana kulingana na uzoefu wa mwanangu wa thamani ningemruhusu. Niliona magurudumu ya geuka kwa utaratibu kichwani mwake. Nilihisi alikuwa mwisho wa kitu cha muhimu, na kisa kikatoka. "Unajua Baba, nafikiria vitu vitaendelea vizuri kama ungelikuwa mkubwa wakati mwengine na mimi pia niwe mkubwa wakati mwengine." "Vema mwana, hilo kweli ni shauri la kufurahisha," Nilisema nikisafisha koo langu. Kulikuwa na wakati wa kimya nikijaribu kufikiria sababu nzuri kwa nini ushauri wake ulikuwa na hitilafu lakini singeweza kupata na kama singepata sisi sote tungeelekea tabuni. "Vema, hivo sivyo vile Bibilia inavyo tuambia tufanye, mwana," "Na kwa nini uniambie kitu cha kufanya kila wakati?" "Vema mwana, Yesu ameniuliza nikufunze jinsi ya kuwa kijana aliye na nguvu, na kwa kuwa Yeye ni mkubwa wangu na fikiria ni vema kufanya vile anavyoniambia kufanya.

Uzazi kweli ni masomo ya kizingo. "Mwana, tafadhali kaa chini unapokula." "Aa, si vizuri!" "Mrembo, tafadhali okota vitu vyako vya kucheza na uviwe." "Aa mama, nataka kwenda nje kucheza." "Mwana, ni wakati wa kwenda kitandani." lia, piga nduru, makelele, "Lakini wewe hauenda kitandani sasa. Mbona mimi niende? Haya yote ni amri na masharti! Unaweza kufikiria kwamba wazazi ni wakatili wakati wote. Kwa nini watoto hawaelewi unataka wakae kimya na wale polepole mezani ili wazifadhaishe kubadilishwa chakula tumboni ili kifae? Au unataka kuwafunza kuwa wasafi na wakupendeza ili wajifunze kuwa na utaratibu na wafanye vizuri wakati wanapokuwa wakubwa? Na mbona watoto wafurahi kwamba unawakinga kuwa wagonjwa kwa kuwafanya wapate usingizi mwingi? Kwa nini? Kwa sababu hawajui mashimo na hatari za maisha.

Mtume Paulo anachukua mfano huu ili kuonyesha safari katika maisha ya Kikristo.

> Lile nisemalo ni kwamba wakati wote mrithi akiwa bado ni mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ndiye mmiliki wa mali yote. Wagalatia 4:1

Paulo anaelezea uhusiano wa mwana na mzazi wake kama hakuna tofauti na ule wa mtumishi na bwana wake. Baba lazima amfunze mwana wake kanuni za ufalme wa mbinguni, lakini mwana na asili yake ya kiini cha Dura haelewi sababu ya kumfundisha. Wingi wa mafunzo ambayo babake atamfundisha ni kinyume na asili yake na ni kazi ya bidii na hakuna tofauti na kuwa mtumishi. Mtoto wakiume anaweza kushangaa kwa urahisi. "Kwa nini babangu ananizuia kufanya vitu vingi ambavyo nataka? Ni najihisi mtumwa. "Mwana, fanya hili, mwana, usifanye hivyo, haionekani vizuri!"

Hali hii inafafanua kamili vile Mungu anavyofanya na sisi akitafuta kututayarisha katika ufalme wake. Wengi wanaona matakwa ya Mungu kuwa magumu na ya kufinyilia na kila mara wanauliza, "Kwa nini Mungu aliruhusu hili kunifanyikia au kwa nini maisha ya Kikristo yanaoneka kuzuia watu kufanya mambo wanayoyataka? Kuna wengi pia ambao wanaojumuika na makanisa ambao wameridhika kubaki wana kama vile watumishi, wanaotekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo na wakitumaini kwamba watatunukiwa kwa kulingana na juhudi zao, watu hao wamo hatarini yakumezwa kwa hisia za yule ndugu mkubwa katika hadithi ya mwana mpotevu.

Paulo anatuelezea vile tunaweza kuepushwa na dukuduku za maisha na anauliza vile Mungu anafanya na sisi. Wakati tunapoelewa kwamba Mungu ni Baba yetu na anatutayarisha kuingia katika ufalme wake na anatupenda sana basi uhusiano wetu naye unaanza kuwa wa busara. Amri na masharti hayaonekani kama vikwazo na vizuizi vya kutuzuia kuwa na raha; bali vinakuwa milango ya uhuru ambayo yanafunua uangalifu wa huruma ya Mungu kwetu sisi na anavyotamani sana kutupokea sisi kama urithi kamili kama wana wa Mungu. Paulo anafafanua hivi:

> Vivyo hivyo na sisi, tulipokuwa bado watoto wadogo, tulikuwa utumwani chini ya taratibu za kawaida za ulimwengu. (4) Lakini ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe, ambaye alizaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, (5) kusudi awakomboe wale waliokuwa chini ya sheria, ili tupate kupokea zile haki kamili za kufanywa watoto wa Mungu. (6) Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, anayelia, "Abba! Yaani, Baba." (7) Kwa

> hiyo, wewe si mtumwa tena, bali ni mtoto, nawe ikiwa ni mtoto, basi wewe pia ni mrithi, mrithi wa Mungu.(8) Zamani, mlipokuwa hamumjui Mungu,mlikuwa mkitumikia viumbe ambavyo kwa asili si Mungu. Wagalatia 4:3-8

Haya ni baadhi ya maneno mazuri katika maandiko. Kama vile tunavyotambua kafara ya Yesu ili kutuhifadhi sisi kufanywa wana wa Mungu, tumetolewa kwa utumwa wa ufalme wa Shetani. Tumeachiliwa kutoka kwa ukatili wa kiini cha Dura na tunasimama tukiwa na nguvu na bora kama wana na binti za Mungu, tukijua kwa ajili ya Yesu tutakuwa wana Wake wapendwa. Je Roho wa Mungu amelia ndani ya moyo wako, "Abba Baba;" "Baba, Baba?" Je unahisi salama katika upendo wake kwamba unaweza kukimbia mikononi mwake ukijua kwamba haujakaribishwa tu bali unatamaniwa sana na Yeye?

Je, umerudi katika hali yako ya utoto ya kumtukuza Baba ambayo inang'aa akiwa karibu. Mpaka uwe na uzoefu wa uhuru huu, utakuwa kila siku mtumwa ambaye anayeishi na mashaka  kwamba kesho utapewa adhabu kali.

Kama wana wa Mungu, urithi wetu ni wa hakika. Tunaweza kumkaribia kwa ujasiri na kufanya maombi yetu kwake; tunaweza kwa hakika kumuamini Yeye kwamba anajua kile kilicho kizuri kwetu. Kila kitu ambacho kinatufanyikia maishani kinatusaidia kukua katika ufahamu wa ndani kuhusu thamani yetu katika ufalme wa Mungu na kuvunja utumwa wa kiini cha Dura.

Unaweza kukumbuka katika sura ya 6 tulijadili kazi kubwa ambayo Mungu anakabiliwa nayo akitafuta kuleta kizazi cha wanadamu katika upendo wake wa kutukumbatia. Hivi ndivyo vidokezi tena:

1. Njia ya kuipa jamii ya mwanadamu hekima ya kutambua hali yao ya kukata tamaa, pamoja na mbinu kwao ya kuathiriwa na mwelekeo sawa bila kukiuka uhuru wao wa uchaguzi.

2. Njia ya kuwaonyesha kuwa walikuwa na mtazamo mbaya wa tabia na ufalme wa Mungu na kwa namna fulani kuwaonyesha kuwa ukweli anawapenda.

3. Njia ya kuondoa hisia yao ya hatia na ukosefu wa usalama na kuwarejeshea utambulisho wao wa kweli na thamani kama wana wa Mungu.

4. Njia ya kurudisha hisia yao ya kusudi, sababu yao ya kuwepo au hatima.

5. Hayo yote ya hapo juu yanahitaji muda. Adamu na Hawa walikuwa wamepoteza maisha yao wenyewe, basi walihitaji mfumo wa kuegemezea uzima wao ili kuwapa muda wa kuchagua na kuamua.

6. Tunapofanya haya yote, Mungu lazima adumishe hisia ya haki, hawezi puuza uasi wao na kusema ni sawa. Ingawa Mungu katika huruma zake haruhusu matokeo kamilifu ya uchaguzi wao kuwaangukia, Adamu na Hawa lazima wafahamu matokeo ya uchaguzi wao ili waanze kuthamini kosa la yale walilotenda.

Kazi ya Yesu katika huduma yake, kifo na kufufuka imepeana suluhu kwa changamoto hizi zote. Ni nani anawezakuelewa nguvu za msalaba wa Kristo? Iko ndani sana kuliko kutoa makosa matendo yetu; iko ndani ndani kabisa.

Je unaweza kupiga magoti na kutazama msalaba hivi sasa na kuona wokovu wako kutoka kwa kiini cha Dura? Je unaweza kuisikia sauti kutoka mbinguni ikisema wewe ni mwana wangu mpendwa ambaye ninafurahishwa naye. Je unaweza kumpatia hatia, chuki, kiburi na uchungu Yeye? Hebu kubali furaha yake kamili kukumwagikia kama gharika hivi sasa. Unaweza kama haujawahi. Siri ya kuepuka kiini cha Dura ni kutokubali kuwa mtumishi, lakini kuwa mwana au binti.

## 17. Anguko la Babeli

Iligonga kama umeme. Mashine ya Ujerumani ya vita ilikimbia katika viwanja vya Uholanzi na Ufaransa, na katika usiku moja nchi hizi zilikuwa zimeshikwa kama ngumi ya chuma katika ulinzi wa mashini ya Nazi. Kuishi katika nchi ambayo ina watu ni uzoefu wa kukauka. Babangu aliishi wakati huu katika mji wa Assen uliokuwa kaskazini mwa Uholanzi.

Watu walifinyiliwa katika utumishi wa mashini ya Ujerumani. Majasusi walikuwa tayari kuwasema kwa askari polisi wa siri waliokuwa wanaogopwa, na wakati wowote wangepata milango yao ikibishwa na kuona mpendwa wao akivutwa, pasipo kuonekana tena. Uongozi wa Kinazi ulionyesha alama za kiini cha Dura, roho ya uzuifu ambayo ilikuwa tayari kuwamaliza wapinzani wote, kuongoza kwa hofu na kuonyesha mamlaka yake kwa kuridhika kishetani.

Kuvuliwa na kumaliziwa mali, kuchoshwa na minyororo ya kunyanyaswa, Uholanzi haikuwa imejianda kwa msimu wa baridi wa mwaka 1944. Hawangetoka manyumbani mwao kwa kuogopa ya kwamba wakirudi hatakuweko tena, ikiwa wamevuliwa kuni. Wengi mjini walifarika kutokana na nja na baridi. Ni kwa mda gani jinamizi hili litadumu?

Mwishowe wajerumani wakarudi nyuma, wakilipua madaraja, kuharibu silaha za vita na kuacha uharibifu mwingi vile inavyowezekana. Babangu anakumba kila mtu akicheza mtaani na majeshi ya nchi rafiki yakigawa vyakula. Ilikuwa ni vigumu kuamini kwamba ilikuwa imekwisha, mwishowe uhuru!

Roho ya Kaini bado i hai, na kitabu cha Ufunuo kinafunua kwamba kabla ya Kristo kurudi hali hii ya uzoefu, kutokuwa na usalama, wivu, na kutokuwa na thamani ya roho hii itadhihirisha nguvu zake mara ya mwisho kabla kufariki. Yohana anatufafanulia mnyama mwenye vichwa saba na pembe kumi akitoka baharini.

> Nami nikamwona mnyama akitoka ndani ya bahari. Mnyama huyo alikuwa na pembe kumi na vichwa saba, akiwa na taji kumi kwenye hizo pembe zake na juu ya kila kichwa kulikuwa na jina la kukufuru. Ufunuo 13:1

Mnyama amepewa uwezo na mamlaka juu ya mataifa yote ya dunia na dunia yote ikamuabudu na kujisajilisha kwa uwezo wa mnyama.[45] Uwezo wake wakinyama unasimama dhidi ya uhusiano wetu na Mungu aliyeumba mbingu na nchi. Anataka kupata kuabudiwa.

Sababu ambayo mnyama huyu anaweza kwa urahisi aminisha ulimwengu wote kumfuata ni kwa sababu anaenda kwa kiini cha Dura kama chombo cha kutengenezea nguvu za umeme. Ananena lugha tunayoizungumza kiasili. Anatutia nguvu kutafuta utambulisho wetu kwa kufanikisha na kutekeleza, na anatutia moyo tukutane na Mungu katika masharti yetu, kwa kuleta kafara zisizokuwa na damu na kumtarajia Mungu akubali na kuitikia ibada yetu.

Dunia nzima tayari iko chini ya nguvu hii lakini haitambui. Dunia ikakataa mambo ya busara ya uhuru na ikirudia uzuifu wa ulimwengu kwa kupitia hofu na nguvu za kimabavu, itakuwa ni ishara ya nje ya kile kilicho ndani ya moyo wa kila mmoja wetu. Mungu hakai kwa hali ya uzembe na bila kufanya lolote. Anatuma ujumbe wa mwisho wa hatari sana ili kuonya ulimweng usijiachilie kwa nguvu za huyu mnyama. Inakuja kwa njia ya ujumbe wa malaika watatu. Ujumbe wa kwanza unatuambia tuwewaangalifu na kutukumbusha kwamba tunastahili kumwabudu Mungu aliyeziumba mbingu na nchi. Inatuelekeza kwa kafara ya Yesu na inatukumbusha ya kwamba kafara ya Kaini haiwezi kukubaliwa na Mungu. Hatuwezi kujilipa upendeleo kwa Mungu, wokovu wetu tulinunuliwa kwa damu ya mwana kondoo.[46]

---

[45] Revelation 13:2,7

[46] Revelation 14:6,7

Mungu tena anatukumbusha ukweli wa maana sana. Anauweka kwa lugha hii:

> Malaika wa pili akafuata akisema, "Ameanguka! Ameanguka Babeli aliye mkuu, yeye aliyeyafanya mataifa yote kulewa kwa mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake.'' Ufunuo 14:8

Kwa nini Mungu anatumia neno Babeli? Tukitazama Bibilia tunapata ya kwamba ni Nimrodi aliyejenga mji wa Babeli, Ereku, Akadi,Kalne katika nchi ya Shinaru."[47] Nimrodi ndiye mtu  wa kwanza kuandikwa kwamba aliaanza ufalme wake mwenyewe. Pia ni vizuri kufahamu ya kwamba Nimrodi wakati fulani alimuoa mama yake – ilikuwa familia ambayo ilisambaratika! Pia kuna ushauri ya kwamba Nimrodi alimuua baba yake ili amuoe mama yake. Haijalishi, nyumba ya Nimrodi haikuwa katika msingi wa mafunzo bora ya ufalme wa Mungu, ambapo uhusiano wa kijamii ni mtakatifu.

Maisha ya Nimrodi nyumbani kwake yalikosa usalama hadi akaanza kujulikana na kile alichotenda baadala ya yule aliyekuwa wake. Katika mwanzo sura ya kumi, Bibilia inaorodhesha kizazi cha wanadamu. Kila mtu alitambulishwa na babake alikuwa ni nani msingi ukiwa ni uhusiano wa kifamilia. Hivi ndivyo ufalme wa Mungu unavyoendeshwa. Nimrodi alijulikana kama mwindaji hodari na kiongozi hodari.

> Alikuwa hodari kuwinda wanyama (mbele)[48] za Bwana; Kwa hiyo watu hunena, Kama Nimrodi, hodari wa kuwinda wanyama mbele za Bwana. (10) Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari. (11) Akatoka katika nchi ile akaenda mpaka Ashuru, akajenga Ninawi, na Rehoboth-iri, na Kala; (12) na Reseni, kati ya Ninawi  na Kala, nao ni mji mkubwa. Mwanzo 10:9-12 NIV

Nimrodi akiongozwa na kutokuwa salama, aliona haja ya kujionyesha. Kwa hivyo aliaanza kujenga miji na pia alianza kujenga majeshi ili kuyashinda makabila yaliyomzunguka. Mwanahistoria hodari ananena:

---

[47] Mwanzo 10:10 NIV

[48] Neno *mbele* linaweza somwa kama *dhidi*..

> Mamlaka ya viongozi waliopita imekuwa juu ya hisia za kifamilia, na kupanda kwa mfalme ilikuwa ni mfano wa uzuifu wa malezi ya wazazi. Nimrodi kinyume, alikuwa mkubwa katika jimbo, na watu walikuwa makaazi tu bila kujali uhusiano wowote. Kwa hiyvo, kulikuwa na makabila makubwa – familia – na jamii; sasa kulikuwa na nchi, jamii ya kisiasa na serikali.[49]

Karibu ulimwengu wote leo umefuata nyayo za Nimrodi. Nchi leo ni za kisiasa na za kimajimbo, si za kikabila wala kuhama hama. Ni vizuri kutambua njia zilizofuatwa na Nimrodi ili kujenga mtindo huu wa nchi ya kisiasa. Mungu ameuita mtindo huu kwa nchi ya kwanza aliyoijenga ambayo inaitwa Babeli. Angalia vile Babeli ilivyoendelezwa katika moyo wa wanadamu.

1. Inaanza na watoto ambao wameachiliwa na baba zao.
2. Kisha kwa sababu ya kutokuwa na usalama, kila mara wanatafuta kibali.
3. Hii tamaa ya kutaka kibali inawasukuma watu kufanya mambo huzuni ili kulipia upweke wao na kutokuwa na thamani.

Hiki ndicho kiungo cha siri ambacho kinacho tengeneza mvinyo wa Babeli ambao ni wa kufunga watu. Ni kina nani kati yetu ambao hawajapata janga la hisia za kutokuwa na thamani, au juhudi za kuwaonyesha wengine tunacho kile kinacho hitajika? Wangapi kati yetu ambao wamehisi juhudi zetu za kumpenda Mungu kuwa ni za kuanguka kamili na hakuna haja ya kujaribu tena? Wangapi kati yetu ambao wamepatikana na kung'ang'ania mamlaka kazini, shuleni au kanisani na wamesikia au kunena maneno ya hasira au maneno ya kukata kama njia ya kujikinga au katika kujaribu kupanua ufalme wetu mdogo. Je, ulimwengu wote haunywi katika kikombe hiki? Je, kama tunafanya hivyo, sisi si kwa kweli watumwa wa Babeli?

Kwa hivyo maana ya kuanguka kwa Babeli ni nini? Kauli, "Babeli imeanguka," inatoka moja kwa moja kwa Yeremia 51:8 na inapata muktadha wake katika Yeremia 50 na 51. Katika Yeremia 50, Mungu anaelezea watu wake wamepotea kama kondoo ambao wamepotezwa na wamesahau mahala pao

---

[49] A.T Jones, *Empires of the Bible*, (Review and Herald Publishing, 1904) uk. 51.

pakupumzika. Watu wa Mungu wameshikwa mateka na Babeli na wamesahau nyumbani kwa kweli, mahali pa pumziko. Lakini Mungu hajawasahau wana wake. Anatoa ahadi hii nzuri.

> Bwana wa majeshi asema hivi, Wana wa Israeli, na wana wa Yuda, wameonewa pamoja; na wote waliowachukua mateka wanawashika sana; wanakataa kuwaacha. (34) Mkombozi wao ni hodari; Bwana wa majeshi ndilo jina lake; yeye atawatetea kwa bidii, apate kuistarehesha nchi, na kuwasumbua wakaao katika Babeli. Yeremia 50: 33, 34

kisha katika sura ya 51 tunasoma hivi:

> Kimbieni kutoka kati ya Babeli, kila mtu na ajiokoe nafsi yake; msikatiliwe mbali katika uovu wake; maana ni wakati wa kisasi cha Bwana, atamlipa malipo. (7) Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa Bwana; kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa na wazimu. (8) Babeli umeanguka na kuangamia ghafla; mpigieni yowe; twaeni zeri kwa maumivu yake; ili labda apate kuponywa. (9)Tungependa kuuponya Babeli, Lakini haukuponyeka; Mwacheni, nasi twendeni zetu, Kila mtu hata nchi yake mwenyewe; Maana hukumu yake inafika hata mbinguni, Nayo imeinuliwa kufikilia mawinguni. (10) Bwana ameitokeza haki yetu; Njoni, tutangaze katika Sayuni Habari za kazi ya Bwana, Mungu wetu. Yeremia 51: 6-10

Kwa muktadha wa sura hii, Watu wa Mungu wameshikwa mateka na Babeli. Wamepotoshwa, lakini Mungu anaenda kuwakomboa, si kana kwamba wanastahili lakini ni kwa sababu wao ni watoto wake.

Ingawa kauli, “Babeli umeanguka,” ni kauli ya hukumu na mapatilizo, pia ni ahadi ya uhuru kwa Israeli, kwa kuwa Babeli imeshika Israeli mateka.

Babeli iliyoko katika ujumbe wa malaika wa pili inawatoa Israeli wa Kiroho katika mashaka, kutokuwa na thamani na roho ya uzuifu ambayo inatulazimisha sisi kutenda dhambi tukitambua ya kwamba tumekubalika katika Mpendwa, na kwa kweli sisi ni wana wa Mungu kwa kupitia kafara ya

Yesu, kutokuwa na usalama kwote na kutokuwa na thamani zote zinafagiliwa mbali, na tunasimama huru kama wana wa Mungu.

Ujumbe wa malaika watatu pia unaitwa Ujumbe wa Eliya, na pia si ajali kwamba mwisho wa ujumbe huu katika Malaki 4:6 inasema kwamba Mungu atageuza mioyo ya baba iwaeleke watoto wao, na mioyo ya watoto iwaeleke baba zao. Hivi ni kusema kwamba nguvu za huu ujumbe zitaachiliwa wakati tutaamini kwa kweli sisi ni wana wa Mungu, sio kwa kile tulichokitenda, bali kwa kile Yesu ametutendea.

Achana na Babeli na mafundisho yake ya kiini cha Dura. Usibaki kuwa mtumishi lakini lia “Abba Baba” na ujuwe wewe ni mwana wake mpendwa. Kwa kupitia kwa Kristo, Tuko huru.

**Vita vya utambulisho ni safari ya kujitambua binafsi. Ni makaribisho ya kujifunza kuhusu thamani yako katika muktadha wa mahusiano.**

**Maisha yetu yameshambuliwa na kelele ya ujumbe wa mara kwa mara ambao hutuambia kwamba mafanikio huja tu kutokana na kujidhibitishia wenyewe na kuthibitishia ulimwengu kuwa tuna kila kinachohitajika, kuwa tuna mambo sawa. Ni mfumo ambao hutufunza kuhisi kuwa na thamani na umuhimu wakati ambao tumefaulu na kufanikiwa kwa kiwango fulani. Matokeo ya mfumo huu yako na ushahidi kuwa sio mazuri. Mamilioni wako katika dhiki na mamia yanamaliza maisha yao katika kukata tamaa.**

**Nakukaribisha ujifunze hali ya kweli ya vita tulivyo ndani yake – vita vya utambulisho wa kile kinachofafanua thamani yetu na karama. Vigingi viko juu kwa kuwa ni uzima na mauti. Kitabu hiki kina safari yangu na kanuni nilizojifunza njiani. Uhuru ni kitu ambacho hutegemea lakini kitabu hiki kinaelezea barabara yangu kwa uhuru.**

**Adrian Ebens**
**fatheroflove.info**